**16 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 16 Mei, 2024**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya Mwaka 2023.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. AMINA ALLY MZEE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu karibu. Sasa namuita Mheshimiwa Saasisha Mafuwe uliza swali lako.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Waziri tunaishukuru Serikali imetupelekea fedha nyingi sana kwenye miradi ya mwaka wa fedha ambao tunao tunamalizia lakini sasa hivi tunaendelea kupitisha bajeti ya Wizara mbalimbali kwa mwaka wa fedha unaokuja lakini bado kuna miradi michache ambayo tuliahidi kwa wananchi kwamba Serikali itatekeleza hususan miradi ya Wizara ya Kilimo ile ya umwagiliaji, Wizara ya TAMISEMI, barabara ambazo tumeahidi kwa wananchi. Je, Serikali ina mpango gani sasa leo tuko mwezi wa tano kuhakikisha ile miradi ambayo michache iliyobaki tunaenda kuitekeleza na kuimaliza ili kuendelea kuwahakikishia wananchi matarajio yao kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan miradi yote itekelezwe kwa kiwango ambacho tumepitisha kwenye bajeti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mbunge wa Hai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inaendelea kutekeleza bajeti yake huku tukitengeneza miradi mbalimbali ya kimkakati na ile ambayo inatoa huduma kwa jamii yetu. Tunaenda kukamilisha mwaka wa fedha mwezi ujao mwishoni mpaka tarehe 30 na kwa mujibu wa kikao chetu cha mwisho kati ya Kamati ya Uongozi inayoundwa na Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge pamoja na Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imetuhakikishia kupeleka fedha kwa kila wizara kulingana na maombi yao ili kuendelea kukamilisha kazi zote ambazo zilikuwa zimepangwa za mwaka huu wa fedha ambao unaoishia tarehe 30 Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba miradi yote iliyoratibiwa na wizara zote ikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara zote zilizoomba fedha na kupitishiwa na Bunge lako Tukufu, fedha hizo zitatolewa na kwenda kwenye Wizara husika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yote. Hayo ndio majibu ya msingi kwenye hili swali ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwepo na mgongano wa kisheria kati ya Sheria ya Madini na Sheria ya Ardhi, ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Madini mmiliki wa leseni anayo haki ya kulinda eneo lake na kuzuia wenyeji kulitumia bila yeye kuridhia. Pia Sheria ya Ardhi inampa haki mmiliki wa ardhi kutokunyangangwa ardhi hiyo bila fidia. Kutokana na mgongano huo hata pale mmiliki wa leseni anapoamua sasa hataki hilo eneo baada ya miaka mingi hakuna sheria inayomtaka aweze kulipa fidia kwa kuchelewesha matumizi hayo, matokeo yake maeneo mengi zaidi ya miaka 20 yameshikiliwa na wawekezaji na wananchi wamekosa fidia. Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba kuna haja ya kupitia sheria hizi mbili ili kutoa haki kwa wananchi ambao sasa wanakaa kwenye mgogoro mkubwa na wawekezaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nimemuelewa vizuri anataka kujua mgongano uliopo sasa wa wamiliki wa ardhi waliopewa vibali na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sheria ya Wizara ya Madini ambayo inatoa haki kwa wachimbaji, wafanya utafiti wa madini ambao vipo chini ya ardhi. Hapa tunazo sheria mbili, sheria inayomwongoza mwananchi anayetaka kutumia ardhi kwa ujenzi kilimo na shughuli za kawaida juu ya ardhi kwa sababu tunazo sheria mbili ya juu ya ardhi na ile ya chini ya ardhi ambapo kuna rasilimali madini inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, migongano iliyopo sasa kwenye maeneo yetu ni pale ambapo mwananchi amejenga, mwananchi amelima mazao mbalimbali lakini eneo hilo hilo linatolewa kibali cha uchimbaji chini ya nyumba, chini ya shamba lake. Sasa nini kinatokea? Ni kwamba inapotolewa leseni ya utafiti wa madini ambayo yako chini ya eneo la ujenzi wa nyumba na mashamba na huku juu kuna shamba limepandwa lina mazao lakini kuna nyumba basi huyu wa chini wa madini anawajibika kumpa fidia huyu aliyeko juu, kwa mujibu wa sheria ya sasa ambayo tunayo na imeendelea kutuletea migogoro maeneo kadhaa kwa sababu hao walioko juu wanaona wanayo haki pia kule chini lakini kwa mujibu wa sheria hapa tuna sheria zetu mbili ambazo zinaonekana zinagusa sana watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi kwa sasa inafanya mapitio ya sera yake ili ipelekee kuunda sheria tena na kwa kuwa baada ya sera hii kukamilika tutakapokuwa tunatengeneza sheria itakuja hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kuliona hili na kutoa mchango wetu wa mawazo kwa uzoefu tunaoupata kwenye maeneo tunapotoka ya migogoro hii kati ya wamiliki wa ardhi eneo la juu linalotumika kwa ujenzi na mashamba na wale wanaopata leseni kwa sheria za umiliki wa ardhi ya chini ambapo kuna madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutakapokamilisha uandaaji wa sera hii ya Wizara

ya Ardhi ambayo pia itakuja kubaini maeneo haya na kuitengenezea sheria tutakuja kuliangalia kwa kina zaidi tukiongozwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ambayo pia nyenyewe itaanza kutuongoza namna nzuri ya ya kutengeneza ambayo sheria ambayo haitakuja kutuletea migongano. Kwa sasa kwa sheria tuliyonayo inapotokea mtu anapata kibali cha madini, basi huyu hutoa fidia kama kuna mtu yeyote hapa juu ana nyumba, ana mashamba au vinginevyo, hiyo ndiyo sheria ambayo kwa sasa tunayo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na mlundikano mkubwa wa madeni kwa watumishi wetu na madeni hayo yanatokana na stahiki zao mbalimbali, ikiwemo likizo, uhamisho na mengine mengi. Madeni haya pia yanawapunguzia watumishi wetu morali ya utendaji kazi. Ni nini kauli ya Serikali ya kuhakikisha inaondoa kadhia kubwa iliyopo kwa watumishi wetu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Majala, Mbunge wa Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo watumishi wa umma ambao wana stahiki zao na yapo maelezo thabiti ya kila mtumishi wa umma anapokuwa na stahiki lazima alipwe. Serikali inaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba haitengenezi kadhia inayompunguzia morali ya kufanya kazi kwa mtumishi yeyote. Najua yako madeni katika maeneo mbalimbali na mimi nimepata kufanya kazi ya Chama cha Wafanyakazi cha Walimu, uzoefu wa maeneo ya madeni ni pale ambapo mtumishi hupanda daraja na anatakiwa kulipwa maslahi mapya lakini tukachelewa kidogo kukatengeneza deni tunaita *arrears*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yako madeni ya watumishi wanapotakiwa kwenda kusoma zipo stahiki zao, matibabu na vitu

kama hivyo. Serikali katika kipindi cha miaka mitatu hii imefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan kati ya eneo ambalo amelitolea msisitizo ni kuhakikisha kwamba watumishi wetu wote wenye stahiki ya aina yoyote ile lazima walipwe kwa wakati. Nasi tumesisitiza, Wakuu wa Idara, Vitengo na wale wenye dhamana ya malipo wahakikishe kuwa kwanza tufanye uhakiki wa wote wenye madeni ya watumishi wetu kila idara na kazi hiyo tulishakamilisha na malipo tunaendelea kuyalipa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua inawezekana pia bado shughuli zinaendelea na madeni yanazalishwa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba amini kwamba Serikali inaendelea kufanya jukumu hilo la kuhakikisha kwamba tunalipa madeni ya maeneo yote baada ya kuwa tumefanya uhakiki na yako maelekezo maalum kwa sekta za kazi kwenye Halmashauri, Wizara kuendelea kuhakiki na kuratibu vizuri ulipaji wa madeni haya. Yapo madeni yanalipwa kutoka Serikali Kuu nayo pia tunapeleka fedha kwa ajili ya ulipaji, yako madeni ambayo yanalipwa kwa ngazi husika tumeshawaambia waweke kwenye mipango yao ya bajeti ili madeni hayo yaweze kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zote hizi ni kuhakikisha kwamba watumishi hawavunjiki moyo katika kufanya kazi kwa kudai madai yao, stahiki zao kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, tunaendelea kuhakikisha kwamba madeni haya tunaendelea kuyalipa na sasa tumejikita pia kulipa hata mafao ya wafanyakazi waliomaliza muda wao, wale wastaafu kupitia taasisi yetu *PSSSF* na kazi hiyo inaendelea vizuri na wale wachache ambao bado hawajalipwa nataka niwahakikishie kuwa malipo yao ambayo ni stahiki yao yatalipwa kama ambavyo Serikali tumejipanga, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na ongezeko la kodi na ushuru mbalimbali wa halmashauri katika sekta ya madini hapa nchini na hivyo kupelekea kuongeza gharama kubwa za uzalishaji

kwa wachimbaji wadogo wadogo na kupelekea wachimbaji wadogo wadogo kutafuta njia mbadala ikiwemo hata kukwepa kodi. Nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha ya kwamba inaondoa asilimia moja ambayo hutumika kama ada ya ukaguzi kwenye asilimia saba inayokusanywa kama mrahaba ili iiache asilimia moja kwenye halmashauri zetu na halmashauri iweze kuondoa kodi na ushuru hizi ili iwaondolee wachimbaji wadogo wadogo mzigo mkubwa ambao unawakabili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi sikumsikia vizuri na pia sikumwelewa naomba arudie swali lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassim, rudia tena swali lako.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na ongezeko la kodi na ushuru mbalimbali kwenye halmashauri katika sekta ya madini na hivyo kupelekea kuongeza gharama za uzalishaji kwa wachimbaji wadogo wadogo na kupelekea wachimbaji wadogo wadogo kutafuta njia mbadala ikiwemo kukwepa kodi. Nini kauli ya Serikali katika kupunguza asilimia moja ambayo hutumika kama ada ya ukaguzi kwenye asilimia saba inayokusanywa kama mrahaba ili asilimia moja ile iweze kubaki kwenye halmashauri zetu na halmashauri ziweze kuondoa kodi na ushuru huu ambao ni mzigo mkubwa kwa wachimbaji wadogo wadogo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wachimbaji wadogo wadogo kwenye sekta ya madini ambao Serikali kupitia Wizara yetu ya Madini imejielekeza katika kuhakikisha kuwa majukumu haya wanayatekeleza kila siku yanawaletea tija kwenye shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia tozo mbalimbali kwa wachimbaji wadogo zinazoandaliwa na Wizara ya Madini pamoja na TAMISEMI. Naomba nimfahamishe kwamba sasa hivi tunalo zoezi la kufanya mapitio ya aina zote za tozo zinazotolewa kwenye halmashauri zetu kupitia Wizara za kisekta ambazo zinagusa sana wajasiriamali wadogo wakiwemo wafanyabiashara wadogo wadogo ambao pia kwenye sekta ya madini kuna wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mapitio haya ambayo bado yanaendelea na yatakamilika baada ya muda mfupi na kwa kuwa leo limetolewa swali hili, basi nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kufanya mapitio na tunapokamilisha naamini hili pia tunalichukua kuwa sehemu ya ushauri ambao tutaufanyia kwenye mabadiliko hayo ili kuweza kuwafanya wachimbaji waweze kutekeleza majukumu yao kama wanapaswa kulipa kodi, basi tutambue kodi hiyo na halmashauri pamoja na Wizara ya Madini tujue mapato yao yatakuwaje? Hayo ndio majibu ya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwepo na leseni za uchimbaji madini katika maeneo mbalimba nchini kwa kupitia njia ya mitandao. Leseni hizi zimekuwa zikienda katika maeneo ambayo yanamilikiwa na wananchi kwa muda mrefu kama makazi, mashamba, na hata maeneo ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa ambao wamekuja kumiliki leseni hizi wamekuwa au wakiingia ubia na watu mbalimbali au wakiuza kwa mara nyingine na hivyo kuwafanya wamiliki wa awali kubaki masikini. Nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha wananchi mbalimbali ambao ni wamiliki wa awali wa maeneo haya wanajengewa uwezo ili waepukane na wimbi la umasikini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena Mheshimiwa Mbunge aliulize vizuri halafu niweze kutoa majibu sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, rudia swali lako.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwepo na upatikanaji wa leseni za uchimbaji madini kwa kupitia njia ya mtandao. Leseni hizi zimekuwa zikienda kugusa maeneo ambapo awali wananchi kwa muda mrefu wamekuwa wakiyamiliki, mfano, mashamba, maeneo ya mifugo na hata makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa baada ya kumiliki maeneo hayo wamekuwa wakiingia ubia au wakati mwingine kuyauza na kupata fedha nyingi kiasi cha kwamba wale waliokuwa wamiliki wa awali wamebaki katika wimbi la umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha wanawasaidia wananchi wetu hasa pale madini yanapogundulika katika maeneo mbalimbali nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, hilo swali lako ni la kisekta. Lipeleke kwenye sekta husika na Serikali wamekusikia hapa, watakusaidia majibu sahihi. Mheshimiwa Mariki. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inafanya kazi nzuri na kubwa kujenga miundombinu ya elimu na kuhakikisha kwamba elimu inafika nchini kote; lakini kumekuwa na changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu, hali inayopelekea baadhi ya wanafunzi kupanga mitaani na kuhatarisha usalama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta sera ya ulazima kuhakikisha kwamba inajenga mabweni katika kila shule ya sekondari ili kuwasaidia wanafunzi hawa, hususan watoto wa kike ambao wamekuwa wakipata changamoto kubwa njiani?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba wakati mtu anatoa hoja yake msipige makofi. Meza haisikii na mjibu maswali naye anapata taabu kusikia. Ngojeni mpaka majibu yakitolewa ndiyo mtaweza kupiga makofi. Nawaomba sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariki, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango Kazi wa Wizara ya Elimu katika ujenzi wa miundombinu ya sekta ya elimu na hasa sekondari, tumeanza hatua kadhaa za maboresho ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanajua kwamba katika mpango wote wa maendeleo, upo mpango wa muda mfupi, wa kati na mpango wa muda mrefu. Kwenye ujenzi wa shule za sekondari, tumeanza hatua za muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka tulipokuwa tunafanya maboresho ya ujenzi wa shule za sekondari, tulianza na shule za Tarafa. Tukaona bado umbali wa kufikiwa na vijana wetu ni mkubwa, tukaanza na zoezi la ujenzi wa shule kila Kata. Zoezi hili limekamilika. Tuna zaidi ya 90%, na kila Kata hapa nchini ina shule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye ujenzi wa shule hizi tulianza na ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu. Tumeendelea kujenga maabara na kuimarisha ujenzi wa nyumba za walimu na sasa tunaanza kujenga shule za bweni ambazo zinahitaji kujenga mabwalo na mabweni. Kazi hii ndiyo tuliyonayo sasa ya kujenga mabweni kwa baadhi ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwenye maeneo yao. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi sana za ujenzi kwenye miundombinu ya elimu ikiwemo na sekondari. Pia, tumeshajenga hata shule maalum iliyokamilika pamoja na mabweni kwa kila mkoa. Hiyo ni mikakati ya kwenda kujenga mabweni kwenye

shule zetu za sekondari ili kupunguza umbali kwa wanafunzi ambao wanatoka mbali, iwe ndani ya Kata au Kata jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya hivi katika kila sekta kwa mahitaji ambayo yanahitajika kwenye maeneo haya. Tumeanza maabara, sasa tunajenga mabweni na mabwalo. Malengo yetu ni kila shule ya sekondari iwe na bweni ili wanafunzi waweze kulala huko, wasome huko, wacheze huko na inakuwa rahisi zaidi kumpa nafasi ya kusimamia zaidi kwenye masomo yake na kuongeza ufaulu kwenye shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inaendelea na mpango wake wa ujenzi wa mabweni kwenye shule zetu na kama ambavyo tumeanza kujenga shule zilizokamilika. Sasa shule zile ambazo hazikukamilika Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kifupi kijacho tunaamini tutaweza kukamilisha kujenga mabweni kwenye shule zetu karibu zote ili kuruhusu siyo tu wasichana, pia hata watoto wa kiume (wavulana) ambao pia wanasoma, kuwapunguzia umbali na kupunguza adha inayowapotezea nafasi ya kusoma zaidi wanapokuwa wanapata elimu hiyo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu umetoa ruksa kwa watu wake kusafiri ndani na nje ya nchi ilimradi wametimiza vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu kwa kuhangaika kutafuta ajira kama walivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, watafute ajira kokote ndani au nje. Vijana hawa wanakuwa wamepata *VISA*, wana tiketi, wanajua wanakokwenda, wanakwenda kuhangaika kutafuta Maisha, lakini wamekuwa wanapata vikwazo vya kuzuiliwa katika viwanja vyetu vya ndege kutimiza ndoto zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wanapokwenda nje ambako wanapata hiyo ajira, vilevile kunachangia kuleta *remittance* kwa nchi na familia zao. Tumeona wenzetu majirani, wanaoruhusu vijana wao kusafiri dunia nzima jinsi wanavyofaidika na *remittance* za vijana wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi hizi ambazo zimekuwa kero kubwa. Sasa nini kauli ya Serikali ili kuwaondolea usumbufu vijana wetu hawa ambao hawajaonekana na matatizo, wametimiza masharti yote, lakini wanakatishwa kutimiza ndoto zao na yale ambayo wamekusudia? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshua, Mbunge wa Zanzibar kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vyote vya ndege ulimwenguni vinazo sheria za kimataifa kwa ajili ya usalama wake na hasa kwenye nchi viwanja hivyo vilipo, vinataka kila anayesafiri na kutumia viwanja vya ndege awe amekamilisha masharti ya kiusalama kwa nyaraka zake, lakini pia hata anaposafiri na aina yoyote ya mizigo yote lazima iwe salama. Huo ni wajibu wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo kwenye viwanja vya ndege kusimamia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wetu unaonyesha, tukichukua mfano hapa nchini kwa vijana ambao wanataka kusafiri, tunayo Idara ya Uhamiaji, ndiyo idara nambari moja ambayo inahakiki uhalali wa yeye kutoka ndani ya nchi kwenda nje ya nchi na uhalali wa abiria yeyote anayetoka nje ya nchi kuingia ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, viko vyombo vingine vya usalama vinavyojiridhisha kwamba abiria huyu anatoka akiwa salama asije akaaibisha Taifa letu, lakini abiria huyu anaingia nchini akiwa salama, asije akahatarisha usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vyombo hivi vinao wajibu wa kufuatilia mwenendo wa abiria yeyote yule anayesafiri kwa lengo la usalama tu na wala siyo usumbufu. Hivyo basi, pale ambapo vyombo hivi vinakuwa na mashaka kwamba abiria huyu anayo mashaka mashaka, basi vyombo hivyo hufanya kazi yake. Pale inapothibitika, hawezi kumruhusu kusafiri kwa sababu anatakiwa asafiri akiwa salama. Kama ana nyaraka zote, anaweza kusafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inawezekana pia yako hayo matatizo kwenye viwanja vyetu vya ndege. Mimi nawasihi vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea kutoa huduma kwa weledi, kuhakikisha kuwa wale wote ambao hawana mashaka, wana nyaraka zao zimekamilika, waendelee na safari zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona watu wanasafiri, wanaingia nchini lakini wale wote ambao wana mashaka wataendelea na taratibu zao. Huku pia kwa abiria wanaosafiri ni muhimu kila abiria kujiridhisha kuwa kwanza ana nyaraka zote lakini pia asiwe na vile vifaa vyote ambavyo vinavyotakuwa visipite au visibebwe na abiria anaposafiri kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta kila uwanja wa ndege wametoa orodha ya vifaa ambavyo abiria wanazuiwa kuvibeba na wameweka mahali ambako wewe unatakiwa kuvitunza ili utakaporudi uvikute kama ni lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, usalama wa wasafiri wa viwanja vya ndege umeimarika na tunaamini wasafiri wote sasa watazingatia masharti ili kuwawezesha kusafiri safari zao bila usumbufu wowote, waende huko kupata ajira, kufanya shughuli zao, kusalimia ndugu na wale wanaokuja nchini, tujiridhishe kwamba abiria wote wanaoingia nchini kwetu kutoka nje ya nchi wako salama na kutohatarisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo majibu ya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hujaniona huku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na utabiri wa hali ya hewa wa kutahadharisha juu ya majanga mbalimbali ikiwemo hili janga la vimbunga. Kwa bahati mbaya sana, hivi karibuni tumeona kwamba majina hayo mengi yamekuwa ni ya jinsia ya kike, kama Kimbunga Cleopatra, Kimbunga Caterina na hivi karibuni Kimbunga Hidaya, lakini hatujasikia Kimbunga John, Kimbunga Getere au Kimbunga Kanyasu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hilo kwa masikitiko makubwa, nikisema kwamba hamuoni sasa iko haja kwa Serikali, haya majina yakiletwa kutoka nje yabadilishwe au myatohoe ili yalete maana nzuri? Vijana wetu wanaingia katika kutoa kashfa kwa kutumia haya majina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe maoni yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, kaa tu. Viko vimbunga vina majina tofauti. Kuna Kimbunga Fred. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa muda wako. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, kwa niaba Mheshimiwa Mabula.

Na. 352

**Kujenga Barabara za Mitaa Kisesa Bujora – Magu**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA K.n.y. MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara za Mitaa kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kisesa – Bujora – Magu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Mawaziri, mfanye kama anavyofanya Mheshimiwa Katimba, hata hajaitwa anakuja, kwa sababu ana hamu ya kujibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa sita kwa kiwango cha lami pamoja na uwekaji wa taa za barabarani katika Mji wa Kisesa – Bujora – Magu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara za Wilaya ya Magu kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiswaga kwa niaba ya wananchi wa Magu, anashukuru sana kwa majibu ya Serikali na ni imani yake kwamba fedha hizo zitakwenda kwa wakati na zitatatua changamoto zilizopo pale Kisesa – Magu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali inaonesha dhamira ya dhati kupeleka fedha sasa kwa ajili ya kukamilisha miradi ambayo imeshaanza, kuna barabara zenye

kilometa 12 ambazo zinahitaji fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu mpaka nne. Serikali iko tayari kuhakikisha barabara hizi za Mkolani – Sauti, Sauti – Luchelele na barabara ya kutoka Bugarika – Mahina, zinakamilika kwa kiwango cha lami kwa sababu zilishaanza kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mpango wa uboreshaji wa barabara katika Jiji la Mwanza katika Jimbo la Nyamagana. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya Mkolani – Sauti, Sauti – Luchelele na Bugarika, imepandishwa hadhi sasa kutoka kwenye kiwango cha barabara ya changarawe kwenda lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, imetengewa shilingi bilioni moja na milioni sitini na moja. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba barabara alizozitaja zinaendelea kujengwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa haraka kukamilisha ujenzi wa barabara za lami kwenye Mji Mdogo wa Katesh ambao kwa sasa uko 30% ya kilometa 10 iliyoahidiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inajenga barabara zote hizi za wilaya ili kuwasaidia wananchi kufikia huduma za kijamii na

kujenga Uchumi, kwa maana wananchi waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa ikiwemo barabara katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Kamamba.

Na. 353

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara – Kakonko**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. ALOYCE J. KAMAMBA,** aliuliza: -

Je, lini ahadi ya ujenzi wa barabara ya kilometa tatu kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kakonko itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA),** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi mwaka 2020 kuhusu ujenzi wa barabara katika Mji wa Kakonko kwa kiwango cha lami kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kilometa 1.83 zimeshakamilika na kilometa moja inaendelea kujengwa na ujenzi umefikia 58.7%. Utekelezaji wa ujenzi huu umekuwa ukifanyika kwa awamu ambapo mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilometa 0.63 kwa kiasi cha shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilometa 1.2 kwa

shilingi bilioni moja ulifanyika na mwaka 2023/2024. Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilometa moja kwa shilingi bilioni moja. Aidha, katika mwaka 2024/2025, Serikali imeweka katika mipango yake ya bajeti, kujenga kilometa 0.17 kwa kiwango cha lami ili kukamilisha urefu wa kilometa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya Wilaya ya Kakonko ikiwemo Barabara za Mji wa Kakonko kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni lini Serikali itajenga barabara ya Kakonko – Kabare hadi Muhange kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itajenga Daraja la Mto Mkoza kuunganisha Kata ya Mbanga na Lusaba katika Jimbo la Buhigwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara ambayo ina kipande cha *TANROADS* na ina kipande cha *TARURA*. Kipande cha barabara ya *TANROADS* ni kilometa 34.5 na kipande cha *TARURA* ni kilometa 8.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kile kipande cha *TARURA* ambacho kinatokea Gwarama, Kabare mpaka Muhange tayari katika bajeti kimeshawekewa fedha na kwamba kitajengwa na tena kinachongwa na kuwekwa changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itahakikisha kwamba inajenga barabara hii kwa upande wa *TARURA* lakini kwa upande wa *TANROADS* na wenyewe wataendelea kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusiana na kujenga Daraja la Mto Lukoza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshatenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili ili kuunganisha kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Bujela - Masukulu mpaka Matwebe ni barabara inayohitaji kuwekewa lami na ni barabara korofi. Ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kijenga barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mkubwa sana wa barabara aliyoitaja na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kuja kujenga barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Na. 354

**Kutengeneza Barabara za Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ambazo zimeharibika Wilayani Chunya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza bajeti ya *TARURA*, Wilaya ya Chunya kutoka shilingi milioni 744.35 mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 2.24 mwaka 2023/2024. Aidha, Wilaya ya Chunya imepokea fedha ya dharura shilingi milioni 160 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili kufanya matengenezo ya baadhi ya barabara ikiwemo za Nkung`ungu na Kalungu zilizoathiriwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali ina mpango wa kutumia shilingi bilioni 2.24 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara mbalimbali katika Wilaya ya Chunya zenye jumla ya kilometa 148 na ukarabati wa madaraja mawili. Serikali itaendelea kuuhudumia mtandao wa barabara wa Wilaya ya Chunya kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini tunaishukuru Serikali pia kwa kutuongezea bajeti kutoka bilioni shilingi milioni 700 mwaka 2019/2020 mpaka bilioni 2.2 tunashukuru sana. Pamoja na kutuongezea bajeti hiyo, Wilaya ya Chunya kijiografia ni kubwa sana na ina barabara nyingi na ndefu. Je, Serikali haioni haja sasa kutuongezea bajeti angalau ifike shilingi bilioni tatu ili barabara nyingi ziweze kutengenezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kutokana na mvua ambazo zimeendelea kunyesha kwa mwaka huu na barabara nyingi kuharibika na Serikali kutupatia shilingi milioni 160 ambazo ziliwezesha kutengenezwa kwa barabara mbili ya Kalungu pamoja na Nkung'ungu: Je, Serikali haioni haja sasa kutuongezea fedha ya dharura ili barabara za kwenda Mapogoro - Godima - Sangambi - Mawelo na Matwiga na zenyewe ziweze kutengenezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumwomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani na Serikali, kama hivyo tayari mwaka wa fedha 2019/2020 bajeti ya barabara katika jimbo lake ilikuwa ni shilingi milioni 744.53 lakini mwaka huu 2023/2024 tunazungumzia bilioni 2.24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusudia na ni dhamira yake kuhakikisha kwamba inaongeza fedha ili kuhakikisha mtandao mrefu uliokuwa nao wa barabara hizi za wilaya katika jimbo lako zinajengwa. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge endelea kuipa imani Serikali, itaongeza fedha ili kuhudumia barabara katika jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, tayari fedha za dharura shilingi milioni 160 zimeshaletwa katika jimbo lake kwa ajili ya kuhudumia barabara na hasa yale maeneo korofi. Nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga milioni 226 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara ya Mapogoro – Godima – Isenyela - Mawelo na Matwiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kuzijenga na kuzikarabati barabara zote katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Kipengele kwenda Lupila inaunganisha majimbo matatu Ludewa, Wanging'ombe na Makete. Ni lini Serikali itatoa fedha barabara hii ya kiuchumi iweze kujengwa na wananchi wa Makete waweze kuitumia kwa shughuli zao za maendeleo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, barabara zote ni za uchumi. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari nimezungumza na Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na barabara hii ya Kipengele – Kipila. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tukitoka hapa tutajadili tuweze kuona ni namna gani tunahakikisha barabara hii muhimu inaweza kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 355

**Kutoa Mikopo ya Asilimia 10 Kupitia Halmashauri**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza tena kutoa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ilisitishwa mnamo tarehe 13 Aprili, 2023 kufuatia maelekezo ya Serikali ya kuangalia upya utaratibu wa utoaji wa mikopo kutokana na changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniaameridhia kurejesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia Julai, 2024. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kukamilisha maandalizi ya utoaji mikopo hiyo kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa jitihada za Mheshimiwa Rais kurejesha mikopo hiyo, lakini ningependa kujua sasa yale makosa yaliyosababisha mikopo ikasitishwa, je, yalisababishwa na mkopaji au mkopeshaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Je, Serikali imejiridhishaje na kujipanga kuhakikisha kwamba makosa hayo hayarudii tena?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya CAG ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 alibainisha upungufu kadhaa ambao umejitokeza katika mikopo hii ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na ilibainika zaidi ya shilingi bilioni 89 imeshindwa kurejeshwa kutokana na sababu nyingi ikiwemo vikundi hewa na kuwepo kwa udanganyifu kwa baadhi ya wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kipindi kile Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo, lakini timu iliundwa kufanya mapitio ili kuhakikisha unatengenezwa utaratibu bora zaidi kwa ajili ya kuhakikisha mikopo hii inatoka na inaenda kuwanufaisha walengwa na inaleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba timu ile ipo ukingoni, maandalizi kwa kiwango kikubwa yamefanyika tayari katika muundo wa usimamizi wa hii mikopo. Kutaanzishwa kitengo cha usimamizi wa mikopo katika ngazi ya Wizara kwa maana Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutakuwa na Kamati za Usimamizi wa Mikopo katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri na Kata yote...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ameshakuelewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kuhakikisha kwamba mikopo hii inatolewa kwa ubora zaidi na inaweza kuwanufaisha walengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwa kuwa Serikali inafanya majaribio ya kutoa mikopo hii ya 10% kwa wanufaika je, Serikali ipo tayari sasa kutoa mafunzo kwa wanufaika kabla ya kuanza kutoa mikopo hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mipango ya uboreshwaji wa namna ya utoaji wa mikopo hii ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wanufaika wa mikopo hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, alichokisema ndicho kitakachofanyika. Serikali kweli ipo tayari kuhakikisha inatoa mafunzo kwa ajili ya kuboresha na kuwa na tija katika vikundi hivi ambavyo vitapokea mikopo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaingia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Ameir Abdalla.

Na. 356

**Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR K.n.y. MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza: -

Je, kwa vipi Mabadiliko ya Tabianchi yanasababisha uvamizi wa wadudu waharibifu kwa mazao mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimwia Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya athari za mabadiliko ya tabianchi ni ongezeko la joto Duniani. Ongezeko hili la joto Duniani huathiri fiziolojia ya wadudu kwa maana ya mfumo wa ulaji, uzaaji na ukuaji. Aidha, tafiti zimethibitisha kuwa joto na mvua huchochea mabadiliko katika uzaaji, ukuaji na kuenea kwa wadudu waharibifu wa mazao pamoja na magonjwa ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii huchangia ongezeko la aina mbalimbali za wadudu waharibifu wa mazao ambao ni tishio katika uzalishaji na ukuaji wa sekta ya kilimo. Kwa Mkutadha huo, kuna umuhimu wa kuimarisha mifumo na mbinu shirikishi za udhibiti wa wadudu waharibifu ikiwemo ufuatiliaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi na kuenea kwa wadudu waharibifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza majibu hayo mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa sababu mapambano haya ya mabadiliko ya tabianchi yanahitaji ushirikiano wa taasisi mbalimbali ziliyomo ndani na nje ya nchi. Nilitaka kujua ni maeneo yapi ambayo Wizara yako inashirikiana na mamlaka ya hali ya hewa nchini katika mapambano ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili kwa kuwa wadudu hawa wameendelea kusambaa hususan kwenye maeneo ya Visiwa vya Unguja na Pemba, ni lini Serikali itafanya tafiti kujua ni athari zipi zinazopatikana kule kuwaathiri wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa na kwa kuhakikisha kwamba *TMA* inatoa taarifa ya hali ya hewa pamoja na hali hatarishi na kutoa tahadhari ya nini kifanyike ikiwemo kutoa taarifa ya joto kali na uwepo wa mvua nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na *TMA* wapo katika hatua ya uandishi wa andiko ambalo wataliwasilisha Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuhakikisha kwamba wanaweza kufadhiliwa kuongeza vitendea kazi, lakini pia na kuendelea kujenga uwezo wa wataalamu wetu ili tuweze kuwa tunapata taarifa ambazo zinaendana na uhalisia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili, kwa vile Sheria yetu ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 inatambua uwepo wa taasisi za utafiti kwa upande wa Tanzania Bara tukiwa na Kituo cha Umahiri cha Utafiti wa Kilimo na Mazao ambapo kipo *SUA* pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua katika visiwa vya Zanzibar tuna *ZALI* ambao wanafanya utafiti lakini ili kuboresha na kupanua wigo wa ushirikiano katika kuhakikisha kwamba wanatambua changamoto zinazojitokeza, wameanza kushirikiana na wenzao wa *SUA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi nyingine inaitwa *TPRI* na wenyewe wanashirikiana kwa ukaribu sana kuhakikisha kwamba Tanzania tunakuwa na taarifa ambazo zinatoa mwanga na uelekeo wa hatua gani zichukuliwe kulingana na wadudu waharibifu wa mazao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu Mheshimiwa Anatropia.

Na. 357

**Bodaboda Kupata Mikataba Isiyo ya Kinyonyaji**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, kwa kiwango gani Serikali inahakikisha Bodaboda wanapata Mikataba ya pikipiki isiyo ya kinyonyaji kutoka kwa wakopeshaji binafsi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kutoa elimu ya kisheria na namna bora ya kuingia mikataba isiyo ya kinyonyaji kati ya waendesha pikipiki na watoa huduma za mikopo ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasihi waendesha pikipiki wote kutumia fursa zinazotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuomba mikopo yenye masharti nafuu inayoratibiwa na Wizara yangu na kutolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Halmashauri. Aidha, waendesha pikipiki wanaweza kuomba mikopo katika katika taasisi rasmi zilizosajiliwa na Serikali ili kuepuka mikopo ya kinyonyaji inayotolewa na wakopeshaji binafsi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni bodaboda inaajiri vijana wengi sana na wengi kati ya vijana hao wana elimu ya kiwango cha chini lakini pia na Uchumi, hivyo hulazimika kwenda kwa wafanyabiashara na wafanyakazi kukopa pikipiki ili walipe kwa mikopo na hiyo mikopo inaishia kuwa mikopo ya kausha damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu: Ni kwa nini Serikali isije na sera, kanuni na sera maalumu ya ku-*deal* na sekta hii ikieleza majukumu na haki za hawa vijana tofauti na ilivyo leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa sababu ni ukweli kwamba wadhulumiwa, ni kwa nini Serikali isije na *standard contract* ambayo itaeleza *at least checklist* ya *minimum qualification* za mkataba anayopaswa kupata ikiwa ni pamoja na kiwango cha riba *(range)* kwamba pikipiki moja mtu anapaswa kurejesha kiasi fulani mpaka kiasi fulani tofauti; na ilivyo leo ambapo vijana wamekandamizwa wakati ni kundi kubwa la bodaboda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi na swali zuri la mwuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge ni mambo yanayotokea na katika kutokea kwake hayatokei tu kwenye bodaboda. Watanzania tumejengwa kwenye misingi ya undugu na ujamaa, kwa hiyo, tuna tabia ya kuaminiana sana hasa mtu anapokuja na shida, wale ambao wana nafasi ya kutatua, wanatumia shida ile kwa kuweka masharti ambayo baadaye yanakuwa mazito sana kwa yule waliyemsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumepokea jambo hili na tumepokea na mengine mengi kama Serikali, tunaendelea kuyafanyia kazi ili kuweza kuweka mipaka ya hayo masharti tunaposaidiana kama Watanzania. Inatokea mtu anaenda kuomba mbegu ya vitunguu, anaambiwa nitakupa kilo tano lakini utarudisha gunia 10; nitakupa kilo moja, utarudisha gunia 15 baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vitu ambavyo vinakuwa siyo msaada, sana sana vinatengeneza *vicious cycle* kwa Watanzania. Kwa hiyo, tunayafanyia kazi na tutafanyia kazi kwa

ujumla wake kwenye vitu, kwenye fedha, na vitu vingine vyote kama hivi ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevisema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Mwakibete.

Na. 358

**Huduma ya Vitambulisho vya Taifa-Busokelo**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma za utoaji wa Vitambulisho vya Taifa katika Halmashauri ya Busokelo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Halmashauri ya Busokelo jumla ya vitambulisho 36,170 vimezalishwa na kusambazwa kwa wananchi kupitia Ofisi za Kata, Mitaa na Vijiji, ambapo kwa mwaka 2023/2024 vitambulisho 23,230 vimezalishwa na kusambazwa kwenye Kata na Vijiji vya Halmashauri ya Busokelo. Aidha, kati ya hivyo, vitambulisho 19,525 sawa na 84% vimeshachukuliwa na wananchi wa Busokelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi wote ambao bado hawajachukua vitambulisho vyao vya Taifa kufika katika Ofisi za Serikali za Mitaa walipojiandikishia kwa ajili ya kuvichukua. Aidha, tunaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwahimiza wananchi katika maeneo yao kwenda kuchukua vitambulisho vyao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. kwanza naipongeza Serikali kwa kuondoa ukomo wa Kitambulisho cha Taifa kwa sababu vitambulisho vya nyuma vilikuwa na ukomo

wa miaka, lakini sasa wameiondoa na hii inatusaidia kwamba Utaifa wetu unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa kuwa Kitambulisho cha Taifa kimekuwa kikitumika maeneo mengi kama maeneo ya benki maeneo ya sensa na maeneo mengine tofauti tofauti: Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Watanzania wote wanapata vitambulisho kwa wakati katika maeneo ya Wilaya zao kwenye nchi zao ikiwemo Jimbo la Makete na Mkoa wa Njombe na maeneo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi wote wanapata vitambulisho kwa wakati kwa sababu vinahitajika sana kwenye matumizi siku hizi hata kwenye usajili wa laini za simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuzalisha vitambulisho vya Taifa na kugawa kwa wananchi na kuanzia mwezi Oktoba, 2023. Baada ya changamoto ya kadi zile kwisha, sasa uzalishaji umeanza wa kutosha na usambazaji umekuwa wa hali ya juu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Makete, wananchi wake watapata vitambulisho vya Taifa ili waendelee kupata huduma kama inavyokusudiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo. Mheshimiwa Kamonga.

Na. 359

**Ujenzi wa Soko la Samaki Manda - Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini Mkandarasi aliyeteuliwa kujenga Soko la Samaki Manda - Ludewa ataanza kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mwambao wa Ziwa Nyasa. Aidha, uwepo wa miundombinu ya kisasa huwezesha kuwepo kwa mazingira safi, salama ya kuandaa, kuchakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi ikiwemo samaki wenye kukidhi viwango vya usalama na ubora unaotakiwa na masoko ya ndani na nje ya nchi ili kulinda afya za walaji na kuongeza thamani ya mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Aprili, 2024 Wizara ilifanikiwa kukamilisha taratibu za kusaini mkataba wa ujenzi wa soko la Samaki Manda na Mkandarasi *Huydavis and Company Limited* na hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024 mkandarasi huyo alikabidhiwa eneo hilo rasmi kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi wa soko hilo ambapo ujenzi wa soko hilo unategemewa kukamilika ifikapo tarehe 14 Desemba, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali bado nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Makonde hasa akina mama na Lifuma wanapata dagaa kwa wingi sana ila wanakosa teknolojia ya kukausha wale dagaa ili wakubalike soko la ndani na nje ya nchi.

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka mahema ya kisasa yanayoweza kukausha kwa kutumia umeme wa jua au wa *TANESCO*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine, ningependa kuishukuru Serikali kwa kuleta zoezi la uhimilishaji ila halijakubalika. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka madume bora manne tuweze kwenda kukaa nayo kule kwa muda fulani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na huu utaratibu wa kukausha dagaa katika mwambao wa maziwa yetu yote makubwa na madogo lakini utaratibu huu umekuwa ni utaratibu wa kizamani sana. Kwa hiyo, Serikali kupitia taasisi ya utafiti *TAFICO* ilifanya utafiti na kugundua kwamba dagaa hao wanaandaliwa kienyeji na wanakuwa hawaandaliwi vizuri. Kwa hiyo, ikaja na mfumo rasmi wa kuandaa matenti ambayo kazi yake yatakuwa ni kukausha dagaa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba matenti haya kwa utaratibu huu mpya yako ndani ya bajeti ambayo juzi mlipitisha. Namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya bajeti kuanza kutekelezwa tutampelekea jimboni kwake kwa ajili ya hao akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la madume, tulikuwa na utaratibu ambao wafugaji wetu tulikuwa tumeuweka katika vituo atamizi. Tulikuwa tunawaelekeza waende kwenye vituo atamizi, viko vituo atamizi ambavyo tulikuwa tunavitumia kama Wizara. Ukienda kule Kituro kuna kituo atamizi, ukienda kule Mwabuki Misungwi kuna kituo atamizi, ukienda hapa *NARCO* Kongwa kuna kituo atamizi. Kwa hiyo, tulikuwa tunawashawishi wafugaji waende kwenye vituo atamizi kwa ajili ya kupata mbegu bora lakini tukagundua kwamba wafugaji hao wanatembea umbali mrefu sana kufata zile mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Wizara tumekuja na mpango, Mheshimiwa Mbunge uki-*organise* wafugaji wako ukatuambia una wafugaji 20 au 30, sisi Wizara tunakuletea madume mpaka nyumbani kwako. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba madume hayo manne unayoyaomba leo hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuko tayari kukuletea, ukishakuwa tayari tupe taarifa tutakuletea mpaka kijijini kwako yatakuja

yatafanya kazi maalum na yakimaliza hiyo kazi maalum yatarudi kuendelea na shughuli nyingine kwa sababu madume hayo yapo kwa ajili ya kazi maalum ya kupandikiza mbegu kwa ajili ya kuleta ng'ombe wenye viwango vinavyotakiwa, ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Mwalo wa Kirando umezama kulingana na mabadiliko ya tabia nchi. Ningependa kufahamu kuna mkakati gani mwingine wa kujenga soko jipya la samaki Kata ya Kirando?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anavyosema Mbunge kwamba mwalo umezama kwa sababu maji yamekuwa mengi sana na tayari tumeshatuma wataalam wetu. Kwa hiyo, wataalam wetu watakapotupa taarifa juu ya nini tufanye, Serikali iko tayari kujenga soko jipya katika eneo hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaingia Wizara ya Fedha, Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 360

**Vyama vya Msingi vya Ushirika Kutumia Mashine za *EFD***

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, kwa nini TRA inalazimisha Vyama vya Msingi vya Ushirika kutumia *EFD machine* wakati hawafanyi biashara na mauzo yao ni mara moja kwa mwaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi *(Tax Administration Act)* ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba, "mtu yoyote anayesambaza bidhaa ama kutoa huduma ama kupokea malipo kuhusu bidhaa ama huduma anazosambaza anatakiwa kwa mujibu wa sheria kutoa risiti za mashine za kieletroniki kulingana na kiasi cha fedha alichopokea kutokana na bidhaa ama huduma aliyotoa."

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taratibu za kikodi zimebainisha kwamba, mfanyabiashara yeyote mwenye mauzo ghafi yenye kiasi cha shilingi milioni 11 na kuendelea kwa mwaka anapaswa kutumia mashine za kielekroniki *(EFD)*. Takwa hili la kisheria linahusisha walipakodi wote wanaofanya biashara mara nyingi au mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa la Serikali kuanzisha matumizi ya mashine ya kielektoniki *(EFD)* ni kuhamasisha na kujenga utamaduni wa kutunza kumbukumbu za biashara. Mashine ya *EFD* ni kati ya vifaa ambavyo humsaidia mfanyabiashara kutunza kumbukumbu za biashara kwa muda mrefu, na kwa upande mwingine huisaidia Serikali kutambua mauzo na kutoza kodi stahiki pale inapopaswa kufanya hivyo. *EFD,* inahakikisha dhana ya uwazi inasimamiwa kikamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nieleze masikitiko yangu. Inaonesha kabisa kwamba Serikali na *TRA* hawajui kabisa kazi za vyama vya msingi vya ushirika. Hivi vyama vya msingi vya ushirika havifanyi biashara, ni wakulima wadogo walioungana ambao wanapeleka mazao yao mnadani na wanafanya *transaction* yao mara moja kwa mwaka na kuwalazimisha kwamba watumie hizi *machine* za *EFD* ni kuwaongezea gharama zisizo na msingi.

Je, Serikali haioni sasa ina haja ya kuwasaidia hawa wakulima kuondokana na hii kadhia ya kutumia *machine* ya *EFD* kwa sababu haina tija? Mwisho hata sisi ambao ni wakulima; mimi mwenyewe ninalima, mtaniambia nitumie *machine* za *EFD*. Mwisho kila mtu hata akilima bustani mtamtaka atumie mashine za *EFD*. Lazima kuwe na *category* ya hizi. Hamwoni sasa imefika wakati kuwepo na sababu ya kuondoa hizi mashine?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme Serikali inatambua kazi za vyama vya msingi. Naliomba Bunge lako Tukufu tutengeneze utaratibu wa kujadili sheria tunapotunga sheria, tusijadili sheria tunapotekeleza sheria. Hili jambo ni la kisheria na mwezi ujao tutajadiliana masuala yanayohusu hatua za kikodi, kama kuna sheria tunaiona haifai, Bunge lako Tukufu lifute sheria hizo, lakini sheria zozote zinazotungwa tusijadiliane kuhusu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria yoyote ya nchi ikishatungwa inatakiwa itekelezwe, na sheria ambayo haifai tuiondoe lakini sheria ambayo ipo kwa ajili ya kusimamiwa inatakiwa isimamiwe na kila Mtanzania atekeleze.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lazima tuwafikishe Watanzania kwenye kutekeleza sheria, tusiwafikishe kwenye utamaduni wa kujadiliana kuhusu kutekeleza sheria. Hivi tunavyosema vyama vya msingi vinavyokusanya vinavyofikia hatua ya kiwango cha zaidi ya shilingi milioni 11, kwa mujibu wa sheria iliyopo vinatakiwa vitumie risiti za kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwamba wanauza mara moja ama wanauza mara mbili, siyo ya msingi sana, kwa sababu kama mtu anauza mara moja kwa mwaka na anapata shilingi milioni 100, anastahili alipe kodi. Hatuwezi tukamtoza kodi mtu mwenye kima cha chini anayepokea shilingi milioni tatu kwa mwaka halafu tukamwacha anayepokea shilingi milioni 100 kwa mwaka. Hii hoja inajitokeza hata kwenye masuala ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo haki kwenda kuchukua kodi ya *Nurse,* kodi ya Mwalimu wa Shule ya Msingi ili ikajenge josho la mtu mwenye mifugo 1,000, 3,000, 4,000, 9,000 au 11,000 kwa msingi tu kwamba yeye ana kundi la mara moja ama kukusanya kwake kunaleta kero. Tusichukue kodi kwa yule ambaye hatukusanyi kwa kero tukamtie umaskini halafu tukamsaidie yule aliyetajiri kisa tu tunashindwa kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuwa tunajadili hatua za kikodi, tutumie muda mwingi, tuchambue zile zote ambazo hazifai tuzitoe lakini zile tutakazosema zinafaa tuiachie mamlaka ya mapato itekeleze sheria kama ilivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Zuena Bushiri.

Na. 361

**Kuhamasisha zao la Pamba Kilimanjaro**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Zao la Pamba Mkoani Kilimanjaro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bodi ya Pamba inaendelea na uhamasishaji wa kilimo cha zao la pamba katika Kanda ya Mashariki inayojumuisha Mkoa wa Kilimanjaro kwa kusambaza mbegu, viuatilifu, kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa pamba katika mkoa huo. Kupitia hamasa inayofanywa, uzalishaji wa pamba katika Mkoa wa Kilimanjaro umeongezeka kutoka kilo 15,497 za msimu wa 2021/2022 hadi kufikia kilo 52,017 katika msimu wa 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuongeza uzalishaji katika Mkoa wa Kilimanjaro hadi kufikia kilo 200,000

katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeweza kupata Kampuni ya UPAMI ambayo imeanza kununua pamba inayozalishwa na wakulima wa Mkoa huo na jitihada za kutafuta wanunuzi wengine zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imepanga kuongeza usambazaji wa mbegu za pamba kutoka tani 12 msimu wa 2023/2024 hadi tani 28 msimu wa 2024/2025. Viuatilifu vitaongezeka kutoka *acrepack* 4,280 msimu wa 2023/2024 hadi *acrepack* 8,000 na mabomba ya kunyunyizia kutoka mabomba 10 msimu wa 2023/2024 hadi kufikia mabomba 30 msimu wa 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Mkoa wa Kilimanjaro unayo maeneo ya Tambarare ambayo yanastawi sana zao la pamba, lakini zao hili linaonekana kwamba halijahamasishwa vya kutosha. Kwa kuwa Mkoa huu maeneo haya tangu zamani yamekuwa yakilimwa sana pamba.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isifanye zao hili kama zao la kimkakati katika Mkoa wa Kilimanjaro ili kukuza uchumi wa wananchi wa Kilimanjaro pamoja na Taifa kwa ujumla?

Swali langu la pili: Kwa kuwa Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 2024/2025 imejipanga kulima hekta 250 ambazo zitakuwa na tani mia tatu, je, ni kwa nini sasa Bodi ya Pamba isifanye mpango wa kuongeza makampuni ya kununua pamba hiyo ili kuleta ushindani wa kibiashara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuhamasisha zao la pamba katika Mkoa wa Kilimanjaro, na nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamba ni moja ya zao la kimkakati na sisi kama Wizara tutaongeza msukumo zaidi katika Mkoa wa Kilimanjaro hususan katika maeneo ya Same na

Mwanga ili tuongeze uzalishaji na wananchi wale waweze kupata kipato cha ziada kutokana na zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza kampuni za uzalishaji, hilo ni jukumu letu kama Wizara na tumeshaelekeza Bodi ya Pamba kuwa sehemu ya wanunuzi wa pamba zinazozalishwa katika Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, jambo hilo lipo na tunalifanyia kazi na ndio maana kampuni ya kwanza ya UPAMI ambayo inaendelea kufanya, basi tutaongeza bodi na bodi itaendelea kutafuta wanunuzi wengine, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Nape Nauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Ndugu Mohamed Khamis Abdullah, Katibu Mkuu; Ndugu Nicholaus Mkapa, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Dkt. Jones Kilimbe, Mwenyekiti wa Bodi, *TCRA*; Bwana Stephen Kagaigai, Mwenyekiti wa Bodi ya *TBC;* Bregadia Mabongo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *TPC;* Profesa John Nkoma, Mwenyekiti wa Bodi Mfuko wa Mawasiliano wa wote; Bi. Zuhura Muro, Mwenyekiti wa Bodi, *TTCL;* Profesa Leonard Msele, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya *TEHAMA ICTC;* Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; Bi. Hawa Mgonja Ngh'umbi, Mwenyekiti wa Bodi ya *TCRA CCC* na Dkt. Mutabaazi Lugaziya, Mjumbe wa Bodi – *TSN. (Makofi)*

Wengine ni Bwana Mobhare Matinyi, Mkurugenzi Idara ya Habari - Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali; Dkt. Jabir K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu – *TCRA;* Dkt. Ayub Rioba Chacha - Mkurugenzi Mkuu – *TBC,* Ndugu Maharage Chande - Posta Masta Mkuu – *TPC;* Ndugu John S. Mukondya, Kaimu Mtendaji Mkuu – *UCSAF;* Bi. Mary S. Msuya, Katibu Mtendaji - *TCRA CCC;* Mhandisi Peter R. Ulanga, Mkurugenzi Mkuu – *TTCL;* Bi. Aisha Dachi, Kaimu Mtendaji Mkuu – Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Dkt. Nkundwe Mwasaga, Mtendaji Mkuu – *ICTC;* Ndugu Emmanuel L. Mkilia, Mkurugenzi Mkuu – *PDPC;* Bwana Mohammed Salim Panjwani, Balozi - Ubalozi

wa Romania na Dkt. Mhandisi George Mulamula, Mtaalamu Mwelekezi, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na mume wa Mheshimiwa Balozi Liberatus Mulamula. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 36 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambao ni familia yake, Kamati ya Utekelezaji UWT Taifa na Kamati ya Siasa Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja, Mbunge, ambaye ni Mfamasia kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambaye ni mtoto wake kutoka Mbulu, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Furaha Matondo ambaye ni rafiki zake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Awack ambaye ni Imamu na Mjumbe wa Kamati ya Msikiti kutoka Karatu, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Bakari Bakari ambao ni wataalamu na mafundi *aluminium* kutoka *Private Life* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Msalala, Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Simon Songe, wapigakura wake kutoka Busega, Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Kamonga ambao ni wapigakura wake kutoka Ludewa, Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni rafiki zake kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Frida Ernest Mkedege. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mafuwe ambao ni rafiki zake kutoka Kahama, Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Ally Makoa, hao ni Maafisa wa *Dodoma FM* na *Dodoma TV* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 70 na walimu watano wa Shule ya Awali ya Msingi *Royal Feat* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 na walimu kumi kutoka Shule ya Sekondari Ammar ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine waliopo Bungeni asubuhi hii waliokaa Jukwaa la Spika, ni wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni viongozi wa Klabu ya Simba kutoka Makao Makuu Jijini Dar es Salaam; kwanza ni Mtendaji Mkuu wa Klabu, Ndugu Imani Kajula na mwingine ni Ndugu Raphael Chegeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, haya makofi yalikuwa kwa dhati au? *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Wana-Simba na *corporates* wote waliopo Dodoma, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Mjengoni anaomba kuwatangazia kushiriki uzinduzi rasmi wa *Simba Executive Network (SEN)* hapa Dodoma. *(Makofi)*

Tukio hili litafanyika leo siku ya Alhamisi katika Ukumbi wa *Midland View Hotel,* Kisasa na mgeni rasmi ni Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson. Muda wa kuanza ni saa 12.00 jioni na hakuna kiingilio. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Fungu 68 kwa mwaka 2023/2024 naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ngoja kwanza. Waheshimiwa Wabunge! Waheshimiwa Wabunge! Waheshimiwa Wabunge! Mbaki hivyo hivyo. Mheshimiwa Waziri endelea. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake madhubuti kwa kipindi cha miaka mitatu tangu aingie madarakani kwa kuendelea kutuongoza vyema huku tukishuhudia maendeleo na uwekezaji mkubwa katika sekta zote hususan Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais katika kufikishiwa huduma za Habari, Mawasiliano na TEHAMA kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kwa miongozo na uongozi wake katika kulisimamia Bunge na Serikali kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kwa unyenyekevu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mbunge) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Tunamtakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikupongeze wewe kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu mkishirikiana na Mheshimiwa Spika. Tunakushukuru sana kwa jinsi ambavyo umekuwa mshauri

na kwa hakika umekuwa mdau wa Wizara yetu na hasa kwenye maeneo ya Teknolojia ya Habari. Umetushauri vema na kutusimamia vema. Tunakupongeza na tunawapongeza wapigakura wako wako kwani wamepata mtu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, uzalendo, uungwana na umahiri wao katika kutusimamia kwa ujumla wake ili tufikie malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa mwaka 2024/2025 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri, kuelekeza na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kuwaahidi kuwa maadam ‘imani huzaa imani’, mimi na wenzangu Wizarani, tutakwenda kusimamia na kutekeleza maelekezo ya Kamati kikamilifu. Ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako. Waheshimiwa Wabunge, kwa unyenyekevu mkubwa nimesimama kuwashukuru sana. Mnatuonyesha upendo mkubwa na mnatupa ushirikiano mkubwa mimi, wenzangu na taasisi tunazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalendo, uungwana na uthabiti wenu katika kuisimamia hii Wizara ndiyo matokeo ya mafanikio.

Kwa unyenyekevu mkubwa nimesimama kuwashukuru Wabunge wenzangu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi (Mbunge) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ninayoiongoza. Karibu sana Wizarani. *We are happy to have you. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee na umuhimu mkubwa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kuliletea maendeleo kwenye Jimbo letu. Ahsanteni kwa imani mnayonipa na ninawahakikishia sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba kuishukuru familia yangu na wanangu kwa uvumilivu, upendo wao na kunitia moyo kila wakati ninapokuwa sipatikani nikitekeleza majukumu ya kazi ambazo nimepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika tutaendelea kumuenzi Mzee huyu kwa umahiri wake na kwa mageuzi ya kisiasa aliyoyafanya, pamoja na kufungua nchi kiuchumi kwa kuruhusu uwekezaji wa Sekta Binafsi. Sisi kwenye Wizara yetu tumefaidika sana na uwekezaji wa Sekta Binafsi. Tunamkumbuka na kumuenzi Mzee Mwinyi kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hayati Lowassa ataendelea kukumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi wake mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali na yale aliyoyaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya CCM na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Kwahani kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2023/2024, yakiwemo mafuriko, maporomoko ya mawe na matope katika maeneo mbalimbali nchini. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, kuendeleza wataalamu wa TEHAMA, kuanzisha na kusimamia Postikodi, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Habari na Mawasiliano nchini ukiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijiti katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanayochochewa na kuwezeshwa na matumizi ya TEHAMA ambayo yatasaidia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kwa wakati ili wananchi waweze kushiriki katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia taasisi tisa ambazo

zimegawanyika kwenye umahususi wa huduma, mashirika ya kibiashara, udhibiti, mfuko, baraza na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, Shirika la Utangazaji Tanzania, Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Tume ya TEHAMA, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Baraza la Ushauri wa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano na sasa *e-Government* nayo imehamishiwa kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala yanayotekelezwa na Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Sekta ya Mawasiliano limeendelea kukua ambapo takwimu zinaonesha kuwa *line* za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 62.3 Aprili, 2023 hadi kufikia *line* milioni 72.5 Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 16.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa *internet* wameongezeka kutoka milioni 33.1 Aprili, 2023 hadi milioni 36.8 Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa hapa nchini wa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni 44.3 mwezi Aprili, 2023 hadi milioni 53.0 mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19.6. Aidha, watoahuduma ya miundombinu ya mawasiliano wamefikia 25 ikilinganishwa na watoahuduma 23 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha Tanzania inapata mapinduzi ya kidijiti na kuelekea kwenye uchumi wa kidijiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanza kutumika kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake pamoja na uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa mapinduzi ya kidijiti yanachochewa na matumizi ya *data* ambayo imekuwa ni bidhaa adimu. Pia Serikali imepitisha Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijiti 2024 - 2034 utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijiti kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huo una nguzo muhimu sita zikiwemo uwezeshaji wa miundombinu ya kidijiti, utawala wa kidijiti na uwepo wa mazingira wezeshi, kujenga uelewa na ukuzaji wa ujuzi wa kidijiti, uwepo wa utamaduni wa ubunifu wa kidijiti na teknolojia wezeshi, tamaduni ya ujumuishaji wa makundi maalum katika matumizi ya kidijiti na kuwezesha huduma za kifedha kwa kidijiti kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Serikali imefanya uamuzi wa kuihamishia Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA)* kuwa moja ya Taasisi chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hatua hii ni muhimu na itawezesha kuchochea ukuaji wa matumizi ya TEHAMA pamoja na ujenzi wa mifumo mbalimbali ya utoaji huduma kwa mujibu wa malengo na mwelekeo wa kisera. Hata hivyo, kikubwa itasaidia sana kuharakisha utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha mifumo yote nchini inasomana. Pia, hapa kipekee tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Baraza la Mawaziri kwa uamuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika safari hii ya mapinduzi ya kidijiti, Wizara imeanza kufanya marejeo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya 2016 pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali 14 itakayotumika katika usimamizi wa Sekta ya TEHAMA ambayo itasaidia kuboresha utendaji kazi wa taasisi kwa kutumia mifumo ya kidijiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo hiyo ni pamoja na ile ya usimamizi wa misingi ya mageuzi ya kidijiti nchini, kujenga uelewa kwa wananchi wote kuhusu matumizi ya TEHAMA, uimarishaji wa makundi mbalimbali katika huduma za kidijiti, matumizi ya akili mnemba, mkakati wa usalama mtandaoni *(Cyber Security Strategy)* pamoja na mkakati wa kufanya tafiti na bunifu za TEHAMA hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Tanzania inapiga hatua zaidi katika uchumi wa kidijiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu inaendelea kuandaa mfumo jumuishi unaojumuisha mifumo mitatu ambayo ni;

(i) Mfumo wa Jamii Namba, ambao utatumika kufanya utambuzi wa kipekee kwa kila mwananchi kuanzia anapozaliwa ambapo atakuwa na akaunti ya kidijiti itakayomwezesha kupata huduma zote za kijamii. Tuondokane na utaratibu wa kuwa na vitambulisho vingi, tunataka uwe na kitambulisho kimoja na kinakupa *access* ya huduma zote.

(ii) Mfumo wa Jamii Malipo ambao utawezesha wananchi kutumia Jamii Namba kupokea fedha na kurahisisha kufanya malipo kidijiti. Mfumo huu pia utasaidia *(Financial Inclusion)* na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

(iii) Mfumo wa Jamii Data Shirikishi ambao unamwezesha mwananchi kumiliki taarifa zake katika kupokea huduma mbalimbali nchini. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Tume ya TEHAMA nchini, imeanza ujenzi wa mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa uitwao *Jamii Data Exchange platform.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Habari nchini ambapo vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 65 mpaka 68 sawa na ongezeko la asilimia 4.6. *Cable Television* zimeongezeka kutoka 57 mpaka 60 sawa na asilimia 5.3. Vituo vya kurusha matangazo ya redio navyo vimeongezeka kutoka vituo 215 mpaka 231.

Vilevile kuna ongezeko la magazeti. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umeendelea kuhakikisha kuwa vyombo vya habari nchini vinakuwa huru kupokea na kutoa taarifa za matukio mbalimbali yanayojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu kutoka *World Press Freedom Index 2024* inayoratibiwa na Taasisi ya *Reporters Without Boarders* zimeonyesha kuwa Tanzania inaongoza Afrika Mashariki kwa kuheshimu uhuru wa vyombo habari, ambapo Kimataifa imeshika nafasi ya 97 mwaka huu kutoka nafasi ya 143 mwaka

2023 na kupelekea kupanda katika kuheshimu uhuru wa vyombo vya Habari. Tumepanda kwa nafasi zaidi ya 46.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la kujivunia na ni jambo la mafanikio sana. Mafanikio haya yametokana na Serikali kuchukua hatua muhimu ikiwemo Bunge lako Tukufu kufanya mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari hapa mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (shilingi/dakika) zimeendelea kushuka kutoka shilingi 29 Juni mwaka 2023 hadi kufika wastani wa shilingi 26 Aprili, mwaka 2024; wakati bei ya dakika nje ya mtandao bila kifurushi imeshuka kutoka wastani wa shilingi 31 Juni mwaka 2023 hadi kufikia wastani wa shilingi 28 Machi mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa gharama za rejareja za *data* bila kifurushi na kwenye kifurushi zimeendelea kupungua. Aidha, katika robo ya mwaka inayoishia Machi, 2024, gharama za *data* ndani ya kifurushi zimeshuka kwa kufikia wastani wa shilingi 2.17 kwa *MB* Aprili, 2024 ikilinganishwa na shilingi 2.25 Juni, mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 212.4. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 30.5 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 18.5 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 11.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 181.9 ziliidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 146.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 35.2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 213.9 sawa na asilimia 107 ya shilingi bilioni 212.4 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha tunaoumaliza. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 16 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 7.0 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 190.6 ni fedha kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023/2024, sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo: -

(i) Kufanya tathmini ya hali ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA, Sera ya Mawasiliano na kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA 2024;

(ii) Kuandaa rasimu ya sera ya kampuni changa za TEHAMA *(startups)*;

(iii) Kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo Rais aliizindua;

(iv) Kuhamisha shughuli zote za ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Taifa cha *Data* kwenda Shirika la Mawasiliano *(TTCL);*

(v) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 3008 na vituo 66 vya Mkongo wa Taifa;

(vi) Kukamilisha upanuzi wa Mkongo wa Taifa kutoka ukubwa wa *200 gigabyte per second* kwenda *800 gigabyte per second* kwenye mizunguko mikuu ya Mkongo wa Taifa na kuanza upanuzi wa Mkongo kutoka *800 gigabyte per second to 2000* au *two terabytes*;

(vii) Kuanza ujenzi wa minara 754 na inaendelea vizuri;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta Africa *(PAPU),* na Mheshimiwa Rais aliuzindua tarehe 02/09/2023, na nadhani ni kati ya majengo bora kabisa katika Mji wetu wa Arusha;

(ix) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF),* na Mheshimiwa Makamu wa Rais alizindua hapa Dodoma eneo la Njedengwa;

(x) Kukamlisha ujenzi wa miradi ya upanuzi wa usikivu wa redio katika maeneo saba ya Serengeti mkoani Mara, Bariadi, Simiyu, Ileje – Songwe, Njombe, Kilwa, Unguja na Pemba;

(xi) Kumalilisha kuridhiwa na kuanza kutumiwa kwa mkakati wa uchumi wa kidigitali;

(xii) Kukamilisha majadiliano kati ya Serikali na umoja wa wa watoa huduma ambapo Serikali ililipwa zaidi ya Dola milioni 33;

(xiii) Kusainiwa kwa mikataba ya mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini Uganda wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 28, Malawi wenye thamani ya Dola za Marekani milioni tano, Burundi wenye thamani ya Dola za kimarekeni milioni tatu na kampuni ya *Airtel* yenye thamani ya Dola za kimarekani milioni nne;

(xiv) Kuunda Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa *Satellite* nchini kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za anga ya juu nchini. Naomba nirudie hapa, tumefanikiwa kuunda Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa *Satellite* nchini kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za anga za juu nchini katika mkakati wa kuwa na *satellite* yetu kama nchi;

(xv) Kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya *TBC* eneo la Vikonje;

(xvi) Kuanza ujenzi wa kiwanda na kufunga mitambo ya kuchapa kwa kisasa wa magazeti ya Serikali;

(xvii) Kuongeza ushiriki wa Tanzania kwenye masuala ya kikanda; na tumeshinda tuzo mbalimbali kwa Shirika letu la Posta kupata *orbit*. Hili nalo ni muhimu; kupata *orbit* mpya ya *satellite* ya $16^0W$ kwa matumizi ya *satellite* za utangazaji na masafa mapya yatakayotumika katika kuboresha usalama wa mawasiliano ya angani na majini, na kupunguza gharama za uwekezaji wa miundombinu ya mawasiliano nchini;

(xviii) Kuwezesha ujenzi wa Kituo cha Mkongo Baharini wa *to Africa* ambao una kasi kubwa ya *17 terabyte per second to 180 terabyte per second;*

(xix) Kuunganishwa ofisi zaidi ya 50 za *RUWASA* kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(xx) Kuunganisha watumiaji 12,584 wa huduma za *fibber* mlangoni;

(xxi) kufanya upembuzi yakinifu wa kituo cha kuhifadhi data Zanzibar;

(xxii) Kuendelea kuhakiki anuani za makazi nchini;

(xxiii) Kufanya maboresho ya mfumo wa anuani za makazi;

(xxiv) Kudhibiti mawasiliano ya simu laghai nchini;

(xxv) Kuanza utekelezaji wa mradi wa miundombinu wa saini za kielektroniki;

(xxvi) Kukamilisha ujenzi wa maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki *(type approval laboratory),* ambao unajumuisha maabara ya kupima mionzi inayotokana na simu za mkononi *(specific absorption rate lab)* na maabara ya kupima masafa ya kifaa *(radio frequency lab)*; na

(xxvii) Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa miji janja *(smart cities)* katika miji ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu mengine ya sekta ya habari mawasliano na TEHAMA yameainishwa kwenye ukurasa wa 19 hadi 42 wa hotuba, na mnaweza ku-*scan* ili kuipata hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake; ambapo katika mwaka 2024 sekta binafsi zimeendelea kushirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya ujenzi wa minara, utoaji wa huduma za *internet,* utoaji wa elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi milioni 700 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, usajili wa magazeti, ada ya mwaka ya magazeti, vitambulisho wa waandishi wa habari, machapisho ya picha mbalimbali, mabango na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2024 wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta, Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2023;

(ii) Kutunga sera mpya ya Taifa ya TEHAMA;

(iii) Kuratibu utungwaji wa sera ya kampuni changa za TEHAMA *(startups);*

(iv) Kuratibu utungwaji wa sheria za anuani za makazi;

(v) Kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama wa Mtandao ya Mwaka 2015 ili iendane na wakati wa sasa, na pia iweze kujumisha masuala ya kumlinda mtoto dhidi ya ukatili wa mtandaoni na masuala ya ugaidi mtandaoni;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa minara ile 758 na kuanza ujenzi wa minara mipya 636 kwenye yale maeneo;

(vii) Kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo 70 ya kimkakati;

(viii) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwenye wilaya 40;

(ix) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi Jirani ya Congo;

(x) Kuanza ujenzi wa kituo cha kuhifadhi data Dodoma na Zanzibar;

(xi) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vyombo vya ulinzi na usalama, kwa maana ya Mahakama, TAKUKURU, Polisi, Magereza, Jeshi la Wananchi, Usalama na kadhalika; pamoja na taasisi za haki jinai zaidi ya 100;

(xii) Kuendelea kusimamia na kuimarisha mifumo ya kusimamia na kupima ubora wa huduma za mawasiliano;

(xiii) Kuwezesha mfumo wa anuani za makazi kuunganishwa na mifumo mingine;

(xiv) Ununuzi wa magari mawili maalum ya kurushia matangazo mbashara yaani *(OB van)* na magari 15 kwa ajili ya shughuli za utangazaji katika vituo vipya vya kurushia matangazo, ikiwemo kuwezesha kutangaza shughuli za Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

(xv) Kuendelea na taratibu za kuanzisha bodi ya ithibati ya wanahabari, baraza huru la habari na mfuko wa mafunzo kwa wanahabari;

(xvi) Kuratibu uanzishwaji wa wakala wa anga za juu nchini *(Tanzania Space Agencies)* na kuandaa kutekeleza mkakati wa anga za juu *(Auto Space Strategy);*

(xvii) Kutengeneza na kutumia mfumo wa kukusanya na kusambaza mizigo;

(xviii) Kusimamia uundaji wa mfumo wa kidijitali utakaowezesha biashara mtandao *(e-Commerce)*;

(xix) Kutekeleza mradi wa kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

(xx) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miundombinu ya kitaifa ya *sign* ya kielektroniki;

(xxi) Kuendelea na uratibu wa uendelezaji wa mifumo ya kitaifa nchini;

(xxii) Kujenga maabara ya akili mnemba na matumizi ya roboti nchini;

(xxiii) Kuendelea kuwezesha uanzishwaji wa ukuzaji wa vituo vya ubunifu (TEHAMA) katika wilaya sita na kwa kuanzia *district ICT startups innovation hubs*;

(xxiv) Kuanza ujenzi wa vyuo viwili vya TEHAMA Nala hapa Dodoma na Buhigwe mkoani Kigoma;

(xxv) Kusajiri wakusanyaji na wachakataji wa taarifa zaidi ya laki tano;

(xxvi) kuendelea kuimarisha usikivu wa redio *TBC* kwa kujenga mitambo ya redio yenye masafa ya *FM* kwenye wilaya saba za Buhigwe, Malinyi, Lushoto, Buchosa, Mafia, Ikungi na Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango mingine ya sekta ya mawasiliano imefafanuliwa katika ukurasa wa 43 mpaka 59 kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta binafsi katika utekelezaji wa bajeti ya 2024/2025. Katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwa mwaka 2024/2025 sekta binafsi imeridhia

kutekeleza majukumu yake kadhaa kwa kushirikiana na Serikali. Maeneo hayo ya ushirikiano ni pamoja na: -

(i) Kuendeleza ujenzi wa minara ya mawasiliano nchini;

(ii) Ujenzi wa *public Wi-Fi* kwenye maeneo kadhaa ya umma ambayo ni vyuo, masoko, hospitali, vituo vya mabasi, stesheni ya treni ya mwendokasi na kadhalika;

(iii) Kukuza bunifu za TEHAMA na kukuza kampuni changa; na

(iv) Utoaji wa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ya kunisaida. Tangu ameingia Wizarani ameleta chachu kubwa, tunamshukuru sana, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru ndugu Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Hana maneno mengi lakini ni mtu wa vitendo sana, ahsante sana ndugu Katibu Mkuu pamoja na Nicholaus Merinyo Mkapa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii; ahsante sana Chinga, ninakushukuru sana na karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nawashukuru wakurugenzi na wakuu wa vitengo katika Wizara, wenyeviti wa bodi za wakurugenzi na taasisi; na mmewaona hapa na wenyeviti wazito sana, ahsanteni sana kwa kazi nzuri mnazofanya. Viongozi wa taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii na kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia habari na TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niseme tumeweza kurudisha mtandao hapa nchini kwa usimamizi mzuri wa *TCRA,* na nimemuona Mkurugenzi wa *TCRA* hapa, ni mdogomdogo, mfupi

lakini mambo yake makubwa sana; tumpongeze huyu mkurugenzi kwa kazi nzuri sana ambayo amefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kipekee kuwashukuru washirika wa maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na sekta za habari na mawasiliano. Washirika hao ni; Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano *(ITU);* Shirika la Umoja wa Posta Duniani; Shirika la Umoja wa Posta Afrika; Benki ya Dunia kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa, Ubalozi wa Korea Kusini nchini na Shirika la Maendeleo la Ufaransa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda na kimataifa yanayohusu sekta hii. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati wa Juu ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee nizitambue kampuni za mawasiliano ya simu za *Vodacom* Tanzania, *Airtel* Tanzania, Honora Tanzania, *Halotel*, *TISPA* na *TTCL* kwa kusambaza huduma za mawasiliano nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kuzitambua taasisi za kifedha ikiwa ni pamoja na Benki ya *CRDB, NMB* na *TSA* kwa mchango wao katika kukuza bunifu za TEHAMA hapa nchini. Pia napenda kuvishukuru vyombo vya habari vyote pamoja na jumuiya zao ikiwemo MOAT, TAMWA, *MCT, UTPC, MISA Tan, TADIO, TMF, TEF, JOWUTA, JUMIKITA* na Jamii *Forums* kwa kuendelea kuhabarisha umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia natambua mchango wa wadau wote wa sekta ikiwemo Kampuni ya Minara Tanzania, *Herios Tower*, *Huawei, Softnet, Telecom Associate,*

*TanzTech* pamoja na *Raddy Fibre* na wengine wengi ambao sikuwataja, wote tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 180,926,557,000 kwa mchanganuo ufuatao: -

Kiasi cha shilingi 38,906,663,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi 28,997,474,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 13,909,189,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na Kiasi cha shilingi 142,019,894,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi 116,469,898,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 25,550,000,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara na pia unaweza ku-*scan* kuipata hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SURA YA 02**

**2.1 UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) kwa Mwaka 2023/24, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka 2024/25.

2.1.1 **Shukrani na Pongezi**

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa kumi na tano wa Bunge la kumi na mbili.

3. **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti kwa kipindi cha miaka mitatu tangu aingie madarakani na kuendelea kutuongoza vyema huku tukishuhudia maendeleo na uwekezaji mkubwa kwa Sekta zote hususan Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara inatambua matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais katika kufikishiwa huduma za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

5. **Mheshimiwa Spika,** vilevile nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa miongozo na uongozi wake makini katika kulisimamia Bunge na Serikali kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

7. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, nikupongeze wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara, hekima na tija kusudiwa kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa na

ya wananchi yanajadiliwa kwa umakini. Pia, niendelee kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Muungano wa Mabunge Duniani (IPU) na Baraza la Uongozi la IPU. Hakika unastahili pongezi za kipekee kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu historia ya kuanzishwa kwa chombo hicho. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.) Naibu Spika, kwa kuendelea kukusaidia kuliongoza Bunge lako. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

8. **Mheshimiwa Spika,** naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao kwangu na Wizara kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya sekta yanafikiwa. Pia ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa Mwaka 2024/25 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara.

Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii. Ninachoweza kuwaahidi kuwa maadam ‘imani huzaa imani’, mimi na wenzangu wizarani, tutakwenda kusimamia na kutekeleza maelekezo ya Kamati kikamilifu. Ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu pamoja na wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara.

Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara ninayoingoza itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya Maendeleo ya Taifa na ya wananchi katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

9. **Mheshimiwa Spika,** Nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ninayoiongoza.

10. **Mheshimiwa Spika,** kipekee na umuhimu mkubwa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu; bila kuisahau familia yangu kwa upendo, uvumilivu katika nyakati zote ambazo nimekua nikiendelea kutekeleza majukumu yangu.

### 2.1.2 Salamu za Pole

11. **Mheshimiwa Spika,** ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na kiongozi wetu Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa umahiri wake na kwa mageuzi ya kisiasa aliyoyafanya, pamoja na kufungua nchi kiuchumi kwa kuruhusu uwekezaji wa sekta binafsi.

12. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hayati Lowassa ataendelea kukumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi mkubwa katika kusimamia shughuli za Serikali.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya CCM na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa

Kwahani kwa tiketi ya CCM. Vilevile, naungana na Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2023/24, yakiwemo mafuriko na maporomoko ya mawe na matope katika maeneo ya Hanang Mkoani Manyara; Kibiti na Rufiji Mkoani Pwani pamoja na Malinyi, Ulanga, Ifakara, Mlimba Mkoani Morogoro na maeneo mengine nchini. Nipende kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na Watanzania wote walioondokewa na wapendwa wao. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

### 2.1.3 Wajibu wa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu; kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA; kuendeleza wataalam wa TEHAMA, kuanzisha na kusimamiana Postikodi, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Habari na Mawasiliano nchini ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijitali katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th, 5th na 6th Industrial Revolution) yanayochochewa na kuwezeshwa na matumizi ya TEHAMA ambayo yatasaidia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kwa wakati ili wananchi waweze kushiriki katika kuleta maendeleo.

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia Taasisi tisa ambazo zimegawanyika kwenye umahsusi wa Huduma, mashirika ya kibiashara, udhibiti, mfuko, baraza na taasisi wezeshi.

Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Shirika la Mawasiliano Tanzania; Shirika la Posta Tanzania; Shirika la Utangazaji Tanzania; Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Tume ya TEHAMA; Tume ya Ulinzi wa

Taarifa Binafsi na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano. Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala yanayotekelezwa na Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

16. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu kuu la usimamizi wa huduma za Mawasiliano kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura 172 (Tanzania Communications Regulatory Act CAP. 172) ambapo pamoja na mambo mengine, Mamlaka imekabidhiwa majukumu ya: -

i. Kutoa leseni za watoa huduma za mawasiliano nchini;

ii. Kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayakufuatwa;

iii. Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa kama gharama za maunganisho kati ya mtandao mmoja na mwingine;

iv. Kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano;

v. Kusimamia rasilimali adimu za mawasiliano ikiwemo masafa, namba na majina ya vikoa;

vi. Kufuatilia utendaji wa sekta zinazosimamiwa;

vii. Kukuza ushindani katika sekta;

viii. Kusambaza taarifa zinazohusu kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na

ix. Kushauriana na mamlaka nyingine za usimamizi katika kutekeleza majukumu sawa na yale ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

17. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheria Sura Na. 303 na lilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari, 1994

baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Shirika lina majukumu yafuatayo:

i. Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya huduma za Posta katika sekta za viwanda, biashara na jamii kwa ujumla kwa ufanisi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii. Kutoa huduma za kutuma na kulipa fedha kwa njia ya hawala za Posta (Money Order na Postal Order), au kwa kutumia njia nyingine zinazoonekana zinafaa; na

iv. Kutoa huduma za Kaunta kwa ajili ya Shirika na Huduma za Serikali bila kuathiri majukumu mengine yaliyotajwa katika Sheria ya uanzishwaji wa Shirika.

18. **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilianzishwa kupitia Sheria Na. 12 ya Bunge ya mwaka 2017 (Tanzania Telecommunications Corporation Act, No. 12 of 2017). Kwa mujibu wa sheria hiyo, Shirika la Mawasiliano Tanzania lina majukumu ya msingi yafuatayo:

i. Kuimarisha ulinzi na usalama wa huduma za mawasiliano ya simu nchini na utoaji wa huduma ya mawasiliano ya simu kibiashara na kiuchumi;

ii. Kutoa huduma za mawasiliano ya simu kwa mujibu wa Sheria;

iii. Kujenga na kuendesha miundombinu ya mawasiliano ya kimkakati kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana;

iv. Kutoa huduma ya miamala ya kifedha inayohusiana na mawasiliano ya simu;

v. Kuendesha mifumo na huduma ya mawasiliano ya simu ikiwemo mfumo wa TEHAMA ndani na nje ya nchi;

vi. Kutoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti na picha;

vii. Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu TEHAMA kwenye mashirika, Taasisi za umma na kwa wajasiriamali; na

viii. Kukuza uwekezaji wa huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya nchi.

19. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni taasisi ya huduma kwa umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257. Majukumu makuu ya TBC ni kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha umma kwa kuzingatia kaulimbiu ya 'Ukweli na Uhakika'. TBC kama Chombo cha Utangazaji cha Umma (Public Service Boradcaster - PSB) kina sifa na majukumu yafuatayo:

i. Kuwafikia wananchi wote nchini bila kujali umbali, idadi ya wakazi au gharama;

ii. Kuandaa maudhui yanayohusu na kugusa maisha ya makundi yote ya jamii na kwa kuzingatia utamaduni;

iii. Kuendesha huduma ya utangazaji kwa fedha zinazotokana na bajeti au vyanzo vingine;

iv. Kulinda, kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Taifa;

v. Kulinda, kutetea na kusimamia rasilimali za Taifa kama vile maliasili, madini, gesi, mafuta, mazingira na urithi wa kihistoria;

vi. Kukuza na kudumisha uzalendo, kutetea na kusimamia maslahi ya Taifa; na

vii. Kulinda, kutetea na kujenga taswira chanya ya Taifa.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa Tamko la Rais la mwaka 1970 na imetokana na utaifishaji wa iliyokuwa Tanganyika Standard Newspapers Limited. Kampuni hii inasimamiwa na kuendeshwa chini ya Sheria ya

Makampuni Sura ya 212. Kampuni ina majukumu makuu manne (4) kama ifuatavyo:

i. Kuwa chombo cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi na wananchi na Serikali yao;

ii. Kuunga mkono sera na mipango ya Serikali na kuhabarisha na kuelimisha umma juu ya sera na mipango hiyo;

iii. Kutafuta na kuandika habari sahihi zenye michango mbalimbali Kijamii, Kisayansi, Kisiasa, Kiuchumi na Kiutamaduni; na

iv. Kuwa kiini cha kutoa habari kwa lengo la kukuza uchumi na kueneza amani na mshikamano kwa Watanzania.

21. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa kwa Sheria Namba 11 ya Mwaka 2006 kwa lengo la kupeleka na kufikisha huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo ya mijini na vijijini yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano. Majukumu ya Mfuko yaliyoainishwa kwa mujibu wa sheria ni pamoja na:

i. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

ii. Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iii. Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iv. Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;

v. Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na

vi. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

22. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya TEHAMA ilianzishwa kwa Amri ya Rais kupitia Tangazo Namba 532 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Kwa mujibu wa Amri iliyoanzisha Tume ya TEHAMA, majukumu ya Tume ni pamoja na:

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya TEHAMA nchini;

ii. Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;

iii. Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani ya TEHAMA;

iv. Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;

v. Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na

vi. Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoainishwa na Sheria.

21. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), imeanzishwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Namba 11 ya Mwaka 2022. Kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wake Tume ina majukumu yafuatayo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa wakusanyaji na wachakataji;

ii. Kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa sheria;

iii. Kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

iv. Kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

v. Kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

vi. Kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;

vii. Kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii; na

viii. Kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

22. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeanzishwa kwa Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura 172. Kifungu cha 38 cha Sheria hiyo kimelipa Baraza majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya TEHAMA nchini;

ii. Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;

iii. Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani ya TEHAMA;

iv. Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;

v. Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na

vi. Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoainishwa na Sheria.

## 2.2 HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NCHINI

### 2.2.1 Hali ya Ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano

25. **Mheshimiwa Spika**, kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2022, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa **asilimia 7.4** mwaka 2022 ikilinganishwa na **asilimia 9.1** mwaka 2021. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zitolewazo na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara Mwaka 2023 **asilimia 69** ya ardhi ya Tanzania (Geographical Coverage) inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani. Sekta hii huchangia katika uchumi moja kwa moja na kupitia sekta zingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia Teknolojia ya Habari.

### 2.2.2 Hali ya Upatikanaji wa Mawasiliano Nchini

26. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **milioni 62.3** Aprili, 2023 hadi laini milioni **72.5** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 16.4**. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka milioni **33.1** Aprili, 2023 hadi milioni **36.8** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 11.2.** Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni **44.3** Aprili, 2023 hadi Milioni **53.0** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 19.6**. Aidha, Idadi ya Watoa Huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano imefikia **25** ikilinganishwa na watoa huduma 23 Aprili, 2023 (hii ni sawa na ongezeko la asilimia **8.7**). Watoa huduma za ziada (Application Services and Value-Added Services) wamefikia **135** ikilinganishwa na watoa huduma **141** Aprili, 2023 (punguzo la **asilimia 4.4**).

### 2.2.3 Hatua iliyofikiwa ya Mapinduzi ya Uchumi wa Kidijitali

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina wajibu wa kusimamia Mapinduzi ya Kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali yanaweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika Uchumi wa kidijitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na muingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidijitali. Ili kuharakisha Tanzania kuelekea katika uchumi wa kidijitali, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanza kutumika kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake pamoja na uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hatua hii ni muhimu hasa ukizingatia kuwa mapinduzi ya kidijitali yanachochewa na matumizi ya taarifa (Data) ambayo imekua ni bidhaa adimu. Pia Serikali imepitisha Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali 2024-2034 utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi.

Mkakati huo una nguzo muhimu sita (6) zikiwemo uwezeshaji wa miundombinu ya Kidijitali, utawala wa Kidijitali na uwepo wa Mazingira wezeshi, kujenga uelewa na ukuzaji wa ujuzi wa kidijitali, uwepo wa utamaduni wa ubunifu wa kidijitali na teknolojia wezeshi, tamaduni ya ujumuishaji wa makundi maalum katika matumizi ya kidijitali na kuwezesha huduma za kifedha kwa kidijitali pamoja na maamuzi ya Serikali ya kuihamishia Mamlaka ya Serikali Mtandao kuwa moja ya Taasisi chini ya Wizara. Hatua hii itawezesha kuchochea ukuaji wa matumizi ya TEHAMA pamoja na ujenzi wa mifumo mbalimbali ya utoaji huduma kwa mujibu wa malengo na mwelekeo wa kisera. Katika hatua hii tunamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza la Mawaziri.

28. **Mheshimiwa Spika**, Katika safari hii ya mapinduzi ya kidijitali Wizara imeandaa miongozo 14 itakayotumika katika usimamizi wa Sekta ya TEHAMA kama ifuatavyo: "Tanzania Enterprise Architecture Framework " ambao unasaidia kuboresha utendaji kazi wa taasisi kwa kutumia mifumo ya kidijitali; "Tanzania Interoperability and Standardisation Framework" ambao utaifanya Tanzania kuwa na viwango vitakavyotambulika kimataifa katika TEHAMA; "Tanzania Digital Public Infrastructure

BluePrint" ambao unasimamia msingi wa mageuzi ya kidijitali nchini; Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya TEHAMA Tanzania ambao utasaidia kujenga uelewa kwa Wananchi wote wa Tanzania katika matumizi ya TEHAMA.

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ujumuishaji wa Makundi Anuai katika Huduma za Kidijitali ili kuhakikisha kuwa hakuna mwananchi anaeachwa nyuma katika matumizi ya TEHAMA. Aidha, miongozo mingine saba (7) ipo kwa wadau ili waweze kuitolea maoni, ikiwemo Mwongozo na Mkakati wa Matumizi ya Akili Mnemba Tanzania; Mkakati wa Kufanya Tafiti na Bunifu za TEHAMA nchini; Mwongozo wa Kitaifa wa Ubadilishanaji Taarifa; Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Jamii Namba; Mkakati wa TEHAMA wa Ufuatiliaji na Tathmini na Mkakati wa Usalama Mtandao - Cyber Security Strategy.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Tanzania inapiga hatua zaidi katika uchumi wa Kidijitali, Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu inaendelea kuandaa Mfumo jumuishi (Samia's Technology Stack) unaojumuisha mifumo mitatu (3) ambayo ni:

***Mfumo wa Jamii Namba,***
ambao utatumika kufanya utambuzi wa kipekee wa kila mwananchi kuanzia anapozaliwa ambapo atakuwa na akaunti ya kidijitali itakayomwezesha kupata huduma zote za kijamii;

***Mfumo wa Jamii Malipo,***
ambao utawezesha wananchi kutumia Jamii Namba kupokea fedha na kurahisisha kufanya malipo kidijitali. Mfumo huu pia utasaidia ujumuishi katika huduma za kifedha (Financial Inclusion) na kuongeza Wigo wa mapato ya Serikali; na

***Mfumo wa Jamii Data Shirikishi,***
ambao unamwezesha mwananchi kumiliki taarifa zake katika kupokea huduma mbalimbali nchini.
Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Tume ya TEHAMA Nchini imeanza ujenzi wa Mfumo wa Ubadilishanaji taarifa uitwao Jamii "Data Exchange Platform/ Tanzania Enterprise Service Bus"

31. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza kutekeleza Mkakati huo kwa kuendelea kujenga miundombinu ya TEHAMA ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Vituo vya Kutunza Data, Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano na kuiongezea uwezo minara (upgrade) inayotumia teknolojia ya 2G pekee ili iweze kutoa pia huduma ya intaneti na Ujenzi wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Aidha, Serikali inaendelea na mradi wa kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi yanayotumiwa na wananchi katika shughuli zao za kila siku ili kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mtandao wa intaneti nchini. Vilevile Serikali inaendelea kuunganisha mifumo ya utoaji huduma ili iweze kubadilishana taarifa na pia kuwezesha huduma nyingi za Serikali kupatikana kwenye dirisha moja kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Fauka ya hayo, Serikali imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao.

32. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia inaendelea na taratibu za kuanzisha Taasisi ya Anga za Juu, Taasisi ambayo inakusudiwa kuongoza juhudi katika uratibu wa masuala ya anga ikiwemo urushaji wa Setelaiti yetu angani na ujenzi wa uchumi wa anga (space economy) kwa ujumla. Hatua hii itarahisisha matumizi ya teknolojia ya anga inayochochea mapinduzi ya kiuchumi na kijamii.

### 2.2.4 Hali ya Sekta ya Habari Nchini

33. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya habari nchini ambapo vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo **65** mwaka 2023 hadi vituo **68** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 4.6** na Cable Television zimeongezeka kutoka **57** Aprili, 2023 hadi **60** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 5.3.** Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo **215** mwaka 2023 hadi vituo **231**Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 7.4** na magazeti yameongezeka kutoka 321 Aprili, 2023 hadi **351** Aprili, 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 9.3**. Aidha, Serikali imeendelea kuweka

mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana.

**2.2.5 Uhuru wa vyombo vya habari**

34. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuhakikisha kuwa vyombo vya habari nchini vinakuwa huru kupokea na kutoa habari za matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii.

Takwimu kutoka World Press Freedom Index 2024 inayoratibiwa na Taasisi ya Reporters Without Boarders zimeonyesha kuwa Tanzania inaongoza Afrika Mashariki kwa kuheshimu uhuru wa habari, ambapo Kimataifa imeshika nafasi ya **97** mwaka 2024 toka nafasi ya **143** mwaka 2023 na kupelekea kupanda katika kuheshimu uhuru wa vyombo vya Habari. Mafanikio haya yametokana na Serikali kuchukua hatua muhimu ikiwemo Bunge lako Tukufu kufanya mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura 229. Aidha, katika kipimo kingine cha mwezi Aprili 2024 cha uhuru wa kutoa maoni kwenye vyombo vya habari cha Afrobarometer, Tanzania imeshika nafasi ya kwanza kwa nchi 39 za Afrika zilizofanyiwa utafiti huo

**2.2.6 Gharama za Mawasiliano ya Simu**

35. **Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (Shilingi/dakika) zimeendelea kushuka kutoka Shilingi **29.0** mwezi Juni, 2023 hadi kufika wastani wa Shilingi **26.00** Aprili, 2024, wakati bei ya dakika nje ya mtandao bila kifurushi imeshuka kutoka wastani wa Shilingi **31.0** kwa Juni, 2023 hadi kufikia wastani wa Shilingi **28.00** kwa Machi, 2024. Mwenendo wa gharama za rejareja za data bila kifurushi na kwenye kifurushi zimeendelea kupungua. Aidha katika robo ya mwaka inayoishia Machi 2024, gharama za data ndani ya kifurushi zimeshuka kwa kiasi kidogo na kufikia wastani wa Shilingi **2.17** kwa Megabyte Aprili, 2024 ikilinganishwa na Shilingi **2.25** kwa Megabyte Juni, 2023. Usajili wa vikoa umeongezeka kufikia **30,090** Aprili, 2024 ukilinganisha na **vikoa 28,076**

vilivyosajiliwa kipindi kilichoishia Juni, 2023. Hili ni ongezeko la vikoa **2,014** sawa na asilimia **7.2**

## 2.3 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WAMPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WAFEDHA 2023/24

### 2.3.1 Hali ya Ukusanyaji wa Mapato

36. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 150.7** ambapo Shilingi bilioni **150.2** ni fedha kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; Shilingi **milioni 24** kutokana na kuuza Vitambulisho vya Waandishi wa Habari; **Shilingi milioni 300** kutokana na mauzo ya picha za viongozi; **Shilingi milioni 30** kwa ajili ya usajili wa magazeti; Shilingi milioni **100** Ada ya mwaka ya magazeti; Shilingi 1,000 marejesho ya fedha za Umma; Shilingi **1,000** Ukumbi wa Mikutano; na **Shilingi 1,000** mapato kutoka vyanzo vinginevyo.

37. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imekusanya **Shilingi bilioni 24.8** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambayo ni sawa na **asilimia 16.5** ya makadirio ya makusanyo, makusanyo haya yataongezeka baada ya kukamilika kwa mradi unaoendelea wa upanuzi wa Mkongo. Aidha, Idara ya Habari-MAELEZO imekusanya **Shilingi milioni 62.1** kutokana na mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi na picha ya Baba wa Taifa, vitambulisho, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti sawa na **asilimia 14.4** ya lengo.

### 2.3.2 Bajeti iliyoidhinishwa

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 212.4**. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 30.5** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 18.5** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 11.9** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 181.9** iliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo **Shilingi bilioni 146.8** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 35.2** ni fedha za nje.

### 2.3.3 Fedha zilizopokelewa na Wizara

39. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 213.9** sawa na **asilimia 100.7** ya **Shilingi bilioni 212.4** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka 2023/24. Kati ya zilizopokelewa **Shilingi bilioni bilioni 16.3** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 7.0** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 190.6 ni** fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo inajumuisha **Shilingi bilioni 102.1** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 88.5** ni fedha za nje.

## SURA YA 03

### 3.1 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

### 3.1.1 Eneo la Habari - MAELEZO

40. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kufanya mapitio na kuandaaa rasimu ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 toleo la mwaka 2024 ambayo ipo katika hatua za uidhinishwaji;

ii. Kuendelea na taratibu za utungaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);

iii. Kukusanya taarifa za utekelezaji wa Miradi katika Halmashauri **109** kati ya Halmashauri 184 zilizopo nchini kwa lengo la kuhabarisha Umma;

iv. Kuendelea na taratibu za kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari;

v. Kutoa leseni **30** za magazeti na kuchapisha vitambulisho **1,000** vya Waandishi wa Habari;

vi. Kuendelea kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, miradi na programu zinazotekelezwa ambapo mikutano nane (8) ya mawaziri wa sekta za muungano na waandishi wa habari ilifanyika wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya muungano; mikutano 72 ya wakuu wa taasisi za umma iliratibiwa ili kuhabarisha umma; vipindi **24** vya programu ya "Kazi Iendelee" vilirushwa kupitia kituo cha Televisheni cha TBC 1 pamoja na mitandao ya kijamii ikiwemo ile ya Idara ya Habari (Maelezo); na mikutano **45** ya Msemaji Mkuu wa Serikali ya kuelezea masuala ya utekelezaji wa Serikali na kutoa ufafanuzi ilifanyika;

vii. Kuandaa mkutano wa **18** wa mwaka wa Maafisa Mawasiliano wa Serikali ambapo jumla ya washiriki 500 kutoka katika Wizara, Mikoa, Taasisi za Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatarajiwa kuhudhuria mwezi Juni 2024;

viii. Kuhamasisha vyombo vya habari vya nje kutangaza fursa zilizopo nchini. Vyombo hivyo ni pamoja na BBC, Reuters, Deutche Welle, China Global Television Network (CGTN), Redio ya China na Redio ya Umoja wa Mataifa (UN Radio);

ix. Wizara imekamilisha kuandaa rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano, ambao upo katika hatua za uidhinishwaji;

x. Kuanzisha na kuendesha mijadala katika Jukwaa la Clubhouse, ambapo mijadala nane (8) iliyowahusisha Mawaziri ilijadiliwa; na

xi. Kutengeneza studio maalumu kwa ajili ya kuandaa na kurusha vipindi vya moja kwa moja. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya utangazaji kwa ajili ya uendeshaji wa studio hiyo.

### 3.1.2 Eneo la Mawasiliano

41. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2023/24 Sekta ya Habari na Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuanza Ujenzi wa minara **758** katika Kata **731** na kuongeza uwezo wa minara **304** kutoka teknolojia ya 2G kwenda 2G/3G na 4G. Hadi Aprili, 2024 Minara **142** imekamilika kujengwa ambapo minara **124** tayari inatoa huduma. Aidha, minara **243** imeongezewa nguvu;

ii. Kufanikisha Tanzania kupata obiti mpya ya setelaiti ya **160°W** kwa matumizi ya Setelaiti za Utangazaji na masafa mapya yatakayotumika katika kuboresha usalama wa mawasiliano ya angani na majini. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha Mashirikiano ya Kimataifa kwenye masuala ya Anwani za Makazi. Jitihada hizi zimeiwezesha Tanzania na Korea Kusini kuingia Makubaliano ya ushirikiano katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi;

iii. Kuunda Kamati ya Kitaifa ya usimamizi wa Setelaiti nchini kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za anga za juu nchini;

iv. Kuanza taratibu za utungaji wa Sheria ya Anwani za Makazi, ambapo hatua iliyofikiwa ni kukusanya maoni ya wadau kuhusu Sheria husika;

v. Kuandaa mpango wa Miaka Mitano (5) wa Masuala ya Anga za Juu. Aidha, Kamati ya Utendaji na Ufundi zimeundwa kuratibu na kusimamia programu ya anga la juu nchini na kufanikiwa kuandaa andiko dhana la mapendekezo ya kuweka uratibu na usimamizi mzuri wa sekta ya anga la juu nchini;

vi. Kuandaa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano ambao umeainisha maeneo **22** ya uwekezaji katika Mawasiliano;

vii. Utoaji wa Huduma Pamoja unaolenga kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu 49 katika dirisha moja;

viii. Kushiriki kikamilifu katika vikao vya Taasisi za Kimataifa zinazosimamia Sekta ya Mawasiliano ambapo Tanzania ni mjumbe wa Baraza la Uongozi la Shirika la Mawasiliano

Duniani (ITU), mjumbe wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Duniani (UPU) na mjumbe wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika (PAPU). Kutokana na Ushiriki huo Tanzania imepata fursa ya kuchaguliwa kwenye Bodi ya Utendaji ya Wadau ya Ubunifu wa Kidijitali ya ITU (An Executive Multi-stakeholder Digital Innovation Board); Tanzania pia imechaguliwa kuwa sehemu ya mpango wa uanzishwaji wa Vituo vya kuchochea ukuaji wa Teknolojia (ITU Network of Acceleration Centres) na ijumuishwe kwenye uanzishaji na matumizi ya Maabara za Kijiditali zinazoratibiwa na ITU "Digital Transformation Labs".

### 3.1.3 Eneo la Uendelezaji wa Mifumo na Huduma za TEHAMA

42. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 yafuatayo yametekelezwa:

i. Kufanya tathmini ya hali ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997. Baada ya tathmini hiyo ilibainika kwamba sehemu kubwa ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu imepitwa na wakati na baadhi ya maeneo kwenye Sera ya Taifa ya TEHAMA yanahitaji kuboreshwa. Aidha, Wizara imeitisha vikao vya wadau wa Kampuni changa za TEHAMA na kupokea maoni yaliyowezesha kupata mikakati ya kisera katika eneo la bunifu za TEHAMA, ujasiriamali na Kampuni Changa (startups); Mapendekezo yaliyokusanywa yamewezesha kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA ikijumuisha Sera zote mbili. Rasimu ya Sera hii ipo katika hatua ya uidhinishwaji ndani ya Serikali;

ii. Kuanza taratibu za utungwaji wa Sheria ya TEHAMA, 2024 na taratibu za uidhinishwaji wa Sheria hii zitaanza baada ya kuridhiwa kwa Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA;

iii. Kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuanzisha Chuo Mahiri cha TEHAMA Nala – Dodoma. Aidha, tathmini ya ujenzi wa chuo hiki inatarajiwa kukamilika Julai, 2024 na itajumuisha maeneo Makuu matatu ambayo ni TEHAMA, majengo na programu za elimu. Vilevile, kupitia Mradi wa

Tanzania ya Kidijitali (DTP) maandalizi ya utoaji wa programu za muda (modular program) kwenye Vyuo Vikuu (UDOM, MUST, UDSM) yanaendelea. Pia, kwa upande wa Chuo cha TEHAMA Kigoma, Kiwanja cha ujenzi wa Chuo hicho kimepatikana Wilaya ya Buhigwe na makisio ya gharama pamoja na michoro ya awali ya ujenzi wa Chuo imeandaliwa na kuwasilishwa TANESCO;

iv. Kukamilisha kuandaa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034. Mkakati huu umeanza kutekelezwa kwa lengo la kuharakisha na kuimarisha mapinduzi ya kidijitali; na

v. Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na ushirikiano na sekta binafsi kwenye masuala ya TEHAMA, ambapo Septemba, 2023 Serikali imesaini Hati ya Makubaliano - MoU na Serikali ya India. Utekelezaji wa MoU umeanza ambapo timu ya wataalamu ilienda kujifunza ujenzi wa mfumo wa utambuzi kidijitali (Digital Identity), mfumo wa malipo na vituo vya ubunifu (innovation hubs). Timu ya wataalamu (Joint Working Committee) imeundwa kati ya Tanzania na India kusimamia utekelezaji wa masuala haya. Aidha, Serikali kupitia Wizara imesaini Mkataba wa ushirikiano na NMB wenye lengo la kukuza bunifu za TEHAMA nchini.

### 3.1.4 Eneo la Miundombinu ya Mawasiliano

43. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 yafuatayo yametekelezwa:

i. Kukamilisha ujenzi wa Kilometa **3,008** na Vituo **66** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

ii. Kukamilisha upanuzi wa Mkongo wa Taifa kutoka ukubwa wa 200Gbps kwenda 800Gbps kwenye mizunguko mikuu ya Mkongo wa Taifa na kuanza upanuzi wa Mkongo kutoka 800Gbps hadi 2000Gbps;

iii. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa brodibandi wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy) ambapo hadi Aprili, 2024 Utekelezaji wa Mkakati huu umefikia **asilimia 70**;

iv. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi data Zanzibar;

v. Kukamilisha majadiliano kati ya Serikali na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano (consortium) kulikopekelea Serikali kulipwa Dola za Marekani **milioni 33**;

vi. Kuwezesha kupungua kwa gharama za uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano kwenye hifadhi za barabara ambapo ada ya awali imepungua kutoka Dola za Marekani **1000** hadi **200** kwa Kilometa na Ada ya mwaka imepungua kutoka Dola za Marekani **1000** hadi **100** kwa Kilometa; na

vii. Kuwezesha ujenzi na uzinduzi wa Kituo cha Mkongo wa Baharini wa 2Africa wenye uwezo wa kusukuma kiwango kikubwa cha intaneti kuanzia 17Tbps hadi 180Tbps.

### 3.1.5 Eneo la Usalama Mtandao

44. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo ilizinduliwa Aprili, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Kufanya mapitio ya Sera tatu (3), Sheria sita (6), Kanuni tatu (3) na Mikataba ya kitaifa na kimataifa na miongozo inayohusiana na masuala ya ulinzi wa mtoto na kupendekeza maboresho; na

iii. Kuendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa binafsi wa mwaka 2014 ambao utaimarisha mazingira ya kushirikiana katika ulinzi wa taarifa binafsi hususan kwa

taarifa zinazovuka mipaka ya nchi kwenda katika nchi zilizopo barani Afrika.

### 3.1.6 Mambo Mengine yaliyotekelezwa na Wizara

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

i. Kuendelea na zoezi la kuhuisha Sera zinazosimamiwa na Wizara ikiwemo Sera ya Posta ya mwaka 2003 na kuendelea kusimamia maandalizi ya utungaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC;

ii. Kutungwa kwa Kanuni za Usajili wa Laini za simu, kanuni za Electronic and Postal Communication (Radio and Televisions Broadcasting Content (Amendment) Regulation, 2022 na kurekebisha Kanuni nyingine sita (6) za usimamizi wa Sekta ya Habari na mawasiliano. Wizara inaendelea kuboresha Kanuni za Usajili wa laini za Simu, Tozo za Muda wa Maongezi wa simu, Kanuni za Masafa na Kanuni za Kushirikiana katika Miundombinu ya Mawasiliano;

iii. Kuandaa Mpango kazi wa elimu kwa umma kuhusu usalama mtandao, ambapo vipindi maalumu **12** vya televisheni na redio vya kuelimisha umma kuhusu usalama mtandao vimeandaliwa;

iv. Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi wa Wizara na rejesta ya vihatarishi vimeandaliwa na usimamizi wake unaendelea;

v. Mpango wa ukaguzi wa ndani uliandaliwa na unaendelea kutekelezwa ambapo maeneo yenye changamoto yameendelea kuainishwa na kufanyiwa maboresho stahiki;

vi. Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na mifumo ya kimenejimenti kwa kufanya ukaguzi wa ndani kila robo mwaka na taarifa kuwasilishwa mamlaka husika;

vii. Kukamilisha kujaza Bodi za Wakurugenzi za Taasisi mbili (2);

viii. Wizara iliwapatia mafunzo ya kujengewa uwezo Watumishi wote kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi. Aidha, viongozi wa Wizara na Taasisi walipatiwa mafunzo maalum (retreat) ya kujengewa uwezo Jijini Arusha;

ix. Kufanikiwa kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya mtandao kwa vijana na watumishi wa umma katika maeneo ya Arusha, Dar es Salaam na Zanzibar na pia kupitia vipindi maalumu vya Televisheni na redio; na

x. Kusimamia Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Wizara katika mji wa Serikali – Mtumba ambapo ujenzi umefikia asilimia **82.5**.

### 3.1.7 Mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa lengo la kuharakisha utoaji wa huduma za habari na mawasiliano nchini. Katika mwaka 2023/24 Sekta binafsi imeendelea kushirikiana na Wizara katika maeneo yafuatayo: Kampuni tano za Mawasiliano ya Simu zimechangia **asilimia 60** ya gharama za ujenzi wa Minara **758** katika Kata **713** nchini; Utoaji wa huduma ya intaneti kwenye maeneo ya wazi; Utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi na salama ya mawasiliano; Kuendelea kuanzisha televisheni na redio kwa lengo la kuwezesha kuhabarisha umma na kuharakisha bunifu za kidijitali. Aidha, Wizara iliwezesha kusainiwa kwa hati ya Makubaliano kati ya Kampuni ya Airtel Tanzania na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuunganisha Shule **3,000** na mtandao wa intaneti kwa kipindi cha miaka mitano.

## 3.2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

47. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **181.95** kwa ajili ya kutekeleza Miradi tisa (9) ya Maendeleo. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya **shilingi bilioni 190.6** Sawa na **asilimia 104.8**. Hali ya utekelezaji wa kila mradi ni kama ifuatavyo;

### 3.2.1. Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi.

48. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 mradi umetengewa **shilingi bilioni 24** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfumo wa Anwani za Makazi. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi bilioni 7.8** sawa na **asilimia 32.5** ya bajeti iliyotengwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuhakiki na kuboresha taarifa katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Manispaa za Morogoro, Iringa, Singida, Kigoma Ujiji na Halmashauri ya Mji wa Masasi. Kupitia zoezi hili Anwani za Makazi 2,308,231 (Tanzania Bara 1,937,111 na Zanzibar 371,120) zimehakikiwa kati ya 12,385,956 zilizokusanywa wakati wa operesheni. Vilevile, Anwani mpya 505,436 zimesajiliwa na kufanya idadi ya Anwani za Makazi zilisosajiliwa kuongezeka hadi 12,891,392sawa na ongezeko la asilimia 4.1.

ii. Kujenga uwezo kwa wataalam wa MDAs, Tawala za Mikoa na watendaji katika Serikali za Mitaa ambapo hadi Aprili, 2024 Wataalamu 6,613 wamejengewa uwezo (Tanzania Bara 5,897 na Zanzibar 716) kati ya 38,078 (Tanzania Bara 37,196 na Zanzibar 882) wanaotarajiwa sawa na Asilimia 17.4.

iii. Kufanya maboresho ya mfumo wa Anwani za Makazi katika maeneo yafutayo:

   a. Kuwezesha Mfumo wa NaPA kutoa barua za utambulisho wa mkazi kidijitali ambapo kwa sasa huduma hii ipo kwenye majaribio kwenye mitaa/vijiji na shehia 13 na Wizara imepeleka vitendeakazi katika maeneo hayo yote ambavyo ni kompyuta, printa na vishikwambi;

   b. Kuwezesha Mfumo kusajili Anwani za Makazi katika maeneo ya hifadhi na vivutio vya utalii ili kuchochea ukuaji na kuongeza wigo wa kutangaza vivutio vyetu nchini;

   c. Kuwezesha wananchi wasio na Anwani za Makazi kutuma maombi ya kupatiwa Anwani bila kulazimika kwenda kwenye ofisi za watendaji; na

d. Kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za Mfumo wa Anwani za Makazi kupitia menyu ya huduma za Serikali ambayo ni *152*00#;

iv. Kuunganisha Mfumo wa NaPA na mifumo kumi **(10)** ya Taasisi za Serikali ya kutolea huduma. Mifumo mingine **28** ipo kwenye hatua ya ukamilishwaji.

iv. Kutunga sheria ya Anwani za Makazi ambayo hadi kufikia Aprili, 2024 ukusanyaji wa maoni ya wadau umekamilika.

### 3.2.2. Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

49. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 80** ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi bilioni 77.08** sawa na **asilimia 96.4** ya bajeti iliyotengwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukamilisha ujenzi wa kilometa **3,008** na vituo **66** vya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hivyo, kufanya upanuzi wa njia za usafirishaji wa mawasiliano kutoka **800Gbps** kwenda **2000Gbps**;

ii. Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo cha kutunza Taarifa (Data Centre) Zanzibar. Mkataba umesainiwa na upembuzi yakinifu umeanza. Kwa sasa Mkandarasi amewasilisha kazi za usanifu wa kituo kwa kupitiwa na Wataalamu wa Wizara. Aidha, kwa upande wa ujenzi wa kituo cha kutunza Taarifa (Data Centre) Dodoma, taratibu za kumpata mzabuni wa kufanya upembuzi yakinifu zimekamilika ili kuanza kazi ya ujenzi;

iii. Kuunganisha ofisi 50 za RUWASA kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

iv. Kuimarisha njia za ndani za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya kuunganisha nchi ya Jamhuri ya Kimedokrasia ya Kongo; na

v. Kukamilisha upanuzi wa Mkongo wa Taifa kutoka ukubwa wa 200Gbps kwenda 800Gbps kwenye mizunguko mikuu ya Mkongo wa Taifa na kuanza upanuzi wa Mkongo kutoka 800Gbps hadi 2000Gbps

### 3.2.3. Mradi wa Tanzania ya Kidijitali

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2023/24 Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 35.18** fedha za nje. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi bilioni 88.58** sawa na **asilimia 251.8** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi tajwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuwezesha ujenzi wa Minara Mipya **758** nchini ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 minara **142** imejengwa ambapo minara 124 imewashwa na inatoa huduma;

ii. Kufanya tathmini ya awali ya Kimazingira na Kijamii katika maeneo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano, pamoja na kuunda dawati la kushughulikia malalamiko katika maeneo hayo;

iii. Kuwezesha kuongeza nguvu minara **243** kati ya minara **304** iliyopangwa kutoka 2G kwenda 3G/4G;

iv. Kuongeza bando la intaneti la Serikali la **Shilingi 1,031,095,800** kwa ajili ya maunganisho ya utoaji huduma za Serikali kwa wananchi;

v. Kutoa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi **20** wa Serikali katika nchi za Ujerumani, Uingereza, Malaysia na Marekani. Aidha, Serikali imetangaza nafasi **480** za mafunzo ya muda mfupi kupitia mradi wa Tanzania ya kidijitali;

vi. Kuwezesha kufanya mafunzo ya usimamizi wa utendaji kazi kwa watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma (PEPMIS); na

vii. Utengenezaji wa mfumo wa usajili wa taarifa binafsi na kushughilikia malalamiko ya taarifa kwa ajili ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

### 3.2.4. Mradi wa Habari kwa Umma.

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 1.5**. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi 711,550,000** sawa na **asilimia 47.4** ya bajeti iliyotengwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu na kuwezesha mikutano **30** kati ya Wakuu wa Taasisi za Serikali na waandishi wa habari na pia kati ya Wakuu wa Mikoa **14** wakiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri zao na waandishi wa habari kwa lengo la kuelezea shughuli za utekelezaji wa serikali kwa wananchi ambapo mikutano hii yote hurushwa mubashara na televisheni za kawaida na zile za mitandaoni;

ii. Kukusanya taarifa za miradi **397** ya maendeleo katika mikoa **16** kati ya **26** ya Tanzania Bara kupitia kampeni ya "Tumewasikia, tumewafikia". Aidha, mikutano kupitia programu hiyo ilifanyika katika mikoa **14** na halmashauri zake; na

iii. Kuandaa video fupi **79**, vibango **95** na habari **73** katika Sekta ya Elimu (msingi na sekondari), Afya, Kilimo, Viwanda, Uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuvisambaza katika mitandao ya jamii.

### 3.2.5. Mradi wa Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 4.5**. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi bilioni 2.5** sawa na **asilimia 55.6** ya bajeti iliyotengwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Ununuzi wa Magari Manne (4) ya Viongozi wa Wizara;

ii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa miradi miwili (2) ya maendeleo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na mradi wa kufunga Mtambo wa Kisasa wa Uchapaji;

iii. Kutoa mafunzo ya uandaaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati na Bajeti kwa watumishi **53** katika ngazi ya Menejimenti na maafisa bajeti wa Wizara; na

iv. Kufanya mafunzo kwa wataalamu **31** wa Wizara kuhusu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

### 3.2.6. Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park)

53. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 mradi huu ulitengewa **Shilingi bilioni 8.4** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea **Shilingi bilioni 2.6** sawa na **asilimia 31.0** ya bajeti iliyotengwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Miji Janja (Smart City) katika majiji ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

ii. Kusimamia upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Umahiri cha TEHAMA Jijini Dodoma;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu usalama wa mtandao katika Mikoa nane (8) ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. Mikoa iliyopatiwa elimu kwa umma ni Mjini Magharibi, Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Tabora na Mwanza. Elimu hii ilitolewa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano;

iv. Kuandaa rasimu ya miongozo mitano (5) ya usimamizi wa miundombinu muhimu ya TEHAMA (CII) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

v. Kuandaa mpango Mkakati wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; na

vi. Ununuzi wa gari la Ofisi kwa ajili ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

## 3.3. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

54. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2023/24 Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 619.96** Hadi Aprili, 2024 Taasisi zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 521.79** sawa na **asilimia 84.17** ya lengo.

55. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo: -

### 3.3.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

56. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2023/24, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilipanga kukusanya **Shilingi 221,167,037,333.62** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (**asilimia 1** ya pato ghafi la watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano pamoja na ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA.

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, TCRA imekusanya **Shilingi bilioni 267.5** sawa na **asilimia 120.95** ya makadirio ya makusanyo ya mapato. Ongezeko la makusanyo haya limesababishwa na kuboreshwa kwa mifumo ya ndani ya utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato ikiwemo “TANZANITE PORTAL” na kuboreshwa kwa zoezi la Kuwajua wateja “Know Your Customer (KYC)” na makusanyo ya mwisho ya masafa sawa na **shilingi bilioni 118.7.**

Shughuli zilizotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni:

**i. Usimamizi wa huduma za mawasiliano nchini**

57. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kuboresha na kusimamia uendeshaji wa Mfumo wa Communication Monitoring System (CMS) ambao unasimamia na

kudhibiti huduma za mawasiliano ya simu nchini. Mfumo huu umeiwezesha TCRA kubaini simu za ulaghai na zile za mitandao ya kijamii (OTT by- pass fraud) kwa kutumia njia za kisasa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, TCRA imeendelea kubaini mawasiliano ya simu za ulaghai zinazoingia hapa nchini na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa ambapo katika kipindi hicho, jumla ya simu za ulaghai **767** zilibainika na kuchukuliwa hatua stahiki.

**ii. Uhalifu mtandaoni**

58. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kudhibiti uhalifu mtandaoni kwa kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na uhalifu wa kimtandao ikiwemo kusimamisha usajili kwa mawakala wanaotembea kwa mikoa iliyoripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya wizi wa kimtandao ambayo yamejikita katika mikoa ya Rukwa, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora, Songwe na Mwanza. Aidha, TCRA inaendelea kushirikiana kwa karibu na Jeshi la Polisi na wadau wengine ili kuhakikisha inakabiliana na tatizo la uhalifu wa kimtandao. Zoezi hili ni endelevu na linalenga kuziba mianya ya upotevu wa mapato pamoja na kuwalinda watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini.

59. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kuboresha Kanzidata ya namba tambulishi kwa kuongezewa uwezo wa utunzaji data (data storage capacity). Katika kusimamia kanzidata huwezesha kubaini na kufungia namba tambulishi za vifaa vya Mawasiliano zilizonakiliwa (Duplicate), zilizotumika kwenye udanganyifu pamoja na zile zilizotolewa taarifa ya kupotea au kuibiwa. Jumla ya namba tambulishi zilizofungiwa ni 95,194 ambazo ziliripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu, hivyo kuwezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko.

60. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha usajili wa namba za simu kwa kuongeza uwezo wa kuhakiki usajili wa laini za simu pamoja na kuhakiki usahihi wa taarifa kutoka Kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Aidha, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua ambapo hadi Aprili, 2024

kulikuwa na laini za simu milioni 72.5. Idadi hii ya laini za simu inahusisha laini zinatotumiwa na watu na laini zinatumiwa kwa ajili ya mawasiliano kati ya mashine kwa mashine (M2M).

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia Mfumo wa kuhakiki simu za ndani na za kimataifa. Mfumo huu umeboreshwa na kuiwezesha Mamlaka kupata takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma kwa ngazi ya mkoa na wilaya. Mfumo huu unawezesha kupata takwimu za mawasiliano ya simu za ndani yaliyofanyika baina ya wateja wa mitandao tofauti pamoja na simu za kimataifa zinazoingia na kutoka nchini. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 jumla ya simu za kimataifa zilizoingia nchini zilikua ni **73,662,098.** Takwimu zinaonyesha kuongezeka kutoka dakika **3,574,914** kwa mwezi Julai, 2023 hadi dakika **10,962,421** kwa Aprili, 2024 ambayo ni sawa na ongezeko la dakika **7,387,507.**

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha Mfumo wa usimamizi wa miamala ya Fedha kwa kuongeza uwezo wa uchakataji wa taarifa na utunzaji. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024, idadi ya miamala imeongezeka kutoka **milioni 492.29** Julai, 2023 hadi **milioni 610.22** Aprili 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 24.0**

63. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa Mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano ambapo hadi Aprili, 2024 jumla ya leseni **1,054** zimetolewa ikilinganishwa na leseni **448** zilizotolewa mwaka 2022/23.

**iii. Kuimarisha upimaji na kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kutoa huduma za udhibiti kwa usahihi zaidi.**

64. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kupima ubora wa mawasiliano ya simu na intaneti kwa mitandao ya Vodacom, Airtel, Halotel, TTCL na Tigo - Zantel Tanzania Zanzibar na Tanzania bara katika Mikoa ya Dar Es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Iringa, Lindi, Mara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Singida, Tanga, Simiyu, na Zanzibar (Unguja na Pemba). TCRA ilifanya ukaguzi kwa watoa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti **137** pamoja na miundombinu

yao ili kubaini ukiukwaji katika utoaji wa huduma ambapo baadhi ya watoa huduma walikutwa na dosari mbalimbali na hivyo kuelekezwa kurekebisha dosari hizo.

65. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na ufuatiliaji wa maudhui katika vituo vya Redio 147 na Televisheni **75** katika mikoa mbalimbali. Ufuatiliaji wa maudhui mtandaoni umefanyika kwa vituo **41.** Mikutano ya mashauriano imefanyika kwa jumla ya vituo **16** na kati ya hivyo vituo viwili **(2)** vilibainika kukiuka kanuni na masharti ya leseni na vilipelekwa kwenye Kamati ya Maudhui, na vituo vingine kupewa barua ya maelekezo.

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuzingatia masharti ya leseni husika na kanuni za kutoa huduma za posta ili kubaini upungufu uliopo na kuchukua hatua stahiki. Kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili 2024 Ofisi za Posta **93** na watoa huduma wa usafirishaji wa vifurushi katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Ruvuma, Tabora, Dodoma, Kagera, Katavi, Mwanza, Singida, Songwe na Rukwa, pia kwa upande wa Zanzibar, eneo la Unguja ukaguzi ulifanyika na hatua stahiki za kiudhibiti zilichukuliwa kwa watoa huduma waliobainika kuwa na dosari za kiutendaji, jumla ya wasafirishaji vipeto **22** waliobainika kutokuwa na leseni za TCRA walipewa elimu jinsi ya kuomba leseni ili waache kufanya biashara bila ya leseni.

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na jukumu la kupanga masafa katika bendi ya 3600-3800 MHz kutumika kwa teknolojia ya intaneti ya kasi (5G) ikiwa ni sehemu ya maazimio ya Mkutano Mkuu wa Mawasiliano Duniani (World Radiocommunication Conference, 2023 – WRC23) chini ya uratibu wa ITU. Aidha, imeendelea na zoezi la kuhuisha taarifa ya upangaji wa masafa ya bendi zinazotumika mahususi kwa huduma za simu na intaneti, utangazaji, usafiri salama wa anga, usafiri salama wa majini na usafiri wa reli.

68. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kusajili vikoa vya intaneti vya dot tz ambapo hadi Aprili 2024 ilisajili vikoa **9,094** na kuhuisha vikoa **13,939** na kufanya jumla ya vikoa vilivyokwisha sajiliwa kufikia **30,090.**

70. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2023/24 TCRA imefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo;

i. Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la PAPU na kuzinduliwa rasmi Septemba 2023 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Kuanza utekelezaji wa mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (NPKI). Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mfumo, kukamilika kwa mafunzo ya kitalaam yanayohusu Saini za kielekitroniki, uagizaji na upokeaji wa vifaa vya mradi na programu za NPKI na kufanyika kwa warsha kuhusu usanifu wa miundombinu ya saini za kielektroniki "NPKI design". Hadi Aprili 2024 utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 87. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuhakikisha usalama wa taarifa za kielektroniki nchini; na

iii. Kukamilisha ujenzi wa maabara ya uidhinishaji wa vifaa vya mawasiliano ya kieletroniki (type approval laboratory), ambao unajumuisha maabara ya kupima mionzi inayotokana na simu za mkononi (specific absorption rate lab) na maabara ya kupima masafa ya kifaa (radio frequency lab). Maabara hizi zinalenga kuwa na vifaa salama vya mawasiliano na kuhakikisha hakuna muingiliano wa mawasiliano na hivyo kuwa na huduma bora za mawasiliano. Ujenzi wa jengo la maabara pamoja na usimikaji wa vifaa vya maabara umekamilika. Kwa sasa majaribio ya upimaji yanaendelea.

### 3.3.2. Shirika la Posta Tanzania (TPC)

71. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Posta Tanzania kwa mwaka 2023/24 lilipanga kukusanya shilingi **39,476,613,000** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ambavyo ni huduma za EMS, barua na biashara ya usafirishaji, biashara ya huduma za kielektroniki, huduma za kifedha na uwakala, biashara ya kubadili fedha za kigeni na miliki za shirika. Hadi Aprili, 2024 Shirika limekusanya shilingi **18,392,628,111** sawa na asilimia 46.6 ya lengo.

Shughuli zilizotekelezwa na Shirika la Posta Tanzania ni kama ifuatavyo:

i. Kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

ii. Kuanzisha vituo viwili (2) vya kukusanya na kusambaza mizigo, vifurushi na vipeto ambavyo ni; Libya (Dar es Salaam) na Uyole (Mbeya);

iii. Kuanzisha na kuhudumia mikoa mipya sita (6) ya posta ya Katavi, Manyara, Songwe, Njombe, Bariadi (Simiyu) na Pwani. Aidha, Shirika limefanikiwa kufungua ofisi katika jengo la Umoja wa Posta Afrika (PAPU) lililojengwa Jijini Arusha;

iv. Kusaini mikataba ya mashirikiano na wasafirishaji binafsi wa mizigo, vipeto, vifurushi ikiwemo; kampuni ya TUTUME World Wide Co. Ltd, Azam Marine, Ethiopian Airlines na ATCL. Aidha, Shirika limeingia Mkataba na NMB kwa ajili ya kuwa mawakala wa nchi nzima pamoja na kuhuisha mikataba ya Agency Banking na benki ya TCB, PBZ na NBC;

v. Kusimika mashine ya kidijitali ya Huduma za kifedha (Virtual Teller Machine – VTM) ili kuwezesha mteja kujihudumia mwenyewe katika jengo la Ofisi ya Posta PAPU Arusha; na

vi. Kuendelea kusimamia utoaji wa huduma za Serikali kupitia vituo vya Huduma Pamoja katika ofisi tano (5) za Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Tanga.

### 3.3.3. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

72. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulipanga kukusanya shilingi **35,102,688,605** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni ruzuku kutoka Serikali kuu, tozo ya huduma, ruzuku kutoka TCRA na Wadau wa Maendeleo. Hadi Aprili, 2024, UCSAF imekusanya

**shilingi 40,764,123,712** sawa na asilimia 116.1 ya lengo. Hadi Aprili, 2024 Mfuko umetekeleza yafuatayo:

i. **Ujenzi wa Minara 758 katika Kata 731**

73. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF imeendelea na ujenzi wa minara **758** katika Kata **731** nchini. Hadi Aprili, 2024 jumla ya minara **142** imekamilika kujengwa ambapo minara **124** imewashwa na inatoa huduma. Minara **126** inaendelea na taratibu za kufungwa vifaa vya redio na kisha kuwashwa. Minara **616** ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na inatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2025 kulingana na Mkataba. Mradi huu, una thamani ya **shilingi bilioni 126** ambapo hadi sasa malipo ya awali yenye thamani ya **shilingi bilioni 64.54** yamelipwa kwa watoa huduma wote.

ii. **Kuiongezea nguvu minara 304 kutoka 2G kwenda 2G/3G na 4G.**

74. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF ilisaini Mkataba na watoa huduma wanne (4) Airtel, TTCL, Honora Tanzania, Vodacom kuiongezea nguvu minara 304 kutoka teknolojia ya 2G kwenda 2G/3G na 4G ambapo utekelezaji wa mradi huu unaendelea. Hadi Aprili, 2024 minara **243** sawa na asilimia 7 tayari imeshaongezwa nguvu na imeanza kutoa huduma.

iii. **Kuboresha huduma za matangazo ya TBC Redio katika maeneo ya mipakani na kuboresha redio jamii.**

75. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeainisha maeneo ya mipakani yatakayoboreshewa huduma za matangazo ya TBC ambayo ni pamoja na Rombo, Usangi (Kilimanjaro) na Bukombe (Geita). Maandalizi ya rasimu ya mkataba wa utekelezaji baina ya TBC na UCSAF yamekamilika na Mkataba umetiwa saini Februari, 2024. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha huduma za matangazo ya redio jamii katika Halmashauri za Mpimbwe, Bariadi, Biharamulo na Arusha umekamilika.

iv. **Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za Posta.**

76. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha manunuzi ya vifaa vya kudurufu alama za msimbo (barcode scanners) **250** kwa ajili ya mradi wa kuboresha utoaji wa huduma za Posta. Taratibu za ufungaji wa vifaa hivyo zinaendelea.

v. **Kuratibu maadhimisho ya siku ya wasichana na TEHAMA.**

77. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya siku ya msichana na TEHAMA ambapo mafunzo hayo yamefanyika kuanzia tarehe 20 – 24 Aprili, 2024 katika vituo vitano (5) vya kikanda (Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam) na Zanzibar katika shindano la Kitaifa kuanzia tarehe 26 - 29 Aprili, 2024. Maadhimisho yamelenga kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wasichana wa kidato cha tatu wapatao 248 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

vi. **Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa watoto wenye mahitaji maalum katika shule sita (6).**

78. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF imechambua na kubainisha shule sita (6) za sekondari za umma zitakazonufaika na mradi wa kupatiwa vifaa vya TEHAMA. Shule zilizochaguliwa ni Balangdalalu (Hanang), Shangani (Mtwara MC), Chanji (Sumbawanga MC), Muhutwe (Muleba), Jendele (Kati) na Pujini (Chake Chake). Kazi ya kukusanya mahitaji ya shule husika imekamilika hata hivyo vifaa hivi hutofautiana kulingana na mahitaji ya watoto waliopo mashuleni. Taratibu za manunuzi zinaendelea kufuatia zabuni kufunguliwa na kufanyiwa tathmini

vii. **Kuunganisha hospitali tano (5) na tiba mtandao.**

79. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF imekamilisha kuziunganisha Hospitali za Rufaa za Mnazi Mmoja iliyopo Unguja na Hospitali ya Rufaa ya Abdalla Mzee iliyopo Pemba katika Mtandao wa Tiba Mtandao unaojumuisha hospitali kuu za Taifa za Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) na Hospitali

ya Kansa ya Ocean Road (ORCI). Kwa sasa wataalamu wanaendelea na majaribio ikiwemo kutuma picha za majaribio.

viii. **Kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi.**

80. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF imekamilisha kufunga mtandao wa intaneti katika viwanja vya maonesho ya kimataifa (Sabasaba) Jijini Dar es Salaam, kwa ushirikiano baina ya TTCL na TANTRADE. UCSAF ilikamilisha kufunga vifaa vya kutolea huduma za bure za intaneti katika maeneo 17 katika viwanja vya sabasaba. Aidha, kwa sasa, UCSAF inaendelea na hatua za awali za maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vituo vya mabasi ya mwendokasi (DART) na mtandao wa intaneti ambapo tathmini ya awali imekwishafanyika kuainisha vituo na maeneo yatakayonufaika na awamu ya kwanza ya mradi. Kwa sasa tayari awamu ya kwanza imeainishwa kuwa ni njia ya Morogoro (Kimara - Kivukoni) na Awamu ya Pili ni Mbagala – Gerezani na mchakato wa zabuni unaendelea ambapo unatarajiwa kukamilika Juni, 2024.

### 3.3.4. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

81. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kukusanya Shilingi **240,000,000,000** kutokana na huduma za mawasiliano, ukodishaji wa vifaa vya mawasiliano, upangishaji majengo na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi Aprili, 2024, Shirika limekusanya **Shilingi 135,216,317,693** sawa na **asilimia 56.34** ya lengo.

82. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili 2024 Shirika limetekeleza yafuatayo:

i. Kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Wilaya 22 za Karatu, Mbulu, Longido, Hai, Mwanga, Pangani, Muheza, Lushoto, Kibiti, Mtama, Nachingwea, Newala, Mbinga, Ludewa, Ileje, Vwawa, Mbogwe, Msalala, Tarime, Sengerema, Rorya na Ngara;

ii. Kuunganisha watumiaji **12,584** wa huduma za faiba mlangoni sawa na asilimia **63** ya lengo;

iii. Kuwezesha upatikanaji wa huduma ya Wi-Fi katika maeneo manne (4) ya umma ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam;

iv. Kufanya tafiti mbili (2) za kuridhika kwa wateja;

v. Kusajili wateja **102,850** wapya wa T-PESA kwa ajili ya kutumia huduma za kifedha za T-PESA; na

vi. Kuunganisha Taasisi sita (6) za Serikali naBinafsi kwa ajili ya huduma za malipo ya mkupuo (bulk disbursement).

vii. Kusainiwa kwa Mikataba ya mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi za Uganda wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 28.8**, Malawi wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 5.5** na Kampuni ya Airtel wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 4.8**;

### 3.3.5. Tume ya TEHAMA (ICTC)

83. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 Tume ya TEHAMA ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 5,284,725,000** kutoka katika vyanzo vya ndani na mgao kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi Aprili, 2024 Tume imekusanya **Shilingi 4,612,570,343.12** sawa na **asilimia 87.3** ya lengo.

84. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Aprili, 2024, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuendelea na ukarabati wa kituo cha kukuza bunifu za TEHAMA cha Dar es Salaam ambapo ukarabati umefikia **asilimia 56**;

ii. Kupata eneo la uwekezaji wa kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA (ICT Refurbishment and Assembly centre) katika Wilaya ya Bagamoyo eneo la Kiromo. Tathmini ya eneo na muundo wa uwekezaji inaendelea ili kuwezesha uazishwaji wa vitega uchumi vya

TEHAMA katika eneo hilo ikiwemo maabara za kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA;

iii. Kuwatambua na kuwasajili wataalam wa TEHAMA **262** kwa lengo la kuwaendeleza. Hivyo kupelekea Idadi ya wataalam wa TEHAMA waliosajiliwa kufikia **1,504**. Aidha, miongozo ya usimamizi wa usajili wa wataalam wa TEHAMA, usimamizi wa taasisi zinazotoa mafunzo ya wataalam wa TEHAMA pamoja na usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA imeandaliwa;

iv. Kukamilisha tafiti kuhusu "Tanzania digital economy road map" na majaribio kwa ajili ya kupima maendeleo ya TEHAMA katika Wilaya ya Kinondoni na kuzinduliwa rasmi kwenye kongamano la TEHAMA Oktoba, 2023;

v. Kuendelea na utafiti kwa ajili ya kupima maendeleo ya intaneti nchini, mwingiliano wa mifumo ya Kitaifa (National inter-operability proof of concept); na hali ya ukuaji na maendeleo ya kampuni changa za kukuza bunifu nchini;

vi. Kuandaa Mkutano wa mwaka wa wataalam wa TEHAMA Oktoba, 2023 ambapo jumla ya washiriki **750** kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki. Aidha, Serikali kupitia ICTC imefanikisha kuandaa mikutano miwili maalumu kwa ajili ya vijana na Wanawake kwenye TEHAMA ambapo washiriki **520** walihudhuria;

vii. Kusaini Mkataba wa mashirikiano naTaasisi ya Belinda and Gates Foundation kwa ajili ya kukuza ubunifu na kuanzisha kampuni changa za huduma za kifedha kwa wanawake na vijana na kuendelea na mashirikiano na benki ya CRDB ya kutekeleza programu ya Imbeju yenye lengo kukuza kampuni changa za TEHAMA. Hadi Aprili, 2024 Kampuni changa **20** zimepita katika hatua mbalimbali za uchambuzi na ziko katika hatua za mwisho za uchambuzi wa kibiashara ili kupatiwa mitaji;

viii. Tume imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha TURKU cha Finland kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Resilience Academy hapa nchini kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya UDSM, SUZA,

MoCU, ARU na SUA. Uanzishwaji wa kituo hiki utasaidia kujenga uwezo na kuongeza ujuzi katika masuala ya TEHAMA hususan katika sekta ya elimu, utafiti, uendelezaji wa miji, mazingira na uhifadhi wa Data za TEHAMA; na

ix. Kuwajengea uwezo wataalam **176** wa TEHAMA katika maeneo ya usalama wa mifumo, uundaji wa mifumo pamoja na usimamizi wa mifumo (Software Safety, Network Development and Security Systems and Network Administration and Network Defender). Pia, vijana **303** wamepatiwa mafunzo maalum ya ubunifu katika ulimwengu wa intaneti na kujenga uwezo katika kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA.

### 3.3.6 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

85. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 Shirika la Utangazaji Tanzania lilikadiria kukusanya kiasi cha **Sh. 46,860,319,000** kutoka katika vyanzo vya mapato ya Shirika na mgao kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi Aprili, 2024 TBC imekusanya **shilingi 36,209,228,890** sawa na **asilimia 77.3** ya lengo na kufanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kukamilisha miradi ya upanuzi wa usikivu wa redio za TBC katika maeneo ya Serengeti – Mara, Bariadi – Simiyu, Ileje – Songwe, Njombe, Kilwa – Lindi, Unguja na Pemba. Aidha, katika kipindi hiki TBC ilizindua studio za kisasa za kidijiti za redio (TBCTaifa, BongoFM na TBCInternational) zilizopo barabara ya Nyerere. Vilevile, miradi mingine iliyokamilika ni ufungaji wa mitam bo na vifaa katika studio za televisheni jijini Dodoma pamoja na studio za redio ya vijana (BongoFM) ambayo ni mahsusi kwa habari za vijana na wapenda burudani inayotan gaza katika mfumo wa kidijitali;

ii. Kuboresha matangazo ya Tanzania Safari Chaneli kwa kukarabati jengo la ofisi, kununua vifaa vya kurusha matangazo mbashara ya Televisheni (Live U - 3) na kutafsiri vipindi 325 vya chaneli ya Tanzania Safari kwenye lugha tano (Kingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu na Kichina);

iii. Kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa mitambo ya mifumo ya TEHAMA ya kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);

iv. Kununua vifaa kwa ajili ya kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook);

v. Kununua magari sita **(6)** kwa lengo la kuboresha utendaji wa TBC. Aidha, taratibu za ununuzi wa magari tisa **(9)** na ununuzi wa gari moja la OB van zinaendelea; na

vi. Kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya TBC katika eneo la Vikonje Jijini Dodoma ambapo hadi Aprili, 2024 ujenzi umefikia **asilimia 18.**

**3.3.7. Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**

86. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24, Kampuni ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 30,860,282,250** kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya ndani pamoja na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi Aprili, 2024 Kampuni iliweza kukusanya kiasi cha **Shilingi 18,303,871,910** sawa na **asilimia 59.3** ya malengo yaliyopangwa.

87. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili, 2024 Kampuni imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuendelea na ujenzi wa kiwanda kwa ajili ya kufunga mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji ambapo ujenzi umefikia **asilimia 35.** Aidha, Kampuni imepokea jumla ya mitambo mipya ya kisasa mikubwa minne (4) pamoja na mitambo midogo saba (7) ambayo ni sehemu ya mitambo mikubwa. Kwa ujumla mitambo hiyo iliyopokelewa ina thamani ya **shilingi 15,749,232,000.43;**

ii. Kuongeza wauzaji na mawakala wapya wa magazeti **(8)** katika mikoa ya Dar es Salaam **(3)**, Tanga **(2),** Kilimanjaro **(1)** na Morogoro **(2);**

iii. Kuongeza wateja binafsi 80 na Kampuni tano **(5)** walionunua magazeti mtandaoni hivyo kufanya jumla ya wateja binafsi kufikia **1,354** na kampuni **34** mtawalia;

iv. Kukamilisha uundaji wa Programu Tumizi ya simu ambayo inatarajiwa kuongeza idadi ya watumiaji wanaojisajili kusoma habari na maga zeti ya TSN mtandaoni. Kampuni inafanya mapitio ya mwisho ya programu hiyo kabla ya kuanza kutumika rasmi kabla ya Julai, 2024;

v. Kutoa ushauri na huduma za kihabari kwa taasisi mbalimbali. Aidha, Kampuni imefanya mazungumzo yenye lengo la kukuza ushirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi zikiwemo wizara, taasisi na mashirika ya umma, vyombo vya habari, balozi na taasisi za kimataifa. Taratibu za ukamilishwaji wa makubaliano ya utoaji wa huduma za ushauri wa kihabari zinaendelea kati ya TSN na Wizara ya Kilimo; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi - INEC; Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Kilimanjaro, Lindi na Mtwara; Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha - AICC; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF; Shirika la Posta Tanzania - TPC; na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA;

vi. Kuanza ujenzi wa studio ya kisasa (multimedia studio) pamoja na ununuzi wa vifaa vya studio,

vii. Ununuzi wa magari sita (6) kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Kampuni ; na

viii. Kuanzisha na kutekeleza programu maalum ya mahojiano na viongozi wastaafu ijulikanayo kama 'Former Leaders Bench with Daily News". Jumla ya viongozi **12** wakiwemo Makamu wa Rais wastaafu, mawaziri wakuu wastaafu, maspika wastaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita wa Zanzibar wamefanyiwa mahojiano kwa lengo la kutoa mitazamo yao juu ya uongozi wa nchi hii kuanzia awamu ya kwanza hadi

sasa pamoja na kutoa elimu juu ya historia na masuala mbalimbali yanayohusu taifa kwa ujumla.

### 3.3.8. Tume ya UlInzI wa TaarIfa BInafsI (PDPC)

88. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24, Tume ilikadiria kupata na kutumia kiasi cha **Shilingi 500,000,000** kutoka Serikali Kuu ikiwa ni fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Ofisi. Hadi Aprili, 2024 Tume imepokea **Shilingi 254,166,666.65** sawa na **asilimia 50.8**

89. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili 2024 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kupata ofisi ya Tume Jijini Dodoma na Zanzibar;

ii. Ununuzi wa vifaa vya ofisi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Tume;

iii. Kujenga uwezo kwa wataalamu wa Tume na Wizara ikiwemo kufanya ziara za mafunzo katika nchi za Kenya, Ethiopia, Uganda, Nigeria, Ghana na Urusi;

iv. Kutengeneza na kuanza kutumia mifumo ya uendeshaji, ikiwemo kuwezesha usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi ambapo taasisi zaidi ya **300** zinaendelea katika hatua mbalimbali za usajili, pamoja na mfumo kwa ajili ya kuwezesha upokeaji wa malalamiko kuhusu ukiukwaji wa masharti ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kuyashughulikia; na

v. Kuandaa Mkakati wa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu shughuli za Tume na Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

### 3.3.9. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA– CCC)

90. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2023/24 Baraza lilipanga kukusanya Shilingi **710,000,000.00** kama tengeo kutoka Mamlaka

ya Mawasiliano Tanzania. Hadi Aprili, 2024 Baraza limepokea **Sh.532,500,000** sawa na **asilimia 75** ya lengo.

91. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili 2024 Baraza limetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kufanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) ili kuona namna bora zaidi ya kuliwezesha Baraza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Taarifa ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Baraza na kuimarisha vyanzo vya fedha limeandaliwa;

ii. Kujenga uwezo wa watumishi wawili (2) wa Baraza ili kukuza uwezo wao katika utekelezaji wa kazi;

iii. Kujengea uwezo Kamati za watumiaji wa huduma za mawasiliano katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Arusha, Tanga, Mwanza, Kagera, Kigoma, Tabora, Mtwara, Lindi, Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Manyara na Pwani ili kuongeza ufanisi katika kutumia mfumo wa kidijitali (mtumiaji app/portal) wa kuwasilisha maoni, changamoto na hoja za watumiaji katika utekeleza majukumu yao;

iv. Kuunda mfumo wa Mtumiaji App/Consumer Portal kwa lengo la kuwa na mfumo rafiki na rahisi kutumika na watumiaji katika kuwasilisha maoni na masuala yenye maslahi yao. Aidha, mfumo huu unatumika na Baraza kutoa elimu kwa watumiaji na Kamati za Watumiaji za Mikoa kutuma taarifa zao;

v. Kufanya Mikutano miwili **(2)** ya mashauriano na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano ya Simu (TAMNOA). Aidha, Baraza limewasilisha masuala ya watumiaji kwa watoa huduma kwa lengo la kufanyiwa maboresho;

vi. Kutoa elimu, kuhamasisha na kupokea maoni ya watumiaji kupitia vipindi vya Redio **21**, Televisheni 6. Aidha, watumiaji

8,503,640 wamefikiwa kupitia mitandao ya kijamii ya Baraza na watumiaji wenye ushawishi (social media influencers);

**SURA YA 04**

## 4.1 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

92. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2024/25 kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021.

### 4.1.1 Makadirio ya Mapato ya Wizara

93. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 100,700,000,000** ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, usajili wa Magazeti, ada ya mwaka ya Magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

### 4.1.2 Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

94. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inasimamia Mapinduzi ya Kidijitali yanayowezeshwa na TEHAMA na pia kuimarisha mfumo wa kupashana habari kwa kusimamia uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka Msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Ili kuwezesha mageuzi na mapinduzi haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi kwa kutunga na kuhuisha Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia

Sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini, kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao nchini, kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali, kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao, kuimarisha upatikanaji wa habari nchini, na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa (Startups).

### 4.1.3. Mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kuendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ili kuharakisha maendeleo kwenye Sekta ya Mawasiliano. Katika Mwaka 2024/25 sekta binafsi imepanga kushirikiana na Serikali katika kutekeleza majukumu ya kisekta kwenye maeneo yafuatayo:

i. Kampuni za simu za Airtel Tanzania, Vodacom Tanzania, Honora Tanzania na Halotel zimepanga kuendelea kushirikiana na Serikali kwenye ujenzi wa minara **627** ya mawasiliano ya simu kati ya minara **758** na kuendelea kuongeza uwezo kwenye minara **75** kati ya minara **304**. Aidha, kampuni hizi zimepanga kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa minara mipya **636** ya mawasiliano ya simu;

ii. Kampuni ya simu ya Airtel Tanzania imepanga kupeleka huduma ya Wi-Fi katika maeneo **16** kati ya **120** yaliyopendekezwa na Wizara kwa Mwaka 2024/25; Maeneo yatakayofikishiwa huduma ni: Vyuo, Masoko, Hospitali, Vituo vya mabasi na Stesheni za treni ya mwendokasi;

iii. Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) imepanga Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano nchini; na

iv. Kushirikiana na Serikali katika kukuza bunifu za TEHAMA na kukuza kampuni changa za TEHAMA.

### 4.1.4. Eneo la Habari – MAELEZO

96. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kukamilisha na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano;

ii. Ukamilishaji wa maboresho ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003;

iii. Kukamilisha na kusimamia uanzishwaji wa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Wanahabari;

iv. Kuisemea Serikali kuhusu programu na miradi inayotekelezwa na kuratibu ukusanyaji wa maoni ya wananchi;

v. Kuchapisha nakala 5,000 za jarida la nchi yetu na nakala 2,000 ya picha za Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere;

vi. Kukusanya na kusambaza habari kuhusu utekelezaji wa programu na miradi ya Serikali;

vii. Kuratibu mkutano wa mwaka wa Maafisa Mawasiliano Serikalini;

viii. Kuchapa na kutoa leseni za magazeti na vitambulisho vya Waandishi wa Habari;

ix. Kuratibu vyombo vya habari katika matukio mbalimbali ya kitaifa;

x. Kuhuisha Muundo wa Maafisa Habari Serikalini;

xi. Kuratibu Mikutano ya Taasisi, Mikoa na Halmashauri za Wilaya na Vyombo vya Habari; na

xii. Kuratibu na kufanya Tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma.

### 4.1.5. Eneo la Mawasiliano

97. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kukamilisha ujenzi wa minara ya mawasiliano ya Simu 616 na kufikia jumla ya minara **758** katika kata **713**;

ii. Kuratibu na kusimamia ujenzi wa minara mipya 636 ya mawasiliano ya simu;

iii. Kuendelea na utekelezaji wa Programu za Anga la Juu ikiwemo kuratibu uanzishaji wa Wakala ya Anga la Juu nchini (Tanzania Space Agency) kwa ajili ya kukuza matumizi ya teknolojia za Setelaiti katika kuwezesha urahisi na unafuu katika upatikanaji wa huduma za mawasiliano na huduma nyingine ikiwemo ulinzi na usalama, tafiti, kukabiliana na majanga na utabiri wa hali ya hewa nchini;

iv. Kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Ushiriki wa Tanzania Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano;

v. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kuvutia Uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano;

vi. Kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uwekezaji katika mawasiliano nchini ili kuandaa Mkakati wa Kukuza Uwekezaji katika Mawasiliano Nchini;

vii. Kusimamia ukamilishwaji wa taratibu za ujenzi wa Kituo cha Kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha Biashara Mtandao;

viii. Kusimamia uundaji wa mfumo wa kidijitali utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce); na

ix. Kufanya uchanganuzi wa hali ya mpango wa upelekaji wa miundombinu ya posta na kuandaa mpango wa kufikisha miundombinu hiyo kote nchini;

### 4.1.6. Eneo la Miundombinu ya TEHAMA

98. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia Shirika la Mawasiliano Tanzania pamoja na usimamizi wa ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

ii. Kufanya mapitio ya mwongozo wa miundombinu muhimu ya TEHAMA;

iii. Kutayarisha Mpango Kabambe wa Miundombinu ya Kitaifa ya TEHAMA; na

iv. Kufanya upembuzi yakinifu katika ukuzaji miundombinu ya kidijitali ya kitaifa.

### 4.1.7. Eneo la Uendelezaji wa Mifumo na Huduma za TEHAMA

99. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuratibu maandalizi ya Sheria ya TEHAMA itakayojumuisha maeneo ya Teknolojia zinazoibukia ikiwemo Teknolojia ya Akili Mnemba (AI);

ii. Kujenga mfumo wa kufungamanisha taarifa za kila mwananchi ili kuwa na akaunti ya kidijitali (Mwananchi/Jamii Profile) itakayomwezesha kutumia huduma mbalimbali za kidijitali nchini;

iii. Kuendelea kusimamia uanzishwaji wa Vyuo viwili (2) vya TEHAMA Jijini Dodoma na Buhigwe Kigoma;

iv. Kuwaendeleza wataalam 30 wa TEHAMA kwenye programu za muda mrefu na wataalam 450 kwenye programu za muda mfupi;

v. Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na taasisi binafsi ili kutumia bunifu za kidijitali zilizopo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

vi. Kuendelea na uratibu wa uendelezaji wa Mifumo ya Kitaifa nchini;

vii. Kuratibu tafiti za TEHAMA nchini na kuendelea kusimamia Mkakati wa matumizi ya Tafiti za TEHAMA nchini; na

viii. Kuandaa Miongozo mbalimbali ya kuwezesha matumizi ya TEHAMA Nchini.

### 4.1.8. Eneo la Usalama Mtandao

100. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia usajili na usimamizi wa Miundombinu Muhimu ya TEHAMA nchini;

ii. Kuanzisha Kituo kimoja cha usalama wa Mawasiliano cha Taifa;

iii. Kuhuisha mfumo wa takwimu za makosa na matukio ya mtandao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Mahakama;

iv. Kuongeza uwezo wa Kitengo cha Uchunguzi wa Kidijitali kwa Jeshi la Polisi katika ofisi ya makao makuu ya Dar es Salaam na Kanda ya Zanzibar.

v. Kuhuisha Mkakati wa Elimu kwa Umma wa Usalama wa Mtandao 2024/25-2027/28; na

vi. Kutengeneza Mkakati wa ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili mtandaoni.

### 4.2. MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

101. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha Serikali inaharakisha kuwa na Jamii yenye habari sahihi na iliyowezeshwa Kidijitali kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakusudia kutekeleza Miradi tisa (9) ikiwa na dhima ya kuwezesha utoaji wa huduma za uhakika na za gharama nafuu za Habari, Teknolojia ya Habari, Mawasiliano ya simu na Posta kwa kuweka mazingira yanayokuza ubunifu katika kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa Kidijitali, miradi hiyo ni:

#### 4.2.1. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

102. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25 Wizara imekadiria kutumia Shilingi **80,700,000,000** kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi huu ni:

i. Kuwezesha utengenezaji wa mfumo wa Kitaifa wa Miundombinu ya Mawasiliano ya TEHAMA Kijiografia (Broadband Geographical Information System);

ii. Kuwezesha ujenzi wa kituo cha Kitaifa cha Kuhifadhi Data Dodoma na Zanzibar;

iii. Kuendeleza na kutekeleza miundombinu ya Mkongo wa mwisho (Last Mile Optic Fiber) kwa taasisi **100** za haki za jinai, Taasisi za Ulinzi na Usalama (Mahakama, TAKUKURU, Polisi, Magereza, JWTZ, Usalama) na Taasisi nyingine za Serikali;

iv. Kuunganisha taasisi za haki jinai, Taasisi za Ulinzi na Usalama (Mahakama, TAKUKURU, Polisi, Magereza, Jeshi la Wananchi Tanzania) na taasisi nyingine za Serikali (vituo vya afya, shule) kwenye mikongo ya mwisho (last mile connectivity) na kusimamia uunganishaji wa Wilaya **40**, Taasisi na nyumba **200,000**;

v. Kuwezesha usakinishaji (installation) na uboreshaji wa vifaa vya mikutano ya video (Video Conference) katika Wilaya **100**;

vi. Kufuatilia ujenzi wa Kilometa **186** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) kutoka Kigoma hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

vii. Kusakinisha ufikiaji wa Wi-Fi katika maeneo **50** ya umma nchini;

viii. Kufanya upembuzi yakinifu kwa programu ya Kitaifa ya ukuzaji wa Miundombinu ya kidijitali;

ix. Kufanya Jaribio la kukubalika kwa Muda (PAT) na Jaribio la Kukubalika kwa Kiwanda (FAT) kwa miundombinu ya brodibendi iliyosakinishwa;

x. Kufanya Ufuatiliaji wa miundombinu ya broadband;

xi. Kusimamia ujenzi wa kituo cha TEHAMA Mji wa Serikali Mtumba; na

### 4.2.2. Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu

103. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umelenga kuboresha na kuimarisha uwezo wa wataalaam ndani ya Wizara katika matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, kutoa elimu kwa wananchi kutambua uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na matumizi ya TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na salama ya TEHAMA yanayozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika Mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 3,089,894,000** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Fedha hizo zimekusudia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi nane (8) ya Wizara ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi na kwa namna itakayoleta tija;

ii. Kuandaa agenda ya utafiti na miongozo katika eneo la utafiti na ubunifu katika TEHAMA;

iii. Kubainisha maeneo ya kipaumbele kwenye TEHAMA ya kufanyiwa tafiti;

iv. Kuchambua na kubaini vihatarishi katika Sekta, kuandaa mpango wa kukabiliana navyo na kusimamia utekelezaji wa mpango;

v. Kutoa mafunzo kwa viongozi na wataalam kuhusu namna bora ya kusimamia vihatarishi wakati wa utekelezaji wa majukumu;

vi. Kufanya maandalizi ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na kusambaza kwa wadau;

vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli katika Idara tano (5), Vitengo nane (8) na Taasisi tisa (9);

viii. Kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za Sekta;

ix. Kuwezesha na kuratibu mkutano wa mapitio ya utendaji wa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na

x. Kuwajengea uwezo watumishi 70 wa Wizara na Taasisi kuhusu ufuatiliaji na tathmini.

### 4.2.3. Mfumo wa Anwani za Makazi

104. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25 Wizara imekadiria kutumia Shilingi **11,500,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuratibu utungaji wa Sheria ya Anwani ya Makazi na kuhuisha sheria zilizopo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi;

ii. Kuwezesha Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA) kuunganishwa na mifumo mingine ya kutolea huduma za kijamii;

iii. Kukamilisha zoezi la kuhakiki taarifa za Anwani za Makazi;

iv. Kuboresha mfumo wa kidijitali wa Anwani za Makazi ili kuendana na viwango vya kimataifa vya mifumo ya Anwani za Makazi;

v. Kujenga uwezo kwa wataalam na Watendaji **31,465** katika Halmashauri **167** nchini kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi;

vi. Kuhamasisha matumizi na kuelimisha umma kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi;

vii. Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi; na

viii. Kuwezesha usimamizi katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi.

#### 4.2.4. Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Parks)

105. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuimarisha na kuendeleza ujuzi kwa wabunifu katika masuala ya TEHAMA nchini kwa lengo la kukuza vipaji na kuongeza wigo wa vijana kujiajiri katika shughuli mbalimbali za TEHAMA. Kwa mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 4,000,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi zifuatazo:-

i. Kufanya tathmini ya ujenzi wa Chuo cha TEHAMA;

ii. Kuwezesha ujenzi wa vyuo viwili (2) vya TEHAMA vya Nala – Dodoma na Buhigwe – Kigoma;

iii. Kuwezesha mafunzo kwa watumishi 25 katika TEHAMA;

iv. Kuratibu ufundishaji wa programu ya anga za juu katika taasisi mbili (02) za elimu ya juu nchini;

v. Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Anga la Juu (Outer Space Strategy);

vi. Kuratibu uridhiwaji wa Mkataba wa Anga la Juu;

vii. Kuwezesha uboreshwaji wa maabara za kiuchunguzi wa kidijiti kwa Jeshi la Polisi katika ofisi ya makao makuu ya Dar es Salaam na Kanda ya Zanzibar;

viii. Kuwezesha utekelezaji wa Kituo cha Taifa cha Operesheni za Mtandao;

ix. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miongozo mitano (5) ya Miundombinu Muhimu ya TEHAMA;

x. Kuratibu mapitio ya Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015;

xi. Kuwezesha uandaaji wa Mkakati wa Kumlinda Mtoto Mtandaoni;

xii. Kuwezesha uboreshwaji wa maabara ya uchunguzi wa kidijitali katika Kitengo cha Makosa ya Mtandao Dar es Salaam na Zanzibar;

xiii. Kuwezesha mafunzo kwa awamu nne (4) ya Kamati ya Kitaifa ya Mawasiliano ya Usalama Mtandaoni; na

xiv. Kuratibu uhuishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mawasiliano ya Usalama wa Mtandao.

**4.2.5. Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Project)**

106. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi **24,850,000,000** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi zifuatazo:

i. Kuwezesha ujenzi wa Vyuo vya TEHAMA Nala - Dodoma na Buhigwe - Kigoma;

ii. Kukamilisha usakinishaji, uanzishwaji na matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (Jamii Data Lake) nchini;

iii. Kufanya upembuzi yakinifu wa kusimika Mfumo wa Miji Janja (Smart Cities) katika miji ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

iv. Kuwezesha mafunzo kwa wataalam **150** wa TEHAMA kutoka Wizara, Mikoa, Idara zinazojitegemea na Wakala pamoja na Serikali za Mitaa kuhusu teknolojia zinazoibukia (emerging technologies);

v. Kufuatilia utekelezaji wa afua za uchumi wa kidijitali; na

vi. Kuunganisha taasisi 891 katika mtandao wa Serikali.

### 4.2.6. Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

107. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia Shilingi **2,100,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea na uanzishwaji wa kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA (ICT Refurbishment and Assembly centre);

ii. Kuendelea kuwezesha uanzishaji na ukuzaji wa vituo vya ubunifu vya TEHAMA katika Wilaya sita **(6)** kwa kuanzia (District ICT Startups Innovation hubs);

iii. Kuendeleza uwezo wa wataalam wa TEHAMA ili kuendana na ukuaji wa teknolojia;

iv. Kujenga maabara za Akili Mnemba (AI) na matumizi ya Roboti nchini;

v. Kuandaa viwango vya matumizi ya TEHAMA Tanzania;

vi. Kuboresha mfumo wa kuwatambua na kuwasajili watalaam wa TEHAMA nchini; na

vii. Kuendelea kufanya utafiti kuhusu muelekeo wa maendeleo ya TEHAMA nchini.

### 4.2.7. Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

108. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia Shilingi **9,800,000,000** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi zifuatazo:

i. Upanuzi wa usikivu wa redio za TBC kwa kujenga mitambo ya redio yenye masafa ya FM kwenye Wilaya saba **(7)**;

ii. Ununuzi wa magari **15** kwa ajili ya shughuli za utangazaji katika vituo vipya vya kurushia matangazo ikiwemo kuwezesha kutangaza shughuli za Uchaguzi Mkuu na wa Serikali za Mitaa;

iii. Ununuzi wa magari mawili **(2)** maalumu ya kurushia matangazo mbashara (OB Van); na

iv. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kurushia matangazo mbashara kwa idhaa zake za redio na televisheni kwenye idhaa za TBC1, TBC2, Safari Chaneli, TBCMtandao na televisheni ya Kiingereza kwa mtandao awamu ya tatu **(3)**.

### 4.2.8. Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji

109. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia Shilingi **5,000,000,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo za mradi:

i. Kukamilisha ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji;

ii. Kukamilisha ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kisasa ya uchapaji;

iii. Ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Kampuni; na

iv. Ununuzi wa malighafi kwa ajili ya shughuli za uchapaji.

### 4.2.9. Mradi wa Habari kwa Umma

110. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2024/25 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 980,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo za mradi:

i. Kuandaa na kusambaza makala za televisheni kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri **184** kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;

ii. Kujenga Kituo cha Habari kitakachojumuisha ofisi, kumbi za mikutano, maktaba ya kidijitali na studio; na

iii. Kuanzisha na kuendesha chaneli ya televisheni ya Serikali itakayokuwa ikitangaza shughuli za utekelezaji wa Serikali kama vile matukio ya kitaifa na kimataifa, mikutano, ziara na mikutano na Waandishi wa Habari.

### 4.3. MIPANGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

111. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zimekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 786,663,818,024.99** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Mchanganuo wa makusanyo na shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

### 4.3.1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

112. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2024/25, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inatarajia kukusanya **Shilingi 201,736,566,472.99** kutokana na vyanzo vya ada za leseni, ada za masafa, matumizi ya namba za mawasiliano, Mfumo wa Kusimamia Mawasiliano ya Simu (CMS) na ada za uhakiki wa vifaa vya kielektroniki.

113. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa huduma za mawasiliano ili kuhakikisha kuwa huduma hizo zinatolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na kwa kuzingatia masharti ya leseni;

ii. Kuimarisha ukusanyaji wa ada za kiudhibiti ili kuhakikisha usimamizi wa huduma bora za mawasiliano;

iii. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wa TCRA ikiwemo kuwapatia mafunzo endelevu ili kukuza uwezo wao katika utekelezaji wa kazi za kiudhibiti;

iv. Kuimarisha usimamizi wa Mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano;

v. Kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao;

vi. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (NPKI) ili kuhakikisha usalama wa miamala ya kielektroniki nchini;

vii. Kuweka mazingira wezeshi ya uchumi wa kidijitali kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za mawasiliano;

viii. Kuendelea kuimarisha mifumo ya kiudhibiti na kupima ubora wa huduma za mawasiliano ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na usimamiaji wa Sekta;

ix. Kufuatilia, kujibu na kuripoti matukio ya usalama wa kimtandao ili kupunguza mashambulizi;

x. Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia zinazoibuka (emerging technologies) kwa ajili ya kufanya maboresho yanayostahili katika kuisimamia sekta kwa ufanisi;

xi. Kudhibiti ulaghai katika mitandao ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji sahihi wa mapato ya Serikali kutoka kwenye miamala ya simu kutoka nje ya nchi (International Incoming traffic); na

xii. Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za TCRA Dodoma na Zanzibar.

### 4.3.2. Shirika la Posta Tanzania (TPC)

114. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Shirika la Posta Tanzania linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 43,415,885,000** ambapo **Shilingi 39,415,885,000** zitatoka katika vyanzo vyake vikuu ikiwemo; huduma za barua, fedha na uwakala, biashara ya kubadili fedha za kigeni, barua za haraka (EMS), miliki (real estate), biashara mtandao (e-business) na huduma za usafirishaji (logistics services) na **Shilingi 4,000,000,000** kutoka Serikalini na Umoja wa Posta Duniani (UPU).

115. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2024/25, Shirika la Posta Tanzania limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutengeneza na kutumia mfumo wa kukusanya na kusambaza mizigo ("uberlike" pick and delivery system);

ii. Kuanzisha matumizi ya magari ya umeme na kubadilisha magari yanayotumia mafuta ili kupunguza gharama za uendeshaji;

iii. Kuanzisha kituo cha kudhibiti na kusimamia usafirishaji (logistics main and backup control center);

iv. Kuboresha kituo cha mawasiliano kwa wateja wa ndani na nje (customer call center);

v. Kutengeneza na kutumia programu ya kufuatilia mauzo (sales tracking application) kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato; na

vi. Kutengeneza na kutumia Mfumo wa Mipango ya Rasilimali za Kampuni;

vii. Kutekeleza mradi wa kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

viii. Kuimarisha uendeshaji wa biashara ya kusafirisha sampuli wenye tija kwa kushirikiana na wadau nchi nzima; na

ix. Kutengeneza na kutekeleza mfumo wa Posta Cash e-Wallet ambao unawawezesha mawakala kuweka na kutuma fedha.

**4.3.3. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

116. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2024/25, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 377,912,000,000** kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

117. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Shirika la Mawasiliano Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuunganisha Wilaya na Halmashauri zote nchini na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

ii. Kuunganisha eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

iii. Kufungua huduma za kituo cha data katika Mikoa mitano **(5)** ya kibiashara ya posta; na

iv. Kuunganisha watoa huduma **10** wa biashara za kielektroniki kupitia (mini-apps) kwenye programu tumizi ya T-PESA ili kuwasogezea wateja huduma kwa kutumia mfumo mmoja wa Super App.

### 4.3.4. Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

118. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2024/25 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linakadiria kuwa na mapato ya **shilingi 43,494,079,840** ambapo **Shilingi 14,685,810,840** ni makusanyo ya ndani na **Shilingi 28,808,269,000** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya mapato ya ndani ni pamoja na matangazo ya biashara yatokanayo na chaneli zake za redio na televisheni ikiwemo mitandao ya kijamii.

119. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Shirika la Utangazaji Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Upanuzi wa usikivu wa redio za TBC kwa kujenga mitambo ya redio yenye masafa ya FM kwenye wilaya saba (7);

ii. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la makao makuu ya TBC eneo la Vikonje Jijini Dodoma kwa **asilimia 82** zilizobaki;

iii. Ununuzi wa magari **15** kwa ajili ya shughuli za utangazaji ikiwemo vituo vipya vya kurushia matangazo;

iv. Ununuzi wa magari mawili (2) maalum ya kurushia matangazo mbashara (OB Van);

v. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kurushia matangazo mbashara kwa idhaa zake za redio;

vi. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kurushia matangazo mbashara ya Televisheni kwenye idhaa za TBC1, TBC2, Safari Chaneli, TBCMtandao na televisheni ya Kiingereza kwa mtandao awamu ya tatu; na

vii. Kubadilisha mifumo ya vifaa vya utangazaji vyenye muda mrefu katika vituo vya Utangazaji vya TBC Nyashana - Mwanza, Kaze Hill - Tabora, Mkendo - Musoma, Mnyusi - Tanga na Singida kwa ajili ya upanuzi wa usikivu wa redio.

**4.3.5 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**

120. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2024/25 Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kukusanya **Shilingi 26,831,676,908.00** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya uendeshaji wa Kampuni pamoja na ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida.

121. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika Mwaka 2024/25:

i. Kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma zitolewazo na Kampuni kwa **asilimia 30**;

ii. Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha uchapaji na kufunga mitambo ya kisasa ya uchapaji;

iii. Kuendesha Programu nne **(4)** za mafunzo na kuwajengea uwezo Waandishi wa Habari juu ya habari za kiuchunguzi na uandishi wa kitakwimu;

iv. Kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi Zanzibar;

v. Kuhuisha na kuunganisha mifumo wezeshi ya kiutendaji ya Kampuni ikiwemo mifumo ya fedha, biashara na utawala kuwa ya kidijitali;

vi. Kuunganisha Taasisi na mashirika kwenye huduma ya magazeti Mtandao; na

vii. Kutekeleza mpango kabambe wa kuhabarisha umma kupitia magazeti yake ya Daily News, HabariLEO na mitandao yake ya kijamii kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali kuanzia mwaka 2020.

#### 4.3.6. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

122. **Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 43,614,542,504** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni tozo ya huduma na tengeo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

123.**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea na ujenzi wa minara **758** katika kata **713** kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali;

ii. Kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo 70 ya kimkakati mathalan maeneo ya hifadhi na mipakani

iii. Kuiongezea nguvu minara **135** kutoka teknolijia ya 2G kwenda 2G/3G na/au 4G;

iv. Kuboresha Huduma za matangazo ya TBC Radio katika maeneo mawili (2) ya mipakani;

v. Kuboresha Redio Jamii katika Halmashauri tatu (3);

vi. Kupeleka vifaa vya TEHAMA katika shule **100**;

vii. Kutoa vifaa vya TEHAMA katika vyuo **10** vyenye wanafunzi wenye mahitaji maalum;

viii. Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu **300** wa shule za Sekondari;

ix. Kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo **25** ya wazi; na

x. Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za Posta.

#### 4.3.7. Tume ya TEHAMA (ICTC)

124. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2024/25, Tume ya TEHAMA inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 6,428,707,300** ambapo **Shilingi**

**4,328,707,300** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 2,100,000,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

125. **Mheshimiwa Spika**, ili kuharakisha mapinduzi ya kidijitali, Mwaka 2024/25 Tume ya TEHAMA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kuendelea na uanzishaji na ukuzaji wa vituo sita (6) vya ubunifu wa TEHAMA katika Kanda Tano **(5)** na kituo kimoja **(1)** Zanzibar; pamoja na vituo sita **(6)** vya Wilaya (District ICT Startups Innovation hubs) kwa kuanzia;

ii. Kuendelea na uanzishwaji wa vituo viwili (2) vya kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA (ICT Refurbishment and Assembly centres) katika Majiji ya Arusha na Dar es Salaam;

iii. Kuendelea kufanya tafiti mbili (2) kuhusu muelekeo wa maendeleo ya TEHAMA nchini;

iv. Kuandaa viwango vya kidijitali vya TEHAMA;

iv. Kuendelea kufanya tafiti mbili (2) kuhusu muelekeo wa maendeleo ya TEHAMA nchini;

v. Kuandaa viwango vya kidijitali vya TEHAMA;

vi. Kuboresha mfumo wa kielektroniki wa kuwatambua, kuwasajili na kufuatilia mienendo ya utendaji ya watalaam wa TEHAMA nchini;

vii. Kuanzisha programu maalum ya TEHAMA kwa vijana kwa lengo la kukuza ujuzi wa TEHAMA nchini katika ngazi zote;

viii. Kufanya tathmini ya uanzishwaji wa “Kiswahili Large Language Model” ya kitaifa na meterverse studio;

ix. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati ya uwekezaji na uendelezaji wa TEHAMA nchini; na

x. Kuendeleza bunifu za TEHAMA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa ndani na wa nje.

### 4.3.8. Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)

126. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2024/25 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imepanga kukusanya na kutumia Shilingi **21,800,000,000**. Kati ya fedha hizo Shilingi **21,000,000,000** ni mapato ya ndani na Shilingi **800,000,000** ruzuku kutoka Serikali Kuu.

127. **Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha usalama na ulinzi wa taarifa za watumiaji wa huduma, Mwaka 2024/25 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi itatekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi **500,000**;

ii. Kuimarisha mifumo ya usajili; kupokea malalamiko na rejesta ya wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi;

iii. Kuimarisha upimaji wa utendaji kazi wa watumishi waliopo na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

iv. Kujenga uwezo watumishi **30** wa Tume katika masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

v. Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

vi. Kuimarisha na kukuza mahusiano na wadau wa ndani na nje ya nchi katika masuala yanayohusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

vii. Kuimarisha mazingira ya kuendeleza ubunifu na kufanya tafiti za kimkakati za njia bora za ulinzi wa taarifa binafsi kupitia Vyuo Vikuu, Vituo vya Tafiti, Asasi na Sekta binafsi;

viii. Kufanya ukaguzi kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi **50** juu ya uzingatiaji wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

ix. Kupokea na kutatua malalamiko yanayohusu masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka kwa wahusika wa taarifa;

x. Kufanya na kuchapisha tafiti tatu **(3)** zinazohusu masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

xi. Kuwezesha ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; na

xii. Kuwezesha ununuzi wa magari 12 na pikipiki tano **(5)** kwa ajili ya kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake.

### 4.3.9. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)

128. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2024/25, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) linatarajia kupokea kiasi cha **Shilingi 710,000,000** kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

129. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25 Baraza limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kufanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano kwa lengo la kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

ii. Kuziwezesha Kamati za Watumiaji katika mikoa 21 kwa kuzipatia vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu;

iii. Kuwajengea uwezo Kamati za watumiaji katika Mikoa **20**;

iv. Kuendelea kuimarisha na kutumia mifumo ya mawasiliano ya kidijitali (e-mrejesho & Mtumiaji App/Portal) ili kuboresha utendaji kazi wa Baraza na kuimarisha mawasiliano na watumiaji;

v. Kuendelea kuandaa na kutoa elimu, uhamasishaji na kupokea maoni ya watumiaji kupitia redio, televisheni, mitandao ya kijamii, maadhimisho ya Wiki ya Mtumiaji,

maonesho na matukio ya Kitaifa ili kuongeza uelewa wa watumiaji;

vi. Kushiriki katika Mikutano na mashauriano na TCRA na Mabaraza mengine matatu (3) ya Watumiaji.

vii. Kufanya mashauriano na wadau wa sekta kwa kila robo mwaka kwa lengo la kutatua changamoto za watumiaji na kuboresha huduma; na

viii. Kuendelea kuwapa watumishi wa Baraza mafunzo endelevu ili kukuza uwezo wao kwa utekelezaji wa kazi.

**SURA YA 05**
**HITIMISHO**
**5.1. SHUKURANI**

130. **Mheshimiwa Spika**, Kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi (Mb.), Naibu Waziri; Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu na Nicholaus Merinyo Mkapa, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Habari na TEHAMA.

131. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue fursa hii kipekee kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta za Habari na Mawasiliano. Washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA), Ubalozi wa Korea Kusini nchini na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

132. **Mheshimiwa Spika**, ningependa pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda na kimataifa yanayohusu sekta hii. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025. Kwa upekee niyatambue makampuni ya mawasiliano ya simu ya Vodacom Tanzania, Airtel Tanzania, Honora Tanzania, Halotel, TISPA na TTCL kwa kusambaza huduma za mawasiliano nchini. Vilevile, napenda kuzitambua taasisi za kifedha ikiwa ni pamoja na benki ya CRDB, NMB, TSA kwa mchango wao katika kukuza bunifu za TEHAMA nchini. Pia napenda kuvishukuru vyombo vya Habari vyote pamoja na Jumuiya zake ikiwemo MOAT, TAMWA, MCT, UTPC, MISA Tan, TADIO, TMF, TEF, JOWUTA, JUMIKITA na Jamii Forums kwa kuendelea kuhabarisha umma. Kwa kumalizia natambua mchango wa wadau wote wa Sekta ikiwemo Kampuni ya Minara Tanzania, Herios Tower, Huawei, Softnet, Telecom Associate, TanzTech pamoja na Raddy Fibre

133. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Mwaka 2024/25, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025.

## 5.2. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25

134. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 180,926,557,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:-

135. **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz.

136. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo ndani ya Bunge, wageni wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Kamati ya Siasa Mkoa wa Mbeya, Mwenyekiti wa Mkoa - Ndugu Patrick Mwalungenge; Katibu Mwenezi - Ndugu Christopher Uhangile; Mwenyekiti UWT Mkoa - Bi. Edina Mwahigomole; Mwenyekiti Wazazi - Ndugu James Mwanampondele; Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Mbeya - Ndugu Yassin Ngonyani; Ndugu Fortunas Mjengwa na Alutani Mwasele, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa hii kwa ukamilifu wake iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

(b) Sehemu ya Pili ni Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na

(d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msingi na mawanda ya uchambuzi; kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilichambua taarifa za utekelezaji Fungu 68 - Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2). Katika ulinganisho huo, Kamati ilitathmini mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi uliofanyika kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati imezingatia masuala muhimu yanayogusa Sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa Wizara kuhakikisha inachangia utekelezaji bora wa Ibara ya 18 ya Katiba ambayo pamoja na masuala mengine, inaweka haki kwa kila mtu kutafuta, kupokea na kutoa habari, kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na masuala muhimu ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 212.457 ili kutekeleza malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 190.794 sawa na 89.8% ya bajeti iliyoidhinishiwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kielelezo namba moja kinafafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara ni ya kuridhisha kwani hadi kufikia Februari, 2024, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni juu ya wastani wa 75%. Aidha, Kamati imeridhishwa na mapokezi ya fedha za maendeleo ambayo ni 94.6% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 150.7 wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 619.461. Fedha hizo zilitarajiwa kutokana na vyanzo vifuatavyo:-

(a) Ada na tozo;
(b) Mauzo ya picha za viongozi;
(c) Mauzo ya masafa;
(d) Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(e) Marejesho ya fedha za umma;
(f) Vitambulisho vya Waandishi wa Habari;
(g) Nyaraka za zabuni;
(h) Ukumbi wa mikutano; na
(i) Usajili wa magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikusanya shilingi bilioni12.874 sawa na 8.5% ya lengo. Wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya jumla ya shilingi 438.652 sawa na 70.81% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani, hali ya makusanyo ya Wizara siyo nzuri. Mfano, Wizara ilitarajiwa kwamba mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee ungeweza kuipatia mapato ya takribani shilingi bilioni 150.245. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2024 ni shilingi bilioni 12.812 tu sawa na 8.5%. Kamati ilitaarifiwa kwamba sababu za kutofikiwa malengo haya ni uwezo mdogo *(Capacity)* wa Mkongo wa Taifa

wa Mawasiliano ambapo Wizara imeshindwa kuuza na hivyo kuilazimu Serikali kuchukua hatua za kuongeza uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara unaridhisha kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2024 makusanyo yalikuwa ni 70.81%. Pamoja na hali hiyo, Kamati imebaini masuala kadhaa kuhusu mwenendo wa makusanyo ambapo baadhi ya taasisi zimefanya vizuri katika ukusanyaji na kuvuka malengo wakati taasisi nyingine hazikufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi tano chini ya fungu hilo zimefanya vizuri kwa kukusanya kati ya 65% hadi 111.2% na Taasisi 3 zimekusanya chini ya 50%. Kielelezo Na. 2 kinafafanua hali ya mwenendo wa makusanyo ya kila taasisi; mfano wa taasisi yenye makusanyo ya kuridhisha ni *TCRA* kwani hadi kufikia Februari, 2024 ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 245.917 ambayo ni sawa na 111.2% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, ongezeko la makusanyo haya limesababishwa na kuboreshwa kwa mifumo ya ndani ya utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato ikiwemo "*Tanzanite Portal*" na kuboreshwa kwa zoezi la kuwajua wateja *"Know your Customer (KYC)"* na makusanyo ya mwisho ya masafa sawa na shilingi milioni 118.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine zilizokusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha ni *UCSAF* 99.28%, *ICTC* 84.86%, *TCRA-CCC* 75.10%, *TBC* 66.52% kama ambavyo imeainishwa katika Kielelezo Na. 2. Kamati inazipongeza taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali kwa taasisi ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha yenye chini ya 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa shilingi bilioni 30.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 18.522 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 11.981 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 18.626 sawa na 61% ya lengo la matumizi ya kawaida. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 13.039 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 5.586 ni kwa matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 181.953 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 146.777 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 35.176 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo shilingi bilioni 172.168 zilipokelewa sawa na 94.6% ya lengo; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 83.592 ni fedha za ndani sawa na 48.55% na shilingi bilioni 88.576 ni fedha za nje sawa na 51.45%

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba kuna miradi mitano ilipokea fedha pungufu chini ya 50%, mfano Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji *(TSN)* 7.9%, Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* 20.4%, Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi 24.4%, Ujenzi wa *ICT Parks* 31.7% na Habari kwa Umma 47.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatoa fedha kwa ukamilifu, kwa miradi yote ili kuchochea utekelezaji wa miradi kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi na vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 12 hadi 17 Machi, 2024 Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathmini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo. Taarifa ya kina kuhusu ukaguzi na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inapatikana katika ukurasa wa 16 hadi 22 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muundo wa bajeti kwa mwaka 2024/2024; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu Na. 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 178,426,557,000.00 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 36,406,663,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 142,019,894,000.00 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kielelezo Na. 4 kimebainisha tofauti ya makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara imepungua kwa 16.02% kutoka shilingi bilioni 212 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia shilingi bilioni 178 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Fedha ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa 19.35%, fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo imepungua kwa 21.95%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za matumizi ya kawaida kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/204, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 786.663. Kiwango hiki ni ongezeko la 26.99% ukilinganisha na shilingi bilioni 619.461 iliyopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kielelezo Na. 5 kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi chini ya Wizara ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea Uchumi. Kwa zile taasisi

ambazo katika mwaka wa fedha 2023/2024 hazikutimiza malengo ya makusanyo kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa katika Kielelezo Na. 5, Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 19.35% ukilinganisha na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa fedha za matumizi mengineyo kutoka shilingi bilioni 30.5 hadi shilingi 36.4; Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 24.997 ni kwa ajili ya mishahara, na shilingi bilioni 11.4 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 142,019 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa 21.95% ukilinganisha na Bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika Kielelezo Na. 7; kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 116.469 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 25.550 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba shilingi bilioni 80.7 zilizotengwa kwenye mwaka wa fedha za ndani ni kwa ajili ya kutekeleza miradi Na. 4283 wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ikiwa ni nyongeza ya 0.88% ukilinganisha na shilingi bilioni 80 zilizotengewa kutekeleza mradi huo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sehemu ya dhima ya Wizara ni kuweka mazingira yanayokuza ubunifu kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa kidigitali, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ili kuwezesha ujenzi wa mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uweze kufika hadi nchi za jirani na kuongeza makusanyo na pato la nchi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa jumla; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina

mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ukuaji wa Uchumi; Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo: -

(a) Kamati imebaini kwamba, katika mwaka wa fedha 2023/2024 bajeti ya matumizi ya maendeleo imepungua kwa 21.95%. Kamati inashauri kwamba Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi na kuhakikisha fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati na kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(b) Kamati imebaini kwamba, fedha za matumizi mengineyo zimeongeza kwa 19.35%. Kamati inashauri kwamba, Serikali kuwa wabunifu wa namna bora ya utekelezaji wa majukumu yao ili kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa zitumike kwa malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri mahususi, Kamati inapongeza hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kukabidhi uendeshaji wa Mkongo Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*. Pamoja na pongezi hizo, suala la ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unahusisha usimikaji wa nguzo za zege na uvutaji wa nyaya za faiba. Kamati inashauri, Serikali kupitia upya mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaotekelezwa kati ya *TTCL* na *TANESCO*, ili kuona namna bora ya kuondoa upungufu uliopo na kukamilisha ujenzi huo kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Serikali iharakishe mchakato wa kupeleka Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuongeza pato la nchi. Aidha, inaendelea kuisisitiza kwamba, *TTCL* waendelee kushughulikia changamoto zilizopo ili waweze kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC),* Vikonje. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya maendeleo kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kwa lengo la

kuwezesha Shirika kujenga na kuboresha miundombinu. Pamoja na jitihada hizo, Kamati inashauri kwamba:-

(a) Serikali iendelee kuongeza bajeti ya *TBC* na fedha itolewe kwa wakati;

(b) Serikali iendelee kusimamia wakandarasi na kuhakikisha kuwa, wanalipwa fedha kwa wakati na gharama za ujenzi ziendane na uhalisia;

(c) Serikali ihakikishe kwamba, ujenzi wa miundombinu ya barabara ya kuingia kwenye eneo la mradi inarekebishwa kwa wakati ili kuondoa usumbufu wa kufika eneo husika;

(d) Serikali isimamie zoezi la ulipaji fidia kuwa linakamilika kwa mwananchi aliyebaki kwenye eneo la mradi; na

(e) Kutokana na dhana ya wajibu wa kurejesha fadhila kwa jamii *(CSR)*, Serikali ihakikishe kwamba, kwenye mikataba ya miradi, kiwepo kipengele kitakachowabana wakandarasi kutenga kiasi cha fedha za *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa minara ya mawasiliano nchi nzima. Pamoja na pongezi, Kamati inashauri kwamba Serikali itoe fedha za kutosha na kwa wakati kwa *UCSAF* ili kutekeleza azma ya ujenzi wa minara 758 nchini kote ili kupata usikivu wa mawasiliano nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa mikakati ya kuanzisha vituo mbalimbali vya kuleta ubunifu wa TEHAMA nchini; pamoja pongezi hizo Kamati inashauri kwamba Serikali iongeze kasi ya utekelezaji na uanzishaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Hitimisho. Katika ukuaji wa uchumi wa nchi, Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ni muhimu sana kwani huwezesha sekta nyingine zote kufikia malengo waliyojiwekea. Uwekezaji katika sekta hizi ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo, ni muhimu Serikali

kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Ibara ya 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili ukisaidiwa na Wenyeviti wa Bunge na kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha uliofanikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natumia fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao maoni yao, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akisaidiwa na Mheshimiwa *Eng*. Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge, Naibu Waziri, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi cha uchambuzi wa bajeti. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Mohammed Khamis Abdullah, na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholaus Mkapa kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara walipohitajika kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa niaba ya Sekretarieti na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na

Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 68 – WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**
1.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne (4) zifuatazo:-

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi ambayo inajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) **Sehemu ya Pili** ni Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

c) **Sehemu ya Tatu** ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na

d) **Sehemu ya Nne** ni Hitimisho.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekelezwa kwa kuzingatia masharti mbalimballi yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilifanya mambo yafuatayo:-

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1));

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Kanuni ya 117 (1));

c) Kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 MSINGI NA MAWANDA YA UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.[1]

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilichambua taarifa za utekelezaji za **Fungu 68 –** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2). Katika ulinganisho huo, Kamati ilitathmini mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi uliofanyika kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati imezingatia masuala muhimu yanayogusa sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa Wizara kuhakikisha inachangia utekelezaji bora wa Ibara ya 18 ya Katiba ambayo pamoja na masuala mengine, inaweka haki kwa kila mtu kutafuta, kupokea na kutoa Habari, kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na masuala muhimu ya kijamii.[2]

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari umehusisha taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni:-

a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

---

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023

[2] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

b) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);

c) Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL);

d) Shirika la Posta Tanzania (TPC);

e) Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN);

f) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF);

g) Tume ya Taifa ya TEHAMA (ICTC); na

h) Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC).

## 2.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.2.1 Malengo ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilijiwekea malengo ya utekelezaji wa bajeti. Malengo hayo yalijikita katika vipaumbele vifuatavyo:-

a) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, TEHAMA, Posta na Mawasiliano ya Simu;

b) Kuratibu kazi za upembuzi yakinifu kuhusu ujenzi wa maghala ya kuhifadhia bidhaa za biashara mtandao;

c) Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa Anwani za Makazi kwa kuhakiki taarifa zilizokusanywa wakati wa zoezi hilo;

d) Kuratibu kuanzishwa kwa wakala ya anga la juu nchini (Tanzania Space Agency);

e) Kusimamia upembuzi yakinifu utakaowezesha biashara mtandao (e- commerce);

f) Kusimamia kukamilisha shughuli za ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wa kilometa 2,779; na

g) Kujenga kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Zanzibar na Dodoma.

2.2.2 **Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 212,457,625,000** ili kutekeleza malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 190,794,762,991.93** sawa na **asilimia 89.8** ya bajeti iliyoidhinishiwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**KIELELEZO NA. 1 – MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA WA FUNGU 68 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| BAJETI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 30,503,685,000 | 18,626041,243.61 | 61% |
| FEDHA YA MAENDELEO | 181,953,940,000 | 172,168,721,748.32 | 94.6% |
| **JUMLA** | **212,457,625,000** | **190,794,762,991.93** | **89.8%** |

***Chanzo**: Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara ni ya kuridhisha kwani hadi kufikia Februari, 2024, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni juu ya wastani wa **asilimia 75**. Aidha, Kamati imeridhishwa na mapokezi ya Fedha za Maendeleo ambayo ni **asilimia 94.6** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati. Hali hii inaonyesha kuwa malengo yaliyowekwa yanaweza kufikiwa kama ilivyokusudiwa.

### 2.2.3 **Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kukusanya **Sh. 150,700,000,000** wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanya **Sh. 619,461,665,188.62**. Fedha hizo zilitarajiwa kutokana na vyanzo ada na tozo, mauzo ya picha za viongozi, mauzo ya masafa, huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, marejesho ya fedha za umma, vitambulisho vya waandishi wa Habari, nyaraka za zabuni, ukumbi wa mikutano na usajili wa magazeti.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikusanya **Sh. 12,874,514,308.27** sawa na **asilimia 8.5** ya lengo. Wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya jumla ya **Sh. 438,652,924,924.61** sawa na asilimia **70.81** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya makusanyo ya Wizara sio nzuri. Mfano, Wizara ilitarajiwa kwamba, mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee ungeweza kuipatia mapato ya takribani **Sh. Bilioni 150.245**. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2024 ni **Sh. Bilioni 12.812** tu sawa na **asilimia 8.5**. Kamati ilitaarifiwa kwamba, sababu za kutofikiwa malengo hayo ni uwezo mdogo *(capacity)* wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo Wizara imeshindwa kuuza na hivyo kuilazimu Serikali kuchukua hatua za kuongeza uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba, malengo ya makadirio ya makusanyo yaendane na uhalisia uliopo.

**KIELELEZO NA. 2 – MWENENDO WA MAKUSANYO YA MADUHULI YA FUNGU 68 KUFIKIA FEBRUARI, 2024**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2023/2024 | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRRUARI, 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| WIZARA | 150,700,000,000 | 12,874,514,308.27 | 8.5% |
| TCRA | 221,167,037,333.62 | 245,917,117,655.92 | 111.2% |
| TCRA - CCC | 710,000,000 | 532,500,000 | 75% |
| TTCL | 240,000,000,000.00 | 96,750,336,185.00 | 40.3% |
| TPC | 39,476,613,000.00 | 15,968,712,693.00 | 40.45% |
| UCSAF | 35,102,688,605.00 | 34,851,106,862.00 | 99.28% |
| ICTC | 5,284,725,000.00 | 4,484,895,593.12 | 84.86% |
| TBC | 46,860,319,000.00 | 31,174,091,097.12 | 66.52% |
| TSN | 30,860,282,250.00 | 8,973,692,838.45 | 29.08% |
| **JUMLA** | **770,161,665,188.62** | **451,526,967,232.88** | **58.63** |

***Chanzo**: Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, wastani wa makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara unaridhisha kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2024, makusanyo yalikuwa ni **asilimia 70.81**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hali hiyo, Kamati imebaini masuala kadhaa kuhusu mwenendo wa makusanyo ambapo baadhi ya taasisi zimefanya vizuri katika ukusanyaji na kuvuka malengo wakati taasisi zingine hazikufikia malengo.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi tano (5) chini ya fungu hilo zimefanya vizuri kwa kukusanya kati ya **asilimia 65** hadi **111.2** na Taasisi 3 zimekusanya chini ya **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika**, mfano, taasisi yenye makusanyo ya kuridhisha ni TCRA kwani hadi kufikia Februari, 2024, ilikuwa imekusanya **Sh. Bilioni 245,917** ambayo ni sawa na **asilimia 111.2** ya lengo. Kamati imebaini kwamba, ongezeko la makusanyo haya limesababishwa na kuboreshwa kwa mifumo ya ndani ya utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato ikiwemo "***TANZANITE PORTAL***" na kuboreshwa kwa zoezi la kuwajua wateja "**know your Customer** (**KYC**)" na makusanyo ya mwisho ya masafa sawa na **Sh. Milioni 118.2.**

**Mheshimiwa Spika**, taasisi nyingine zilizokusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha ni UCSAF **asilimia 99.28**, ICTC asilimia **84.86,** TCRA-CCC **asilimia 75.10,** TBC asilimia **66.52** kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 2**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazipongeza taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali kwa taasisi ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha yenye chini ya **asilimia 50**.

**Mheshimiwa Spika,** mfano hadi kufikia Februari, 2024 taasisi zilizokusanya chini ya kiwango ni Shirika la Posta, Shirika la Mawasiliano - TTCL na TSN.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, changamoto ya makusanyo hafifu inatokana na taasisi hizo kutokuwa na mifumo thabiti ya kukusanya maduhuli na kuwepo kwa malengo yasiyo na uhalisia kulingana na uwezo wa taasisi hizo kukusanya. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uwezo wa kila taasisi katika ukusanyaji wa mapato ili kuwa na malengo yanayoakisi uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Posta makusanyo yalikuwa ni **asilimia 40.45** ya lengo. Shirika lilipanga kukusanya **Sh.**

**39,476,613,000** lakini hadi kufikia Februari, 2024 lilikusanya **Sh. 15,968,712,693.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, makusanyo hayo yasiyoridhisha yamesababishwa na changamoto za kiuendeshaji, ambazo utatuzi wake ni lazima kuwepo kwa mikakati madhubuti ya kuendeleza miliki za Shirika, kuimarisha biashara za kifedha na uwakala, kubadili fedha za kigeni, biashara za huduma za kielektroniki, barua na biashara ya usafirishaji na huduma za EMS.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati imejulishwa kuwa, Serikali imeendelea kutenga fedha za mtaji wa uendeshaji kwa Shirika la Posta kuanzia Mwaka 2022/23 ilitenga **Sh. Bilioni 3.3** na Mwaka 2023/2024 **Sh. Bilioni 4** ili kuimarisha Shirika. Vilevile Serikali imeondoa mzigo wa madeni ya kodi na riba kiasi cha **Sh. Bilioni 26.8** kama malimbikizo ili kusafisha mizania ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake thabiti ya kuendelea kulisaidia Shirika ili lipate uwezo wa kujiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Mawasiliano – TTCL, lilipanga kukusanya **Sh. 240,000,000,000** katika mwaka wa fedha 2023/24. Hadi Februari, 2024 makusanyo yalikuwa ni **Sh. 96,750,336,185** sawa na **asilimia 40.3** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya sababu za kushuka kwa makusanyo ya Shirika la Mawasiliano ni madeni wanayodai taasisi za Serikali baada ya kutoa huduma. Kamati inaitaka Serikali kusimamia Shirika hili ili waweze kulipwa madeni kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na jukumu kubwa la uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika hili, ni vyema Serikali ikaliwezesha Shirika hili kujenga uwezo wa kujiendesha kibiashara na kuacha kutegemea ruzuku ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 ilipanga kukusanya kiasi cha **Sh. 30,860,282,250.** Hadi kufikia Februari 2024, ilikusanya **Sh. 8,973,692,838.45** sawa na **asilimia 29.08** ya Lengo. Kamati imebaini

kwamba makusanyo hayo hafifu yamesababishwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutolipwa madeni kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kuwa Serikali imeendelea kufuatilia madeni ya TSN kwa taasisi za Serikali zipatazo 170 kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023/2024. Kiasi cha **Sh. 2,247,695,070.96** sawa na **asilimia 23.6** ya lengo zimekusanywa kutoka kwa wadaiwa wa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba, taasisi zinalipa madeni kwa wakati na inapongeza mkakati wa TSN kuwasilisha madeni yote ya taasisi za Serikali kwa ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara ya fedha ili kuona uwezakano wa kulipwa kutoka kwenye bajeti za taasisi hizo.

### 2.2.4 **Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa, **Sh. 30,503,685,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida **Sh. 18,522,155,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 11,981,530,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 18,626,041,243.61** sawa na **asilimia 61** ya lengo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha zilizopokelewa **Sh. 13,039,240,994** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 5,586,800,249.61** kwenye matumizi mengineyo.

### 2.2.5 **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh.181,953,940,333** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Sh. 146,777,440,000** ni fedha za ndani na **Sh. 35,176,500,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo **Sh. 172,168,721,748.32** zilipokelewa sawa na **asilimia 94.6** ya lengo. Kati ya fedha hizo Sh. **83,592,170,752.49** ni fedha za ndani sawa na

**asilimia 48.55** na **Sh. 88,576,550,996.18** ni fedha za nje sawa na **asilimia 51.45**.

**KIELELEZO NA. 3 – MWENENDO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2024**

| TAASISI/MRADI | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | MAPOKEZI YA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Mradi Na. 4283**: Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano | 80,000,000,000 | 5,149,178,821.14 | 81% |
| **4234**: Anwani za Makazi na Postikodi | 24,000,000,000 | 5,848,483,958 | 24.4% |
| **4280**: Tanzania ya Kidijitali | 35,176,500,000 | 88,576,550,996 | 251% |
| **4383**: Kuimarisha Uwezo wa Taasisi | 4,500,000,000 | 2,591,443,400 | 57.6% |
| **6226**: Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA | 3,300,000,000 | 2,747,007,008 | 83.2% |
| **4279**: Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | 15,000,000,000 | 3,062,185,889 | 20.4% |
| **6567**: Habari kwa Umma | 1,500,000,000 | 711,550,000 | 47.4% |
| **6505**: Kufunga Mtambo Mpya wa Uchapaji | 10,000,000,000 | 794,117,902 | 7.9% |
| **4292**: Ujenzi wa ICT Parks | 8,477,440,000 | 2,688,203,774 | 31.7% |
| **JUMLA** | **181,953,940,000** | **172,168,721,748.32** | **94.4%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya fedha za maendeleo na inatoa

pongezi kwa Serikali kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, mwenendo wa utoaji fedha unaonyesha kuwa, fedha za nje zimetolewa kwa kiwango **asilimia 51.45**, na fedha za ndani zimetolewa kwa **asilimia 48.55**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba kuna miradi mitano (5) ilipokea fedha pungufu chini ya **asilimia 50**. Mfano, Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji **asilimia 7.9**, Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) **asilimia 20.4**, mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi **asilimia 24.4**, Ujenzi wa ICT Parks **asilimia 31.7** na Habari kwa Umma **asilimia 47.4**.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) hali ya mapokezi yasiyoridhisha ya fedha iliyotengwa, inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi na kufifisha manufaa yaliyotarajiwa kwani Wananchi hasa wa pembezoni mwa nchi (mipakani), bado wanapata changamoto ya kupata Habari, kwa sababu ya kutokuwa na usikivu wa masafa ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Aidha, kwa Mradi wa - Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji – TSN kutopokea fedha za kutosha kutasababisha malengo kutokamilika kwa wakati. Ni muhimu mradi ukakamilika kwa wakati ili kuipa fursa TSN kujiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba inatoa fedha kwa ukamilifu, kwa miradi yote ili kuchochea utekelezaji wa miradi yote kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi na vipaumbele vya Taifa.

### 2.2.6 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 – 17 Machi, 2024, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathmini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitoe taarifa za baadhi ya miradi iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati kama ifuatavyo:-

### a) Mradi Na. 4283 - Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, kwa mwaka 2023/24 ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulitengewa jumla ya **Sh. Bilioni 80**. Hadi kufikia Februari, 2024 ulikuwa umepokea **Sh. Bilioni 65** sawa na **asilimia 81** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu ujenzi wa kilometa 1,600 na vituo 32 vya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na kufanya upanuzi wa njia za mawasiliano kutoka 800Gbps kwenda 2000Gbps, vifaa vyote vimewasili nchini na utekelezaji unaendelea. Kamati ilitaarifiwa kuwa mradi huu ungekamilika mwezi Aprili, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** suala la kuunganisha taasisi 50 kwenye Mkongo wa Taifa, mkataba umesainiwa tarehe 25 Agosti,2023 kati ya TTCL na RUWASA ili kuanza ujenzi mradi unatarajiwa kukamilika Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuunganisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mradi umeanza kwa kuimarisha njia za ndani ya nchi na unatarajia kukamilika Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa miradi kama vile kasi ndogo ya mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo ni **asilimia 8.5** ya lengo. Aidha, changamoto ya kimkataba wa ushirikiano wa TTCL na TANESCO katika kujenga miundombinu ya njia ya Mkongo.

### *b) Mradi Na. 4283 – Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Shinyanga Mjini*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi kilichoishia Februari 2024, Shirika limekamilisha mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye awamu ya kwanza ambayo ni **asilimia 83,** awamu ya pili ni

**asilimia 75** na awamu ya tatu ni **asilimia 19** ya lengo. Miradi yote mitatu inatarajiwa kukamilika kwenye kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa Fedha 2023/2024 mfano, mkoa wa Shinyanga mradi umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea mikoa ya Singida - Tabora - Shinyanga na Mwanza na kuona mpango wa Serikali unaoendelea ili kukamilisha ujenzi wa kilometa 4,442 na kuongeza ukubwa wa njia za usafirishaji wa Mkongo, kutoka kipimo cha 200Gbps Kwenda 800Gbps kwenye mizunguko mikuu ya kaskazini, magharibi na kusini. Mradi huu umefikia **asilimia 95** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, awamu ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ilianza Mwaka 2009, ikiwa na uwezo wa 40Gbps kisha kuongezwa uwezo kuwa 200Gbps hadi 400Gbps katika mikoa ya Singida – Tabora – Shinyanga – Mwanza ambapo ujenzi ulianza Mwaka 2021/2022. Aidha, kwa mkoa wa Shinyanga umejikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni usimikaji wa mitambo na ujenzi wa nguzo za zege sambamba na uvutaji wa waya za mkongo.

**Mheshimiwa Spika**, katika awamu hii, uwezo wa mitambo umeongezwa kutoka 200Gbps hadi 800Gbps na tayari mitambo inafanya kazi kwa njia ya Singida – Shinyanga – Mwanza, na njia ya Shinyanga - Kahama. Aidha, ujenzi unaendelea katika maeneo mengine. Mradi huu huu umeongeza njia na kupanua wigo kama ifuatavyo:-

i) Usimikaji na makabidhiano ya mitambo ya kuongeza uwezo kituo cha Mkongo wa Mawasiliano cha Shinyanga umekamilika kwa **asilimia 100** na mitambo inafanya kazi. Ujenzi huu umegharimu **Sh.1,091,722,840.24;**

ii) Ujenzi wa njia ya Mkongo kutoka Shinyanga mpaka Kahama umekamilika kwa asilimia 100 na unafanya kazi na umegharimu kiasi cha **Sh. 594,224, 215.93;**

iii) Ujenzi wa njia ya Mkongo Kahama – Ushirombo – Bukene mpaka Tabora umetekelezwa kwa **asilimia 75** ya lengo, kwa kusimika nguzo za zege na kuvuta waya ADSS km 93,

ambayo imegharimu **Sh. 411,458, 650.41,** ambapo jumla ya gharama zilizotegwa ni **Sh. 543, 857,173.94**;

iv) Ujenzi wa njia ya Mkongo Shinyanga – Maswa – Bariadi umetekelezwa kwa **asilimia 90** ya lengo**.** Kazi iliyofanyika ni upandaji wa nguzo. Kwenye kuvuta waya wa faiba kazi bado haijafanyika. Kamati ilitaarifiwa kuwa, mradi huu unatarajiwa kukamililka mwishoni mwa Mwezi Machi, 2024; na

v) Mradi wa Tabora umetekelezwa kwa **asilimia 75** ya lengo, kwa kusimika nguzo za zege na kuvuta waya ADSS km 93, ambayo imegharimu kiasi cha **Sh. 411,458, 650.41.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kuwa, mradi huu una Changamoto zifuatazo:-

i) TANESCO kutozima umeme kwa wakati (katizo la umeme) ili kupisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hii imepelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi; na

ii) Hali ya hewa iliyopelekea mvua kubwa kunyesha na kusababisha mazingira magumu ya kufanya kazi.

**c)Mradi Na. 4279 – Ujenzi wa Makao Makuu ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Vikonje Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika**, gharama za mradi awamu ya kwanza ni jumla ya **Sh. 54,204,499,116.46.** Hadi tarehe 7 Machi, 2024 Shirika lilipokea **Sh. 8,940,293,022.44**. Mradi umefikia **asilimia 7** ya lengo**.** Hatua zifuatazo zimechukuliwa katika kutekeleza hilo:-

i) Kupata eneo la kujenga Makao makuu mita za mraba 126,300.97 na kukarabati majengo ya ofisi na studio za redio na kituo cha television Dodoma;

ii) Kuanza ujenzi wa majengo ya utawala, studio za redio, televisioni na vyombo vya kidigitali;

iii) Kulipa fidia kwa wakazi 44 wa eneo la Vikonje kwa gharama ya **Sh. Milioni 349.9**; na

iv) Kujenga ukuta wa eneo la mradi unaotekelezwa na Mkandarasi *SUMA JKT Construction CO. Ltd Dodoma.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

i) Kuchelewa kwa malipo ya awali kwa mkandarasi katika mradi; na

ii) Kutokuwepo kwa barabara ya kuingia kwenye eneo ya mradi.

### d)Mradi Na. 4279 – Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano – Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2023/24 mfuko umepata mafanikio yafuatayo:-

i) Mfuko umekamilisha mradi wa UCSAF awamu ya 4B uliohusisha ujenzi wa vituo 11 vya mawasiliano ikiwemo vituo 6 Kanda ya Ziwa inayojumuisha mbuga ya Burigi;

ii) Utekelezaji wa mradi wa UCSAF awamu ya 6 wenye vituo 43 vya mawasiliano na usimikaji wa minara umefikia **asilimia 88** ya lengo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/24;

iii) UCSAF kwa kushirikiana na TBC wameingia makubaliano ya kuboresha usikivu wa TBC radio katika maeneo ya Rombo, Usangi (Kilimanjaro) na Bukombe (Geita); na

iv) Serikali imeendelea kuboresha uwezo wa kifedha wa UCSAF kwa ajili ya kuboresha usikivu wa matangazo ya TBC katika maeneo ya mipakani ambayo ni pamoja na Kisaki – (Morogoro), Mlimba, (Morogoro), Ludewa (Njombe), Ruangwa (Lindi), Kyela (Mbeya), Ngara (Kagera), Makete (Njombe), Mlele (Katavi), Ngorongoro (Arusha), Uvinza (Kigoma) na Mbinga (Ruvuma).

**Mheshimiwa Spika,** imebaini kuna kasi ndogo ya ujenzi wa minara kutokana na sababu mbalimbali kwani hadi kufikia Februari, 2024 idadi ya minara iliyojengwa ni 81 kati ya 758 sawa na **asilimia 10.69** na minara iliyowashwa na kutoa huduma ni 18.

***e) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lako lilipopitisha bajeti ya **Fungu 68** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati isipokuwa kwa maeneo machache ambayo hayajatekelezwa kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya maoni na ushauri yaliyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha, ni Serikali kufanikisha mchakato wa kuikabidhi TTCL usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ili uweze kujiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali kupitia maamuzi ya Baraza la Mawaziri ya tarehe 22 Novemba, 2023 imekabidhi rasmi umiliki na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa TTCL.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Kamati ilishauri Serikali isaidie Shirika ili kulipwa madeni yake kutoka katika Taasisi za Serikali. Hata hivyo, Kamati ilitaarifiwa kwamba mchakato wa suala hilo unaendelea kwani Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Sh. 2,555,944,486** kati ya **Sh. 4,498,934,931** kutoka Taasisi za Serikali zilizozidai ndani ya kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.

2.2.7 **Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufanya uchambuzi wa majukumu yaliyotekelezwa na Wizara na taasisi zake ni kama ifuatavyo:-

***a) Tume ya TEHAMA – ICTC***

**Mheshimiwa Spika**, Tume hii inatekeleza mradi wa kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Sh. 3,300,000,000.** Hadi kufikia Februari, 2024 **Sh. 2,747,007,008.12** sawa na **asilimia 83** ya lengo kimepokelewa na kutumika kama ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilijulishwa kuwa, Tume inatekeleza mradi wa :-

i) Kuendeleza ubunifu wa vifaa vya TEHAMA (ICT Refurbishment and Assembly centre);

ii) Kuendelea na uanzishwaji wa vituo vya kuendeleza bunifu za TEHAMA (Soft centers) vya kikanda katika mikoa 8 ikiwemo Zanzibar mfano, ukarabati wa kituo kikuu cha kukuza bunifu za TEHAMA cha Dar es Salaam ambapo kimefikia **asilimia 40** ya lengo;

iii) Kampuni changa kumi na mbili (12) za ubunifu za TEHAMA zimewezeshwa kushiriki mkutano wa mwaka wa wabunifu uliofanyika tarehe 5 - 7 Disemba, 2023 nchini Algeria; na

iv) Tume imeendelea kubainisha maeneo ambayo vituo vitaanzishwa katika mikoa ya Arusha, Lindi, Mwanza, Tanga, Zanzibar na Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kuna kasi ndogo ya uanzishaji wa vituo vya ubunifu wa TEHAMA nchini. Jambo hili linaweza kukwamisha jitahada za kukuza fursa za ajira kwa vijana katika maendeleo ya Tehama na Uchumi nchini.

***b) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2023/24, Shirika limetengewa jumla ya **Sh. 15,000,000,000.** Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 28 Februari 2024 Shirika lilipokea **Sh. 3,062,185,889** sawa na **asilimia 20.4** ya lengo. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

i) Kuanza taratibu za ununuzi wa gari moja la kurushia matangazo ya moja kwa moja ya TBC (OB VAN);

ii) Kukamilika kwa ununuzi na ufungaji Mitambo na vifaa vya utangazaji vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kuunganisha studio 5 za Mikocheni;

iii) Kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa magari tisa (9) ya shughuli za utangazaji; na

iv) Kuendelea kufanya tathmini kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kurushia matangazo mbashara ya redio nje ya studio kwenye kanda nane (8) na upanuzi wa usikivu wa redio za TBC katika wilaya saba (7) nchini.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zinazokabili Shirika ni upokeaji wa fedha usioridhisha, na usikivu hafifu wa redio za TBC hasa maeneo ya mipakani mwa nchi.

### 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

#### 2.3.1 Muundo wa Bajeti kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 178,426,557,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. 36,406,663,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 142,019,894,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imejiwekea vipaumbele vya utekelezaji wa kibajeti vifuatavyo:-

a) Kutunga na kuhuisha miongozo inayosimamia Sekta za habari, mawasiliano na teknolojia ya habari;

b) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na posta kote nchini;

c) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandao nchini;

d) Kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali ikiwemo namba ya utambulisho wa kidigitali;

e) Kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao;

f) Kuimarisha upatikanaji wa habari nchini; na

g) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa (Startups).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mwaka wa Fedha 2024/2025. **Kielelezo Na. 4** kinabainisha tofauti ya makadirio hayo.

**KIELELEZO NA 4 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA 2024/205 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 30,503,685,000 | 36,406,663,000 | 5,902,978,000 | +19.35 |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 181,953,940,000 | 142,019,894,000 | -39,934,046,000 | -21.95 |
| **JUMLA** | **212,457,625,000** | **178,426,557,000** | **-34,031,068,000** | **-16.02** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Wizara imepungua kwa **asilimia 16.02** kutoka **Sh. Bilioni 212** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 hadi kufikia **Sh. Bilioni 178** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Fedha ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa **asilimia 19.35**, fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imepungua kwa **asilimia 21.95**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa Watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 2.3.2 Malengo ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/204, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya **Sh. 786,663,818,024.99.** Kiwango hiki ni ongezeko **la asilimia 26.99** ukilinganisha na **Sh. 619,461,665,188.62** iliyopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. **Kielelezo Na. 5** kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

**KIELELEZO NA.5 – ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MAKADIRIO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| WIZARA | 150,700,000,000.00 | 100,700,000 | -33.17% |
| TCRA | 221,167,037,333.62 | 201,736,566,472.99 | - 8.78 |
| TCRA - CCC | 710,000,000.00 | 710,000,000.00 | 0 |
| TTCL | 240,000,000,000.00 | 377,912,000,000.00 | +57.46 |
| POSTA | 39,476,613,000.00 | 43,415,885,000.00 | +9.97 |
| UCSAF | 35,102,688,605.00 | 43,614,542,504.00 | +24.24 |
| ICTC | 5,284,725,000.00 | 6,428,707,300.00 | +21.64 |
| TBC | 46,860,319,000.00 | 43,494,079,840.00 | -7.18 |
| TSN | 30,860,282,250.00 | 26,831,676,908.00 | -13.05 |
| PDPC | 00.00 | 42,520,360,000.00 | 0 |
| **JUMLA** | | | |

***Chanzo**: Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi chini ya Wizara ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa zile taasisi ambazo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 hazikutimiza malengo ya makusanyo kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa katika **Kielelezo Na. 5**. Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 2.3.3 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 19.35** ukilinganisha na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) kutoka **Sh. 30,503,685,000** hadi **Sh. 36,406,663,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 24,997,474,000** ni kwa ajili ya Mishahara (P.E.) na **Sh. 11,409,189,000** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo (O.C.).

**KIELELEZO NA. 6 - ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KATI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 18,522,155,000 | 24,997,474,000 | 6,475,319,000 | +34.96% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 11,981,530,000 | 11,409,189,000 | -572,341,000 | -4.77% |
| **JUMLA** | **30,503,685,000** | **36,406,663,000** | **5,902,978,000** | **+19.35%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 68*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) kwa kuwa ongezeko hilo litasaidia masuala ya uratibu wa shughuli zinazosimamiwa na Wizara.

### 2.3.4 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 142,019,894,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa **asilimia 21.95** ukilinganisha na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 7**. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 116,469,894,000** ni Fedha za Ndani na **Sh. 25,550,000,000** ni Fedha za Nje.

**KIELELEZO NA 7 - ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KATI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| CHANZO | BAJETI YA 2023/2024 | BAJETI YA 2024/2025 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 146,777,440,000 | 116,469,894,000 | -30,307,546,000 | -21.95 |
| **FEDHA ZA NJE** | 35,176,500,000 | 25,550,000,000 | -9,626,500,000 | -27.36 |
| **JUMLA** | **181,953,940,333** | **142,019,894,000** | **-39,934,046,333** | **-21.95** |

***Chanzo***: *Randama ya Fungu 68 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, **Sh. Bilioni 80.70** zilizotengwa kwenye fedha za ndani ni kwa ajili ya kutekeleza Mradi Na. 4283 wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ikiwa ni nyongeza ya **asilimia 0.88** ukilinganisha na **Sh. Bilioni 80** zilizotengewa kutekeleza Mradi huo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa sehemu ya dhima ya Wizara ni kuweka mazingira yanayokuza ubunifu kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa kidigitali, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati Madhubuti ili kuwezesha ujenzi wa mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uweze kufika hadi nchi za jirani na kuongeza makusanyo na pato la nchi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI

### 3.1 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo:-

a) Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 bajeti ya matumizi ya maendeleo imepungua kwa **asilimia 21.95**. Kamati inashauri kwamba, Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi na kuhakikisha fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

b) Kamati imebaini kwamba, fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zimeongeza kwa **asilimia 19.35.** Kamati inashauri kwamba, Serikali kuwa wabunifu wa namna bora ya utekelezaji wa majukumu yao ili kuhakikisha kuwa, fedha zilizotengwa zitumike kwa malengo yaliyowekwa.

### 3.2 MAONI NA USHAURI MAHUSUSI

#### *3.2.1 **Ujenzi wa Miundombinu ya Njia za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kukabidhi uendeshaji wa Mkongo kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Pamoja na pongezi hizo, suala la ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unahusisha usimikaji wa nguzo za zege na uvutaji wa waya za faiba. Kamati inashauri kwamba, Serikali kupitia upya mkataba wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaotekelezwa na TTCL na TANESCO, ili kuona namna bora ya kuondoa mapungufu yaliyopo na kukamilisha ujenzi kwa wakati na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Serikali iharakishe mchakato wa kupeleka Mkongo wa Taifawa Mawasiliano kwenye nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuongeza pato la nchi. Aidha, inaendelea kuisisitiza kwamba, TTCL waendelee kushughulikia changamoto zilizopo ili waweze kujiendesha kibiashara.

### *3.2.2* ***Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC), Vikonje, Dodoma***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya maendeleo kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa lengo la kuwezesha Shirika kujenga na kuboresha miundombinu. Pamoja na jitihada hizo, Kamati inashauri kwamba:-

a) Serikali iendelee kuongeza bajeti ya TBC na fedha itolewe kwa wakati;

b) Serikali iendelee kusimamia Wakandarasi na kuhakikisha kuwa, wanalipwa fedha kwa wakati na gharama za ujenzi ziendane na uhalisia;

c) Serikali ihakikishe kwamba, Ujenzi wa miundombinu ya barabara ya kuingia kwenye eneo la mradi inarekebishwa kwa wakati ili kuondoa usumbufu wa kufika eneo husika;

d) Serikali isimamie zoezi la ulipaji fidia kuwa, linakamilika kwa mwananchi aliyebaki kwenye eneo la mradi; na

e) Kutokana na dhana ya wajibu wa kurejesha fadhila kwa jamii (CSR), Serikali ihakikishe kwamba, kwenye mikataba ya miradi, kiwepo kipengele kitakachowabana Wakandarasi kutenga kiasi cha fedha za CSR.

### 3.2.3 Usikivu Hafifu Redio za TBC hasa Maeneo ya Mipakani mwa Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa minara ya mawasiliano nchi nzima. Pamoja na pongezi Kamati inashauri kwamba, Serikali itoe fedha za kutosha na kwa wakati kwa UCSAF ili kutekeleza azma ya ujenzi wa minara 758 nchini kote ili kupata usikivu wa mawasiliano nchi nzima.

### *3.2.4 Uimarajishaji wa Mifumo ya Teknolojia chini ya Tume ya TEHAMA – ICTC*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa mikakati ya kuanzisha vituo mbalimbali vya kuendeleza bunifu za TEHAMA nchini, pamoja na pongezi hizo, Kamati inashauri kwamba, Serikali iongeze kasi ya kutekeleza uanzishwaji wa vituo hivyo. pia kuwekwe mikakati itakayowezesha Serikali kumiliki satelite ili kuimarisha mifumo ya teknolojia, na iimarishe eneo la ulinzi na usalama wa mifumo ya TEHAMA nchini.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 MAELEZO YA HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, katika ukuaji wa uchumi wa nchi, Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ni muhimu kwani huwezesha sekta nyingine zote kufikia malengo waliyojiwekea. Uwekezaji katika sekta hizi ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo ni muhimu Serikali kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Ibara ya 61.

## 4.2 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema Bunge hili ukisaidiiwa na Naibu Spika Pamoja na Wenyeviti wa Bunge, na kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha uliofanikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. **Makamu**
3. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. Mjumbe
4. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. Mjumbe
5. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. Mjumbe
6. Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. Mjumbe
7. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. Mjumbe
8. Mhe. Angelina Malembeka, Mb. Mjumbe
9. Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. Mjumbe
10. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. Mjumbe
11. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. Mjumbe
12. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. Mjumbe
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. Mjumbe
14. Mhe. Livingstone Lusinde, Mb. Mjumbe
15. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. Mjumbe
16. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. Mjumbe
17. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. Mjumbe
18. Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. Mjumbe
19. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. Mjumbe
20. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. Mjumbe
21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb. – Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akisaidiwa na Mhe. Eng. Maryprisca Mahundi, Mb. – Naibu Waziri kwa

ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Mohammed Khamis Abdullah, na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Nicholaus Merinyo Mkapa kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara walipohitajika kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ***ndc*** kwa niaba ya Sekretarieti na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake kwa niaba ya Sekretarieti na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake.

4.3 **MSIMAMO WA KAMATI KUHUSU HOJA**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
16 Mei, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza michango. Tunaanza na wale ambao hawajachangia kabisa. Mheshimiwa Mlaghila, ajiandae Mheshimiwa Kingu. Dakika kumi kumi.

Mheshimiwa Mlaghila, *okay*, Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa shukrani zangu za dhati kwa Kiti chako kwa kunipa

heshima ya kuwa mchangiaji wa kwanza. Mimi naanza kwa kifupi sana, nitachangia maeneo kama matatu/manne na kimsingi ninakwenda kutoa ushauri kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni ukweli usiopingika kwamba, Wizara inayoongozwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, ikiwa kama sisi Bunge tutatoa ushauri wa kimkakati, inaweza kuwa chanzo cha *base* ya kui-*transform* nchi hii katika kuongeza mapato na makusanyo ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu wetu ni mwema sana. Wizara hii imepata Waziri ambaye kimsingi niseme kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Nape umekuwa ukifanya kazi na unaitendea haki sana Sekta ya *ICT* katika Taifa letu. Kwa kifupi pia, niseme juzi tumepata ripoti ambazo zimeonesha kwamba, Tanzania tumekuwa *champion* wa uhuru wa vyombo vya habari katika Nchi za Ukanda wa Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoyasema haya hata milima itatushangaa. Pongezi za dhati, kwa niaba ya Wabunge wenzangu. Pia, ninajua kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuruhusu uhuru mkubwa wa vyombo vya habari katika taifa letu, jambo hili limetuletea sifa na heshima kama Taifa. Nami niwatie moyo Mheshimiwa Nape na Naibu wako kwa sababu, jambo hili limekwenda kuleta wigo wa jamii kubwa za kimataifa kuendelea kuwa na imani na Serikali yetu hasa katika masuala ya habari. Endeleeni kuchapa kazi na kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa lengo la kuleta *transformation* katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo utafiti uliofanywa na George Ogello, huyu ni *scholar* katika masuala mazima ya *ICT* duniani. Alifanya utafiti wake mwaka 2017 anaonesha ya kwamba, asilimia 85 mpaka 90 ya vyombo vya habari vya Afrika vinategemea *government expenditure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niyaseme haya, Mheshimiwa Nape na Naibu wako mnisikilize kwa makini sana. Hapa tunapozungumza vyombo vyetu vya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, na huu ukweli ni lazima Wabunge tuambiane, michakato mingi sana inayoleta mapinduzi

makubwa katika taifa letu vyombo vya habari vina-*play part* kubwa sana ya kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupe takwimu na katika hili nitoe ushauri kwa Serikali yetu inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Je, *Government spending* katika masuala mazima ya habari katika nchi yetu ikoje? Hapa ninapozungumza vyombo vya habari vinaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 19, kwa zaidi ya miaka saba hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo lazima tuyaseme. Mheshimiwa Nape haya tunayasema kwa nia njema, lazima Serikali ije na mikakati ya kuhakikisha kwamba, kwa mujibu wa hii *research* ninayoisema, hauwezi ukaepuka *government expenditure* katika kukuza uhuru wa vyombo vya habari na kuvisaidia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo waandishi wetu wa habari wamekuwa kama ombaomba kwenye taifa hili. Sasa Serikali ninaomba nitoe ushauri wangu, Mheshimiwa Nape, kaeni na Wizara ya Fedha, vilipeni vyombo vya habari mabilioni ya fedha vinayodai, ili viweze kujiendesha tuweze kukuza ajira huko mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza shilingi bilioni 19 haziko kwenye *circulation* kwa vyombo vya Habari. Hivi tunategemea ni vipi vyombo hivi vya habari vinaweza kufanya kazi ya kufichua maovu kwenye jamii kama vinadai fedha? Hawawezi kuwalipa watumishi wao mishahara. Mheshimiwa Nape ninakuomba, kaeni na Wizara ya Fedha, kaeni na Serikali lipeni madeni yote ya vyombo vya habari vinavyoidai Serikali, ili tuweze kuhamasisha utendaji na kukuza sekta ya habari katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechukua *statistics* kwa upande wa nchi ya Kenya. Japokuwa Tanzania tumeanza kufanya vizuri, asilimia 30 ya mapato ya *newspaper* zinazotoka Kenya zinatokana na *Government spending*. Mimi leo nakuja na mawazo, Mheshimiwa Nape, wasaidie wanahabari wa Tanzania utakwenda kuandika *legacy* wewe na Serikali iliyoko madarakani

ya kuwafanya wanahabari waone ya kwamba, uongozi wako na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia mmeacha *legacy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwezekana tengeni hata *percent* ya *Government spending* iende kwenye vyombo vya habari. Hakuna namna tunaweza tukakuza uhuru wa vyombo vya habari kama tutaviacha vi-*struggle on their own* na vina uchumi haba, wafanyakazi hawalipwi mishahara. Mheshimiwa Nape, nami kuanzia leo ninabeba ajenda ya kuwasemea wanahabari na nitakuwa *champion* wao, lipeni madeni ya vyombo vya habari. Serikali yangu sikivu, ninyi mmekuwa ma-*champion*, walipeni wanahabari fedha wanazodai tuweze kuimarisha vyombo vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nakwenda kuzungumza habari ya *contribution* ya *ICT* katika *digital economy* ya nchi. *Statistics* za dunia zinaonesha nchi ya Kenya *ICT* ina-*contribute* asilimia 9.2 ya *GDP* ya Kenya. Ukienda Uganda wana-*contribute* asilimia 9.8. Mheshimiwa Nape nataka nikupe ushauri, kwa nini Tanzania tumeendelea kucheza kwenye asilimia moja mpaka mbili ya *contribution* ya *ICT* katika uchumi wa nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ni moja, ninajua kazi kubwa sana inafanywa na *e-GA* na binafsi ninamjua Mkurugenzi wa *e-GA*, ni kijana mzalendo, mchapakazi sana na muadilifu, lakini nataka nikushauri Mheshimiwa Nape, pamekuwa na *cumbersome procedure*, jambo ambalo kimsingi ninyi Serikali hampaswi kulifanya. Waambie e-GA waache kufanya kazi ya kuendeleza na kukuza vipaji vya kukuza mifumo kwenye nchi, hiyo siyo kazi yao. Acheni kazi hii ifanywe na *private sector*. Hamwezi kukuza uchumi wa nchi kwa kujifungia ndani, *e-GA* wanakaa wanatengeneza mifumo, Mheshimiwa Nape hicho kitu duniani haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi juzi tumepata *exposure* kwa kutumia kodi za Watanzania, tumekwenda pale Marekani. Ukiangalia namna chumi za dunia zinakua, taasisi za Serikali zipo, ni kazi ya kufanya *monitoring* na ku-*evaluate* kampuni zinazotengeneza mifumo. Hizi *cumbersome procedures* za kutaka

ninyi Serikali ndiyo mtengeneze mifumo, ndiyo maana inasababisha *ICT* imeshindwa kuwa na *contribution* kubwa ya kujenga *GDP* ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 nilitoa mfano hapa kwenye hili Bunge nikasema kuna vijana wa Kitanzania wametengeneza mfumo wa hospitali. Wamepandisha mapato Hospitali ya Bugando kutoka shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni tatu, wamepandisha mapato *KCMC Hospital* kutoka shilingi milioni 400 mpaka shilingi bilioni 3.7, wamepandisha mapato Hospitali ya Amana kutoka shilingi milioni mbili kwa siku mpaka shilingi milioni 20 na wamepandisha mapato hapa Dodoma *General Hospital*, vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko tunakozungumza Mheshimiwa Nape ndiko ajira zinakotengenezwa na ndiko uchumi na *tax base* ya nchi inakopanuka. Ahsante kwa kuhamisha *e-GA* kutoka kule ilikokuwa na kuja kwako. Kama Bunge tushauri *e-GA* waache kazi ya kutengeneza mifumo, siyo kazi yao. Wafanye kazi ya ku-*monitor* na ku-*approve* mifumo na wana vijana wazuri. Tuweze kukuza hili Taifa liweze kupata uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kitu kingine, tunazungumza habari ya nchi haina *tax base* ya kutosha. Leo Tanzania walipakodi nchi nzima tunaambiwa tunabebwa na watu milioni tatu, *what a shame* kwenye nchi yetu? Watu wenye uwezo wa kulipa kodi wako zaidi ya milioni 15, wanaolipa kodi ni watu milioni tatu. Ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa naibu spika, Mheshimiwa Nape nataka nikwambie leo, wewe ukiamua kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara yako inaweza ika-*transform* Taifa hili. Tusitegemee 10 hata moja ya *donor*, walipa kodi wakapatikana kwenye nchi yetu. Ni namna gani tunaweza tukafanya? Ni kwa kutumia mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mmemsikia Mheshimiwa Jerry Silaa, kaka yangu mchapakazi ninampongeza, analalamika watu hawajalipa kodi ya pango ya nyumba. Hivi kama Tanzania tunaweza tukajua idadi ya tembo walioko, tunashindwaje

kutengeneza mifumo ya kujua watu wanaotakiwa kulipa *land rent*? Tunakosa kodi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Nape, kwa kutumia *ICT,* tumekwenda Marekani. Hapa Watanzania tunalalamika sana na hiki kitu ni lazima kikome, watu hawalipi kodi. Ukienda Marekani mama ntilie anayeuza *burger* analipa kodi, leo nikiuliza hapa ni Waheshimiwa Wabunge wangapi mnakwenda kwenye *canteen* ya Bunge, mnalipa pesa mnalipia chakula; kuna Mbunge hata mmoja anaomba risiti ambayo kodi inakwenda kwenye Serikali? Kuna Mbunge hata mmoja anachukua risiti pale *canteen*? *People are not paying tax*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia pekee ya kulisaidia hili Taifa ni kukaa na Wizara ya Fedha, na kuacha kuruhusu *cash transaction* kwenye hii nchi. Mheshimiwa Nape tumia Wizara yako, hakikisha kila *transaction* inayofanyika kwenye nchi ifanywe... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, ahsante. Pamoja na mchango mzuri, muda wako umekwisha.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika kumi zimeisha!

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo. *Rules are rules*. Mpira ukiisha kama umefungwa, ndiyo mpira umekwisha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape, mchango huu ni muhimu sana na siku zote tunasema kuna nchi jirani inachangia kwenye *GDP* ya nchi yao *12 trillion shillings* za Tanzania kwenye simu tu hizi. Nendeni mkajifunze. Tunapigwa kweli kweli kwenye mapato ya *telecom* nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mlaghila, utachangia au basi umeamua... *(Makofi)*

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia.

**NAIBU SPIKA:** Haya.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais ambaye ametuletea Mawaziri bora kabisa wa viwango, ambao kwenye Wizara hii wanaongozwa na Mheshimiwa Nape Moses Nauye, akisaidiwa na Mhandisi Marryprisca Mahundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa pongezi hizi siyo kwamba labda wana sura nzuri, hapana. Tunatoa pongezi hizi kwa kazi nzuri wanazofanya na kuitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tulipokuwa tunaingia hapa tumeona roboti iko pale nje. Haya ni matunda ya hawa watu wakisaidiwa na ndugu zetu wa *ICT* ambao wana-*aim* katika kuhakikisha ubunifu wa vijana wetu na kujenga vituo vya ubunifu, ambavyo sasa vinatamalaki nchini. Mmoja wa wanufaika ni mimi kwa sababu, kituo kimojawapo kinaenda kujengwa Kyerwa. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TEHAMA hii ndiyo nyenzo ya kuhakikisha Taifa lolote kwa sasa hivi linasonga mbele. Leo ni lazima tuhakikishe pesa inaenda katika eneo hili kwa sababu, sasa hivi ni sekta mtambuka, sasa Serikali ifanye hima izipeleke kama ambavyo imekuwa ikifanya tangu mwaka 2023 na mwaka 2024, tunaomba ifanye hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote, tunaweza tukazungumza mengi sana, lakini kuna watu ambao wanaendelea kutukwamisha, ambapo ninaitaka Wizara, Mheshimiwa Nape, iwe makini nao. Hawa ni n*etwork providers* wetu; Vodacom, Tigo, akiwemo hata *TTCL pia.* Mheshimiwa Waziri hawa watu wanatupiga. Labda inawezekana ikawa ni kwangu

tu, lakini sidhani katika kitendo kibaya kilichopo kwa sasa hivi ni kwamba *quality* ya mawasiliano nchini kote iko chini na haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapopiga simu, hata unapozungumza masuala ya kibiashara, unaweza ukakuta katikati ya mazungumzo simu inakata, mwenzio hakusikii au wewe humsikii, kumbe kule anaongea peke yake na wewe unaongea peke yako. Jambo hili katika karne hii halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kutokusikika tu, utakuta unazungumza kunatokea sauti ya ajabu katikati, unaweza ukatupa simu. Tunaomba tupate majibu, ni nini kinachofanya hivyo kama siyo kutokututendea haki na kutuonea kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye *quality* ya usikivu na *quality* ya *data* sasa tufanye hima tuongeze na tuwaambie *providers,* tuwape viwango. Hata unapotembea, unajua ni ajabu sana, yaani ukikuta kamlima kidogo tu ukishuka tayari mawasiliano yamekatika. Sasa hili haliwezi likatufikisha kule tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii alikuwa anazungumza Mheshimiwa Kingu, tunataka nchi hii ipate mapato, ninataka nikwambie Mheshimiwa Waziri, hatima hii iko mikononi mwako, kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuki-*register* na tukaondoa *cash money* kwenye mzunguko, tunaenda kuongeza mapato. Kila mlipakodi na kila hela inayotakiwa kwenda Serikalini, itaonekana na itakatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza hapa, tunaenda tunamwambia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wakulima wetu wananyanyaswa, lakini tungewa-*register* kwa *coordinates* zao za sehemu wanazolima, hakuna ambaye angesumbua. Kila kitu kingeenda sawa. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba sasa ni wakati sahihi wa kuchukua hatua kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa. Usikasirike, ndiyo kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kingu hapa.

**NAIBU SPIKA:** Enhe.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa mchangiaji, kaka yangu ninayemheshimu sana na mchango wake ni mzuri, kwamba hii anayoizungumza unapanda mlima *network* inakata; sasa hivi hata hizi takwimu za kutuambia kwamba duniani tuna *line* milioni 72 kwa sababu, wanaweza wakatumia mtandao mmoja wa Vodacom waka-*rom* mitandao mingine, nchi ikawa na *accessibility* ya *network* nchi nzima hazina faida sana kwenye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa kwamba, hizi teknolojia zipo na tayari *East Africa* kuna mkataba umesainiwa na *SADC*. Mkataba umesainiwa, nini shida? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa hiyo kwa mikono miwili. Ni kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaimarisha Wizara hii, ninaiomba Serikali ilipe madeni yake. Kuna mifano mingine hata tukiitoa wakati mwingine haileti maana sana. Hivi leo, kwa mfano *TSN* pesa zao hawajalipwa hata za kwenye sensa walizotengeneza makaratasi ya sensa na vifaa vya sensa. Tunaiomba Serikali ilipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani leo tukaendelea kusema sekta hii inakua wakati Serikali hailipi madeni yake. Tunaomba sana, tunajua kuna mambo mengi ambayo Serikali inatekeleza, lakini tunaomba eneo hili pia likumbukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni lazima tumpongeze Mkurugenzi wa *TCRA*. Ndugu zangu, katika sehemu ambayo imetufanya Watanzania kupunguza vilio kibiashara, ni uwezo mkubwa walionao *TCRA*. Kuna wakati wamezuia mpaka wizi kwenye benki zetu. Kuna nchi zimepigwa hapa lakini kwa kazi inayofanya na *TCRA*, kwa kweli wameweza kutusaidia na kutufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ulinzi wa nchi yetu kijamii pia, unawategemea sana *TCRA*. Wizi wa kwenye mitandao sasa hivi umepungua, kwa kweli tunashukuru na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wa Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari ambao ni Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi na Wataalamu kutoka Sekta Binafsi, Chama cha Wakongwe wa Redio Tanzania Dar es Salaam, watumishi kutoka *Wasafi Media*, watumishi wa *TBC,* Chama cha Watoa Huduma za Mawasiliano, watumishi kutoka *Clouds Media* na Wasanii wa Cheka Tu. Mnaweza mkasimama kwa ujumla. Ahsanteni sana na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Bulaya halafu Mheshimiwa Amandus ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara yangu pendwa ya Habari nikiwa kama mwanahabari. Kwanza kwa kuanzia Mheshimiwa Nape, jana wakati unatoa namba ya watu kupiga wale waliotapeliwa, watu tumetuma meseji, majibu inayokupa kwamba hiyo namba haijahusika na utapeli.

Kwa hiyo, kuna kitu cha ziada cha kufanya kwa sababu sisi wahanga, tumewatumia namba, tumeshatapeliwa, wametoa hayo majibu, nadhani kuna shida bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanahabari wamenituma nikumbushie kwenye Sheria ile ya Habari, yalipita mapendekezo yao tisa, wanashukuru, lakini bado mengine yamekwama na wewe wanakuona mhanga mwenzao kwenye haya mambo. Wanasema mbali na kuwa na imani na wewe, endelea kuyatekeleza yale mambo waliyokuomba kwenye Sheria ya Vyombo vya Habari kwa sababu bado kuna mambo yao hayaendi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la madeni na nilizungumzie kwa uzito wake na athari zake. Mimi nimeanza kazi ya uandishi kama Mwandishi wa Habari mwanafunzi mpaka mwandamizi na kuingia Bungeni. Najua changamoto wanazopata vyombo vya habari na ninajua changamoto wanazozipata Waandishi wa Habari. Mheshimiwa Nape, vyombo hivi vya habari vinajiendesha na vinategemea matangazo kutoka Serikalini. Hivi vitu vingine ni vya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapolipwa, ndiyo wataweza kulipa mishahara, wataweza kujiendesha na kufanya mambo mengine. Leo wana madeni sugu zaidi ya shilingi bilioni 18 na hapo kuna vyombo vingine havijaorodheshwa. Hiyo shilingi bilioni 18, chombo changu cha zamani Uhuru na Mzalendo hapa hakijawekwa na wamenitumia niwatetee, wenyewe wanadai zaidi ya shilingi milioni 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hiyo shilingi bilioni 18, shilingi bilioni 11 ni *TSN*. Watalipaje mishahara? Watajiendeshaje? Sisi tulivyo (Waandishi wa Habari), kazi yetu ni kufanya kazi tu, kimya, hakuna anayetutetea. Mpaka ifike leo humu ndani tuzungumze, siyo sawa, siyo sawa. Haya, ukienda vyombo vingine binafsi, shilingi bilioni saba ziko nje, hawa watu watafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kulipa wiki iliyopita, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu yuko hapa, aliahidi kulipa. Tunaomba hao watu walipwe. Hivi mmeshawahi kuona wahasibu wanalalamika? Mmeshawahi kuona wahasibu wanakopwa? Mmeshawahi kuona taaluma nyingine zinakopwa? Kuna taswira hapa inajengeka *like* wanahabari ni kama watu

wamefeli tu sehemu fulani, wamekuja kutafuta ajira. *No!* Kuna madaktari humu, kuna watu wana *masters*, kuna watu wana digrii. Ni kwamba wamechagua kufanya hii kazi, wasiwe wanasheria, wasiwe madaktari, wasiwe manesi. tunaomba waheshimiwe wapewe stahiki zao kama zilivyo taaluma nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani leo sisi wanahabari tuitwe ombaomba! Sisi! Mnadhania tunapenda! Mnadhania tunapenda! Mnadhania vyombo vya habari hawapendi kulipa watumishi wao? Hela mnazo nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa nini kwenye Bajeti Kuu Mheshimiwa Nape na hili napendekeza, kwenye Bajeti Kuu ya Serikali, walau msitenge *at least* hata 0.3%. Mosi, mtalipa lile deni ni dogo tu, lakini kutakuwa kuna uhakika wa kulipa kwa wakati na kwa soko vyombo vya habari. Nilikuwa natolea mfano tu bajeti ya mwaka 2023 shilingi bilioni 44.39, ukitenga 0.3% ni shilingi milioni 133, mtasaidia uchumi wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari vitaweza kuajiri, na vitaweza kulipa. Leo, 80% ya wanahabari hawana mikataba lakini hawawezi kukaa nyumbani, wana familia, hili tunaomba lifanyiwe kazi. Hata hao wenye mikataba hawalipwi. Leo hii sijui Waandishi wa Habari kikokotoo kitawakokotoa zaidi! Maana hata michango yao haipelekwi. Vyombo vya Habari, uchumi umeyumba. Habari Leo imeacha kufanya kazi na ilikuwa inawadai zaidi ya shilingi milioni 500. Zile familia leo hii ziko wapi? Si zinapata taabu? Hilo naomba lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna baadhi ya vyombo vya habari vinatishwa. Uhuru upo *yes*, lakini siyo kwa kiwango hicho. Tunaomba hilo nalo lifanyiwe kazi, waweze kufanya kazi kwa uhuru. Uhuru wa wingi wa habari lakini na kufanya kazi kwa habari pamoja na watoa taarifa, wanawanyima wanahabari taarifa. Huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, hilo nalo Mheshimiwa Nape naomba ulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna kitu kinanisumbua. Hivi leo unasafiri kutoka Dar es Salaam unaenda Morogoro, unafika

njiani eti *network* ya *Voda* inakata, lakini eneo hilo kuna Tigo, kuna *Airtel*. Sasa, si hizi kampuni zinaweza kukatana, mtu ukaweza ku-*access* hata mtandao, mtu wa *Voda* kwenye eneo la Tigo akapata *network*, kwenye eneo la *Airtel* akapata *network*! Haya ni mambo ya kizamani. Nchi nyingine wanafanya hivyo. Muda wote mtu anatakiwa apate mawasiliano, haijalishi kuna mnara wa Tigo sijui kuna wa *Airtel*. Kampuni zenyewe ndizo zinakatana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kweli kutumia *network* ya *Airtel* bila kufuata utaratibu kwa sababu utakuwa umeingilia *territory* nyingine, lakini kuna taratibu, hizo kampuni zenyewe ma-*giant* zikakaa, zikaongea, kukawa kuna mtandao muda wote. Hii itaondoa kuwarundikia Watanzania *line* nyingi na itaondoa pia urasimu kwenye mawasiliano. Haya mambo jamani yamepitwa na wakati. Ndiyo maana ya teknolojia ya mawasiliano. Twende na dunia, Tanzania siyo kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** …*my brother* unafanya kazi nzuri, tutetee sasa wanahabari, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunakwenda sasa na Mheshimiwa Amandus Chinguile, ajiandae Mheshimiwa Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuungana na wenzangu kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kufanya mapinduzi makubwa kwenye eneo hili la Mawasiliano na Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa na tumeshuhudia minara 758, haijawahi kutokea. Kubwa zaidi ni kwenda sasa

kwenye maono ya Mheshimiwa Rais kwenda kupata *satellite* ya kwetu kama Taifa. Hili ni jambo kubwa na litatuwezesha kuimarisha, pamoja na mambo mengine suala la usalama pia linakwenda kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, Kaka yangu Nape Moses Nnauye, amefanya kazi kubwa. Kwenye Sekta hii ya Mawasiliano na Habari, bila mashaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu wataungana nami kwamba Mheshimiwa Waziri amekuwa akifanya kazi kubwa na nzuri kwa kushirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalamu wengine. Tumeona hata vurugu za kwenye mitandao, zimekuwa zikipungua siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata wale matapeli nao wanaendelea kupungua, japo tunajua kwamba wapo lakini kwa namna ambavyo Wizara imejipanga na inaendelea kushughulika, ni wazi kwamba na wenyewe siku zao za kuishi huko kwenye mitandao zinahesabika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwenye maeneo mawili na hasa nitajikita kwenye Jimbo langu la Nachingwea. Pamoja na kusifia kwa kazi nzuri ambayo inafanyika na Wizara, naiomba sana Wizara kuboresha mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo kwenye Jimbo langu la Nachingwea kwenye Kata ya Mbondo, kwenye Kata ya Kilimarondo, Matekwe, Mtua, Kipara Mtua, Kiegei pamoja na Nditi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo haya ukienda maana yake uwe umeshaaga kabisa nyumbani kwamba nitakaa baada ya siku mbili nitarudi tena au nitapatikana. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba tumepata kwenye bajeti hii iliyopita minara miwili kwenye eneo la Nang'ondo na Mchonda, bado tunaomba kwenye maeneo haya ambayo nimeyaainisha tuweze kupata mawasiliano ili watu wetu pia waweze kwenda na teknolojia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, tunayo redio yetu ya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea pale. Tayari tulishaandika andiko la kuomba vifaa vya kisasa kwa ajili ya

kuimarisha usikivu kwa wenzetu wa *USAF*. Nitumie nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuona namna ambavyo wenzetu wa *USAF* watatusaidia kupata vifaa vya kisasa ili kwenda kuimarisha usikivu wa redio yetu hii ya Nachingwea ambayo kimsingi inaendelea kuwahabarisha watu wa Nachingwea na maeneo mengine juu ya habari na mambo yanayoendelea huku duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana ikikupendeza, tupange ziara ya kwenda Nachigwea, kwenda kufanya ziara kwenye baadhi ya maeneo ili ukaone haya ninayoyasema mwenyewe. Najua unafahamu maeneo hayo, lakini ukienda sasa hii itakusaidia pia kuelewa ni maeneo gani ambayo sisi kama wananchi wa Jimbo la Nachingwea utatusaidia kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naendelea kuunga mkono bajeti hii na Waheshimiwa Wabunge wenzangu naendelea kuwaomba, tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri kwa kazi hii ambayo anaifanya na yeye kwa kweli ni msikivu. Ameendelea kufanya kazi kubwa na ni msikivu, hata ukimpigia simu huwa anapokea na anakupa maelekezo na mnajadiliana mambo. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sichalwe, jiandae Mheshimiwa Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Erick James Shigongo.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mchango wangu upo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda *(Fourth Industrial Revolution)*, *Blockchain Technology, Digital Currencies, Crypto Currencies*. Mheshimiwa Waziri, huko nyuma mara kadhaa katika michango yote, hii ndiyo Wizara peke yake ambayo nimekuwa nikichangia kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nimeendelea kupata wadau wengine ambao wameendelea kuniunga kwamba Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Kingu, hii ni Wizara peke yake ambayo Mheshimiwa Waziri ukiamua kuendana na namna teknolojia inavyoenda duniani, una uwezo

wa kuajiri vijana wengi wa Kitanzania zaidi ya zile ajira ambazo zinaonekana kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusema mchango wangu, namwomba Mheshimiwa Waziri, anaweza akasahau; nina mambo kadhaa. Kwanza, natoa pongezi kwa Kampuni ya Mtandao wa *Vodacom*. Tulipopata changamoto ya mawasiliano, wameturudishia *some GBs* za kutufidia pale ambapo mtandao ulikuwa haufanyi kazi, lakini kwa uungwana wao huo huo, kwa sababu wameturudishia vifurushi kwenye upande wa *internet*, tunaomba pia waturudishie na vifurushi kwenye upande wa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vifurushi tulivyokuwa tumejiunga labda vya kupiga nje ya nchi, siku ile mtandao ulivyopata shida, hatukuweza kupiga. Kwa hiyo, waturejeshee kwa sababu walichukua pesa zetu, kwa uungwana ambao wameufanya kwa kitendo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwombe Mheshimiwa Waziri, jimboni kwangu na nimeshaomba huko nyuma, minara ya mawasiliano kwenye Kijiji cha Naming'ongo na vijiji vingine vinavyozunguka Kata ya Chitete, kwenye Kijiji cha Ntungwa na maeneo mengine ambayo yanazunguka Kata ya Mkomba, Kata nzima ya Kapela na Kata nzima ya Nzoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudi kwenye teknolojia. Nikiwa naingia hapo ndani, nimekutana na yule roboti yako, hujatuambia umempa jina gani? Mwaka 2023 nilichangia kuhusiana na roboti Sofia. Mheshimiwa Waziri, wakati nawahoji wale vijana, wakaonekana hawajui Kiswahili, wakajitambulisha ni vijana wa ki-*South Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wataungana nami ambao wanatembea huko duniani, waliponipa nafasi ya kuhoji maswali kidogo ile roboti yako, yaani wanakwambia mwulize, halafu wao wana-*google* huku pembeni halafu ndiyo unamwuliza yule roboti. Mheshimiwa Waziri nakuomba tu kwa moyo wa dhati na mapenzi makubwa ya nchi yangu, wako vijana wazuri sana wa Kitanzania hapa. Katika hili

naomba kukushauri, sisi vijana wa Kitanzania wenye *profession* ya teknolojia, tunaomba kwenye Wizara yako tutengee siku moja tu kwa mwezi, tupe hiyo siku, tuwe tunakutana kwa ajili ya kushauriana tu kwenye mambo ya teknolojia. Mheshimiwa Waziri, utakutana na vijana wazuri sana ambao watashirikiana na *e-GA* kwenye kufanya kazi. *programming* kama ile ungeweza kupata vijana wazuri, *programmers* ambao wanazijua lugha zote za ki-*programming*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanao uwezo kumkodi yule roboti akaongea lugha zote ya Kiswahili, Kifaransa na lugha zote. Siyo wale wamekaa pembeni ukiwauliza wana-*google* halafu ndiyo wanakutumia, hapana. Pale kwa kweli kwa sisi watu wa teknolojia, umetuangusha Mheshimiwa Waziri. Nimemwona pale nikasema aah, ngoja tuishie hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo waliotangulia kusema wamesema, kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda, kwenye *blockchain technology*, mwaka 2021 Mheshimiwa Rais wetu alitoka hadharani na kutoa kauli zake nzuri sana ambazo zilitoa faraja kubwa sana kwa Watanzania kuhusiana na mambo ya *digital currencies*.

Mheshimiwa Naibu Spiuka, naamini, kauli hizi za Mheshimiwa Rais ambazo zilikuwa zinaamsha ari na kasi kwa vijana wa Kitanzania ilikuwa ni lengo tu wewe kututengenezea mifumo, namna gani ambavyo tuweze kubadilisha teknolojia na tutengeneze pesa. Nakuomba katika hii Mheshimiwa Waziri, akae na Ofisi ya *CAG* amwombe amsaidie kufanya uchunguzi kwenye mitandao, ni pesa ngapi za Kitanzania ambazo zinapotea, *transactions* zinazoingia na kutoka kuhusiana na mambo ya *crypto currencies*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hela nyingi sana zinapotea na sisi kama Taifa tunapoteza. Mimi ninaamini Mheshimiwa Waziri, ukishajua kwamba kule kuna pesa, ukishajua kwamba kule tunatengeneza hela, tumeacha mianya pesa inapotea, ninaamini utatutengenezea mfumo mzuri sana hapa Tanzania ambao vijana wa Kitanzania watatumia teknolojia. Teknolojia

inaendelea kukua ili tuendelee kujitengenezea kiwango kikubwa cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hizi za Mheshimiwa Rais, kwa mfano Rais wa Kenya, kuna kauli yake ambayo ameitoa tarehe 05 ya Mwezi wa Tatu. Mheshimiwa Waziri, nakupa miezi sita tu, kauli hii ya Mheshimiwa Ruto, nakwambia utaona namna ambavyo itapandisha *GDP* ya mapato yao kwenye ulimwengu wa teknolojia. Sisi tunatamani, kauli zetu ambazo Mheshimiwa Rais akizitoa, uweze kuzifanyia kazi, ukae na vijana, uwape nafasi waoneshe uwezo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii ya Mheshimiwa Ruto aliyokuwa ameisema kwa ajili ya kuendelea kuwatia ari watu wake kwenye nchi yake na kuziambia Wizara zake za Kisekta juu ya kauli hii, mimi naamini italeta mapinduzi makubwa sana ya teknolojia na hata vijana wa Kitanzania, kauli hii imewavutia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kum-*quote* Mheshimiwa Ruto, anasema hivi; "*Likewise, marathon digital has been ushered to consult with the National Treasury in Kenya on our Crypto Currencies Regime and to the Ministry of Energy to discuss its energy needs in connection with the crypto currency mining here in Kenya. This is the strong testament on the vast transformative possibilities that exist in an expanded and comprehensive strategic understanding between US and East Africa concerning trade and investment because Kenya, we meant business.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii ya Mheshimiwa Ruto aliisema wakati walipokuwa wamefanya kikao cha *Business Summit* na *American Embassy*, *American Chamber of Commerce* tarehe 03 ya mwezi wa Tano. Kwa nini kauli hii ya Mheshimiwa Ruto ilikuja? Mheshimiwa Ruto naamini kabisa anajua namna ambavyo *block chain* inafanya kazi huko duniani; *digital currencies*, *mining* ambavyo nchi nyingine zinafanya *digital currencies in mining*. Sisi tumechelewa wapi? Tunashindwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nachoamini Mheshimiwa Waziri hamjataka tu kufungua mianya, hamjataka kuamua kuruhusu vijana wa Kitanzania wawape uzoefu wao, mmejifungia.

Tunakuomba siku moja kama ambavyo *Senator* huyu Karungo wa Kenya aliliambia Bunge lake wiki mbili zilizopita kwamba anaiomba nchi yake itume *delegation* Salvador.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasi tunakuomba utume *delegation* Salvador ili mwende mkajifunze. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante. Mengine mwandikie. Tunaendelea na Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ulenge. *(Makofi)*

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Wizara yetu ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kukubali na kuleta sheria ambayo leo sheria hiyo inaenda kuweka uhuru wa vyombo vya habari nchini. Tumewasikia wanaharakati, tumewasikia Waandishi wa Habari wakieleza bayana kwamba sheria ile inakwenda kuwafanya wawe na uwanja huru wa kufanya kazi zao. Kwa hiyo, kwenye hili Mheshimiwa Rais ameonekana ni mwanamapinduzi wa kweli katika uhuru wa kujieleza na kumpa nafasi Mtanzania kupata habari kupitia vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari ambaye yeye ndiye mwenye *instrument* ya kazi hii ya Habari na Mawasiliano ambayo ameifanya vizuri sana. Kwa hiyo, Bunge na Kamati tumeona kazi nzuri inayofanyika kupitia wataalam wake wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia pia usikivu umeongezeka katika redio yetu au shirika letu la habari ambalo ni *TBC*. Maeneo mengi yalikuwa na changamoto lakini sasa

tumeona namna ambavyo usikivu umeongezeka. Bado kuna maeneo hayajakaa sawa, lakini kwa miradi ambayo inaendelea tunaamini *TBC* itaendelea kuwa ni kivutio kwa Watanzania wengi hasa wale ambao wako mipakani. Kwa hiyo, naamini kwa juhudi ambazo zinaendelea zitasaidia sana kuongeza usikivu ambao taarifa nyingi za uhakika zinatokana na *TBC*, kwa hiyo, ninaamini sana kazi hiyo ni nzuri na inafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi mafanikio tumeyaona pia kwenye ujenzi wa minara. Minara 758, tunaona kazi inafanyika sehemu nyingi lakini kwenye hilo hata mimi kama katika Jimbo langu la Singida Mashariki pale Lighwa tayari mnara umekamilika na hivi karibuni unaanza kufanya kazi, na hii itaondoa tatizo kubwa la mawasiliano. Hata hivyo, bado nasubiri minara katika eneo la Matare pamoja na Mang'onyi ambako bado mnara umeanza kufanya kazi kwa maana tumeanza kufanyia kazi na wakandarasi wapo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa niende kwenye eneo la mchango wangu. Mchango wangu ninataka niipongeze sana *e-GA* wanafanya kazi nzuri na Mheshimiwa Waziri eneo hili wewe utakuwa ni *champion* mkubwa wa kuongeza mapato ya Serikali. Ninaamini wewe kama Wizara ni *facilitator* wa Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunaongelea mapato ya Serikali yameshuka hata *CAG* amesema kuna baadhi ya maeneo mapato hayaonekani kwa sababu kuna baadhi ya maeneo hakuna mtandao wa kutosha. Kwenye juhudi ambayo unaifanya ya ule mradi wa Tanzania Kidigitali tukimaliza ninaamini kwamba tutafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili naomba sana tuendelee kuongeza sana nguvu katika mradi ule ili tuhakikishe kwamba kila mahali, kila Wilaya mambo yaweze kwenda vizuri kwa sababu tukiweza kuwa na uhakika wa mifumo, tunaweza kukusanya kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, kazi nzuri imefanyika ya kurudisha mkongo wa

*TTCL* lakini kuna baadhi ya wilaya bado Mkongo wa Taifa haujafika. Naomba nguvu iongezeke ili kuhakikisha Mkongo wa Taifa utakapofika kila mahali utaongeza uwezo wa sisi kuweza kuhudumia katika mifumo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka nishauri katika eneo hilo, kwanza kuhakikisha wanaongeza nguvu kupeleka mkongo katika nchi za jirani kwani ni biashara kubwa sana duniani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tuendelee kuongeza nguvu, umeshaenda pale Burundi umesaini mkataba. Naamini kazi inaendelea. Pia naomba sana kwa *DRC* Congo nako tuongeze nguvu tuweze kupata soko lile ambalo kimsingi litaenda kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Tanzania ya Kidigitali litaenda kupunguza pia tatizo la upungufu wa walimu hasa wa sayansi. Tukiweza kuweka zile *centers* za kufundishia walimu katika Halmashauri zetu tutapunguza tatizo la walimu ambao leo tunalalamika. Naomba sana eneo hili tuongeze nguvu na tuweze kuongeza *facilitation* katika Halmashauri zetu kusaidia eneo la elimu ili waweze kufundishwa kupitia *e-digital.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba sana kwenye maeneo ya miradi inayopelekwa ya minara, kumekuwa na changamoto ya miundombinu ya barabara pamoja na miundombinu ya umeme. Eneo hili linakwamisha sana juhudi za Serikali katika kuongeza nguvu katika kuhakikisha kwamba miradi inajengwa kwa wakati, lakini kama sivyo kuhudumia nayo imekuwa ni changamoto kwa wataalam wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, tunapoanza mradi wa kupeleka mnara sehemu, tuhakikishe barabara imejengwa, tuhakikishe na umeme umefika ili kupunguza gharama ya kuhudumia minara ile na mwisho wa siku tupunguze gharama ya uendeshaji wa mitandao ya simu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka nieleze hayo mambo machache katika mchango wangu. Vinginevyo Mheshimiwa Waziri Nape pamoja na Naibu Waziri tunawategemea sana katika eneo hili, kazi mnafanya nzuri na

naamini kabisa katika muda wa mwaka mmoja ujao tutaweza kubadilisha kabisa sekta ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Eric Shigongo, jiandae Mheshimiwa Ulenge.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana huu ya kutoa mawazo yangu kwa ajili ya ujenzi wa Taifa langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mungu na pia kukushukuru wewe mwenyewe na Wabunge wenzangu kwa namna ambavyo tumekuwa tukifanya kazi ya kutoa michango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba wakati fulani nikiwa kwenye Mkutano wa hadhara kijijini kwangu nilimpigia simu akawaahidi wananchi wa Kijiji cha Mwangika – Bangwe – Iligamba na maeneo ya Visiwa vya Sosswa kuhusu mnara, bado mawasiliano ni matatizo Mheshimiwa Waziri naomba uwakumbuke watu hawa na ninavyoongea hivi sasa najua wananisikiliza, kwa hiyo, timiza ahadi yako ili pia uweze kutunza heshima yako katika Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kusoma utafiti ufuatao, nitasoma kwa lugha ya Kiingereza kama ilivyoandikwa baadaye nitafafanua kidogo. Wameandika hivi: "*Steve Jobs who created the iPhone and iPad wouldn't let his kids use either of these devices until his death in* 2012." *Steve Jobs* aliyetengeneza *iPhone* na *iPad* hakuruhusu watoto wake wazitumie mpaka alipokufa. Hiyo ni ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili inasema, *in recent year's Bill Gates was interviewed by the Mirror* gazeti la Uingereza na akasema, *he does not allow his own children to use cellphone until the age of fourteen*. *Bill Gates* ambaye ni miongoni mwa

waanzilishi wa mambo haya ya mitandao na ubunifu, haruhusu watoto wake kutumia simu ya mkononi au *iPad* mpaka watimize miaka 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuzungumza haya maneno kuwakumbusha Wabunge wenzangu juu ya jukumu tulilonalo la kuwalinda watoto wetu na kizazi kitakachofuata. Sisi tulioko hapa ndani ya Bunge hili na hata walioko nyuma yangu na walioko nje, ni matunda ya wazazi wetu waliyowekeza kwetu ndiyo maana sisi leo ni Watanzania bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu tunawa-*expose* watoto wetu sana kwenye *technology*, wanaachwa watoto muda wote wanatumia simu, muda wote wanatumia *iPad* na wanatengeneza *addiction* au uraibu wa vyombo hivi. Nimesoma utafiti unaonesha ya kwamba uraibu wa *cocaine* na uraibu wa *technology* ni vitu vinavyofanana, vyote vinadhibitiwa na *hormone* inatwa *dopamine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtakubaliana nami ni kwamba juzi ilivyotokea kashikashi ya mtandao, mimi ni miongoni mwa watu ambao nilikuwa na hali mbaya. Nilikuwa najisikia vibaya, najisikia nimekasirika, najisikia sina raha kwa sababu hakuna mtandao. Watu wote walikuwa na *frustration* kwa sababu tu mtandao umekatika, *dopamine* inatusumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachokiomba, sisi kama Watanzania, kama wazazi wa Kitanzania tuwalinde watoto wetu na dhana ya mambo haya. Tukiwa-*expose* watoto sana kwenye mitandao hatutakuwa na Watanzania bora siku za kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nazungumza leo wazazi wa Buchosa wanisikilize na wazazi wa Tanzania wote wanaosikia wanisikilize. Tufanye *responsible parenting,* ulezi watoto wenye kuwajibika, usiwaache watoto wako watumie sana *technology*, waruhusu watoto wako watumie *technology* wakati wa kufanya *homework* na wakati wa kufanya kazi za shule. Mama au baba adhibiti simu. Siyo kila mtoto akilalamika kidogo tu, amenunuliwa *iPhone 14* unadhani kwamba ni sifa. Tunawaharibu watoto wetu, hatutakuwa na Watanzania bora siku za kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Serikali naomba nitoe ushauri ufuatao. Serikali i-*invest* kwenye elimu, i-*invest* kwenye kuelimisha watu kuhusu madhara ya *technology* kwa watoto wetu, lakini pia ihakikishe ya kwamba mashuleni walimu wanalazimika kudhibiti matumizi ya simu. Katika kadhia hiyo naomba tufanye ili kuokoa kizazi kinachofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili mimi ni mwanahabari kama Dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya alivyoongea, kuna hali mbaya sana kwenye vyombo vya habari leo, hali ya vyombo vya habari ni mbaya, wafanyakazi wanashindwa kulipwa mishahara. Hali ni ngumu sana. Labda kama Serikali imeamua kwamba acha vyombo vya habari vife ili tufanye mambo yetu sawa sawa. Hakuna maendeleo bila vyombo vya Habari. Hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni kitu kimoja tu. Ushauri wangu kwa Serikali na Mheshimiwa Waziri unisikilize. Kila Wizara katika nchi hii ina Kitengo cha Habari, naomba bajeti ya Wizara iwe inatenga walau asilimia moja ya bajeti yake iende kwenye Idara ya Habari. Asilimia moja hii ikienda kwenda Wizara ya Habari, mwisho wa siku itaishia kwenye vyombo vya habari, wataishia kulipana mishahara na vyombo vya habari vitaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi vyombo vya habari hatuhitaji ruzuku ya Serikali. Ruzuku ya Serikali ikija kwetu mtatufunga mdomo, haturuhusiwi kufanya biashara na Serikali na vyombo vya habari vya Serikali vijitoe kwenye matangazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekekani *ITV* wapambanie matangazo na *TBC,* siyo sahihi. *BBC* ya Uingereza haichukui matangazo kwa sababu inapata ruzuku ya Serikali. *TBC* wanapata ruzuku, waache kushindana na vyombo vya habari binafsi. Tukifanya hivi, nina uhakika kabisa vyombo vya habari vitakuwa na nguvu na vyombo vya habari hivi kwa uhakika vikiwepo katika nchi yetu vitasaidia sana kupeleka Taifa letu mbele. Vyombo vya Habari, ni *watchdog*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho *(digital economy)* uchumi wa kimtandao. Ameongea rafiki yangu Kingu nimemsikia, lazima *digital* ichangie kwenye pato la Taifa tuko nyuma sana. Nchi hii ina vijana wengi sana wabunifu, lakini wanakosa mitaji. Nimeshaizungumza mara nyingi, nazungumza tena leo ya kwamba tuanzisheni *National Innovation Fund* ili kuwe na fedha za kuwasaidia wabunifu wa Taifa hili. Nimeshaizungumza, hatufanyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wanayo *Innovation Fund,* Ethiopia wanayo, na *South Africa* wanayo. Kuna shida gani sisi kuanzisha *National Innovation Fund*, tukawa tunachangia mfuko huu ili vijana wetu wenye ubunifu wasaidiwe na mfuko huo kufanya *research* na *development* ya bidhaa zao na kufanya *mass production* ya bidhaa zao? Hatuwasaidii wabunifu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwepo kijana mmoja hapa alianzisha MaxMalipo, najua mtamkumbuka; MaxMalipo ikawa *very successfully,* lakini fuatilia historia yake, ilipata *frustration* ya sisi wenyewe na ikafa. Tunanufaika na nini tunapoua *talents* za vijana wetu? Nataka sisi kama Serikali tuwe watu wa kwanza kuwasaidia vijana wetu waweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya jambo hilo, nataka kuwahakikishia Watanzania kwamba nchi yetu itapiga hatua na maendeleo yatakuja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili…

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulenge jiandae Mheshimiwa Neema Kichiki.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote

niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anatamani Wizara hii kuendelea kuwa Wizara wezeshi kwa manufaa makubwa ya Taifa letu na kuboresha huduma katika jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikiliza Mheshimiwa Rais siku moja akisisitiza kukamilika kwa namba zile za kidigitali, *digital identity number* ili Taifa letu liweze kunufaika na uchumi wa kidigitali. Inaonesha dhahiri shahiri dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha Taifa hili linanufaika vema na Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeze watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Waziri wetu kaka yetu, Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Naibu Waziri pale *Eng.* Maryprisca kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nawapongeza, nimeona wametuletea hapa *robot* ile, ni jambo kubwa. Wengine inawezekana tulikuwa hatujawahi kuona *robot,* kwa hiyo, nawapongeze sana kupitia Tume yenu ya TEHAMA, tumeweza kupata *robot* lile hapa Bungeni ni jambo zuri la kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona akina Mheshimiwa Ulega walituletea *protein* hapa kwa maana ya nyama kwa maana ya samaki na ninyi leo mmetuletea *robot*. Nikukumbushe kaka yangu Mheshimiwa Nape, *robot* lile litaondoka lakini nyama na samaki Wabunge walichukua. Nanyi mwone namna ya kuleta zile *home Wi-Fi* kwa Wabunge ili Wabunge nao wabebe wakajionee umuhimu wa hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niseme kwamba Wizara hii kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameongoza, hii ni Wizara wezeshi kwa maana ya kuhakikisha mifumo yetu katika taasisi mbalimbali inakuwa bora na kuweza kurahisisha huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo umeshudia juzi tulipokuwa hatuna mitandao ilikuwa ni *chaos* kubwa katika taasisi mbalimbali za Serikali, lakini kwa wananchi mmoja mmoja, tumeona shida ilivyokuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba niliwahi kuzungumza hapa katika hotuba iliyopita kuhusu umuhimu wa uimara wa mifumo yetu ya TEHEMA kujikinga dhidi ya mashambulio mbalimbali, vilevile na kujinga na upotevu wa *data*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *CAG* ya mwezi wa Tatu ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya mifumo ya TEHAMA taarifa ile imeonyesha ni Taasisi nne tu Serikalini ndizo ambazo zimeweza kuwa na mifumo ambayo inafuata sheria na miongozo ya mitandaoni kwa maana ya *e-Government. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, 82% katika taasisi 22 zilizofanyiwa ukaguzi na Mdhibiti zote zimeonekana duni kabisa katika uimara wa mifumo yetu. Hii maana yake ni nini? Maana yake bado kuna shida ya ubora wa huduma zinazotolewa katika taasisi zetu za Serikali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nimkumbushe kaka yangu Mheshimiwa Nape pamoja na Watendaji wa Wizara hii, tuone umuhimu wa kuhakikisha mifumo inakuwa na udhibiti wa kutosha kuhakikisha kwamba *data* hazipotei, lakini kujikinga na kushambuliwa na mashambulio mbalimbali mitandaoni. Nilionesha mifano hai hapa mara yangu ya mwisho nilipochangia, nchi mbalimbali ambazo zilivamiwa na mashambulio yale mitandaoni ikiwepo Marekani yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kuna umuhimu na haja kubwa ya sisi kuongeza nguvu katika eneo hili ili kuhakikisha mifumo inakuwa imara. Leo tu unaweza ukaenda unataka *license* ya biashara unaambiwa mfumo uko chini, unahangaika muda mrefu, unataka kulipa kodi ya Serikali mifumo iko chini, maana yake tunapoteza fedha nyingi kwa namna ambavyo mifumo yetu haipo imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kuipongeza Serikali kwa suala zima la kuhakikisha linataka kukuza uchumi wa kidigitali kwa vijana kwa kupitia ule mradi wa Tume wa TEHAMA, kwa maana ya kwamba kutaanzishwa zile *ICT hubs* na Mkoa wetu wa Tanga ni miongoni mwa Mikoa ambayo itanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwani 83% ya fedha ambayo ilitengwa kwenye Tume ya TEHAMA iliweza kutolewa. Natamani kuona sasa pale Tanga *La Casa Chika* kile kituo kinaanza kufanya kazi na vijana wa Tanga waweze kutumia uchumi wa kidijiti, waweze kufanya biashara kwa kutumia TEHAMA. Jambo hili kwa hakika Serikali yetu kama tunatamani kweli kukuza vijana kidijiti na kuhakikisha wanafanya biashara kwa kutumia TEHAMA ni katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana katika eneo hili tujitahidi kuhakikisha miradi hii inakamilika na inaweza kushuka kule kwenye wilaya kwa sababu shida kubwa kwenye uchumi kwa vijana ni mtaji. Kama *laptop* moja tu ya shilingi milioni ipo hata moja, kijana anaweza kujiajiri, kutengeneza vifaa mbalimbali, nafikiri ni hatua nzuri sana ambayo kama Taifa tunapaswa kuisimamia kwa karibu ili vijana wetu waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kupitia *laptop* moja unaweza kuanzisha *small enterprise* ya kidijiti. Ni namna nzuri ambayo Mheshimiwa Rais ameiona kupitia Wizara hii ya kuhakikisha inawakwamua vijana kiuchumi. Naomba sana Serikali isisitize mradi huu. Kama ni mradi wa kimapinduzi kwa vijana huu ni mradi namba moja Tanzania. Tusikae nyuma kuuchelewesha mradi huu. Fedha zitengwe ili vijana wa Taifa letu waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Kichiki, wajiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anafanya ya kuendeleza kukuza nchi yetu kupitia Sekta hii muhimu, lakini zaidi namna ambavyo anaweka jitihada za kuimarisha Tanzania ya Kidijiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na muda nitachangia katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ningependa sana kuipongeza Serikali chini ya usimamizi mahiri sana wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambao ulifanyika Aprili, mwaka huu 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kubwa sana na jambo la kupongeza, lakini nitumie fursa hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie zile Kanuni za Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ili kuhakikisha ya kwamba pia kutakuwa na ulinzi wa matumizi hasi ya akili mnemba *(artificial intelligence)* hususan katika kipindi cha uchaguzi. Kwa maana wengi tunafahamu kati ya wahanga wakubwa wa mambo ya ukatili wa kijinsia mtandaoni ni wanawake ikiwemo wanawake viongozi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Nape jambo hili aliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Napenda kuishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo inafanyia kazi maoni yetu Wabunge, inatupatia nguvu zaidi ya kuweza kuendelea kushauri Serikali kwa tija. Nasema hivi kwa sababu mwaka jana 2023 katika bajeti ya Wizara hii, nilishauri Serikali ione namna ya kuhamisha Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)* kutoka kwenye Ofisi ya Rais, Utumishi na ije kwenye Wizara hii ambayo inasimamia masuala ya TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Nape kwa kuibeba hoja hii na

hatimaye sasa *eGA* imehamia kwenye Wizara hii ambayo ina dhamana ya TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii kumshauri sana Mheshimiwa Waziri Nape kwamba sasa tumefanya jambo jema kuhamisha *eGA* kuileta chini ya Wizara yako. Tunatambua chini ya Wizara yako sasa kutakuwa kuna *eGA* pia kutakuwa na Tume ya TEHAMA. Ni dhahiri kutakuwa na maeneo ambayo vyombo hivi viwili kutakuwa na mwingiliano. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri weka jitihada za haraka tuletee hapa Bungeni Sheria mbili zinazosimamia *eGA* na Sheria inayosimamia Tume ya TEHAMA ili tuhakikishe tunafanya maboresho ambayo yatapelekea *e-GA* na Tume ya TEHAMA kufanya kazi kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Nape atakapohitimisha hoja yake, atupatie maelezo kuhusu mchakato huu wa kuleta sheria hizi mbili utafanyika lini ili jambo hili liweze kufanyika kwa haraka na tupate tija inayostahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeona katika ziara zake zote anazokwenda nje ya nchi, anatafuta fursa kwa ajili ya vijana wetu wabunifu *(start-ups)*. Pia wageni wa kutoka nje ya nchi wanapokuja hapa Tanzania inawekwa jitihada kubwa ya kuwakutanisha wageni wale na *start-ups* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri ameshasema mara nyingi kwamba inakuja Sera ya *Start-up* lakini bado haijaja. Wewe Mheshimiwa Waziri ni Waziri wa vitendo sio Waziri wa maneno. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utupatie kauli ya kueleweka na ambayo tutaweza kuona kweli utekelezaji wake. Ni lini Sera ya *Start-up* sasa itakuwa tayari? Maana hatuelewi mkwamo? Kwa nini kuendelee kuwa na mkwamo, wakati ajenda hii ameibeba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan? Tusififishe jitihada hizo na kuendelea kukwamisha vijana wetu wabunifu katika teknolojia kwa kuwafanya wakose Sera ya *Start-up* hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea naona jitihada kubwa sana za Serikali kuhimiza *digital economy* (uchumi wa kidijiti) lakini mpaka leo hii bado malipo ya *PayPal* hayaruhusiwi hapa nchini. Ni wakati sasa umefika tuone ni namna gani ambavyo Benki Kuu kwa kushirikiana na Wizara yako Mheshimiwa Waziri Nape, iweze kuruhusu malipo ya *PayPal*. Hii ni kwa sababu vijana wengi ambao wanafanya kazi ya kujiajiri kupitia *digital* na teknolojia, inabidi malipo yao ya *PayPal* yapitie kwenye nchi nyingine ilhali sisi hapa wanashindwa kupitishia malipo yao hapa kutokana tu na kwamba bado tumeamua kuzuia malipo ya *PayPal. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuwa nimeona tunaenda kuandaa Maabara ya *Artificial Intelligence*. Ili Maabara hii ya *Artificial Intelligence* iweze kufanya kazi vizuri, pamoja na sekta nyingine zote ambazo tumezisikia zinakwenda kutumia *Artificial Intelligence*, Sekta ya Afya, Kilimo pamoja na TEHAMA ni lazima tuwe na Sera ya Akili Mnemba *(Artificial Intelligence)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea, Jumuiya ya Afrika *(African Union)* wanaandaa mkakati wa akili mnemba kwa ajili ya Afrika *(Africa Artificial Intelligence Strategy)*. Kwa hiyo, sisi kama Tanzania hatupaswi kubaki nyuma. Mheshimiwa Waziri naomba sana katika orodha ya zile sera na mikakati ambayo unakwenda kuandaa, uweke kipaumbele. Tuwe na Sera ya *Artificial Intelligence* ambayo itatupatia mwongozo katika Taifa letu kwa namna gani tunakwenda kutumia akili mnemba kwa manufaa na kwa namna gani tunakwenda kudhibiti mianya mbalimbali ambayo itatokana na akili mnemba ambayo itakuwa na matokeo hasi, ikiwemo masuala ya utapeli, ulaghai bila ya kusahau ukatili wa kijinsia mtandaoni hususan kwa wanawake viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili hili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Ilikuwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 katika Bajeti Kuu ya Serikali, niliishauri Wizara ya Fedha ishirikiane na Wizara hii ya TEHAMA kuona namna ambavyo wataweza kuanza kutoza kodi ya huduma ya kidijiti kwenye makampuni kama *google, facebook* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kufanyia kazi uamuzi ule. Maana yake mwaka huu mwezi Aprili, *TRA* wametuambia kutokana na uamuzi wa Serikali na sisi hapa Bungeni tulipitisha, tayari Serikali imepata mapato mapya, takribani shilingi bilioni 12.6. Mapato haya mapya yametokana na kwamba uamuzi thabiti wa Serikali kuiangalia Sekta ya Kidijiti kama na yenyewe ni chanzo cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kama ambayo wamesema Wabunge wengine, Sekta unayoisimamia wewe inayo tija kubwa sana na inao uwezo na mchango wa kuongeza pato la Serikali. Ni lazima tuangalie maeneo yote ambayo yanapaswa kulipiwa kodi yaweze kulipiwa kodi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Nape Nnauye na Uongozi mzima wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita, halafu jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ametupatia afya njema na tupo hapa leo. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuisaidia Wizara hii ya Mawasiliano, tumeona pesa zimeongezeka na ubunifu umeongezeka kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Nape Nnauye, hapa niseme nipo *conflicted* kidogo. Unajua, Jumatatu ya wiki hii, Mheshimiwa Nape alikuwa Kiteto na kwa kweli amefanya kazi kubwa sana. Leo nisipomsifia hata wananchi wa Kiteto watashangaa sana. Mheshimiwa Waziri na sisi tulishakubaliana, mimi ni mwanafunzi wako wa siasa halafu wewe ni mwanafunzi wangu wa sheria, si ndiyo bwana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca; Mheshimiwa Rais alikupongeza sana

kipindi kile upo kwenye Wizara ya Maji kwamba, unakwenda sawa na umeletwa huku kwenye minara kuna kupanda milima sana na hiyo kazi utaiweza vizuri sana. Mheshimiwa Katibu Mkuu na timu nzima na Mkurugenzi wa *UCSAF* ambaye kila wakati kwa kweli mimi bila kuzungumza habari za *UCSAF* naona kama sijachangia hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusoma Ripoti ya Kamati nimefarijika sana. Taasisi za Wizara yako Mheshimiwa Waziri zimepongezwa kwa kukusanya pesa nyingi sana, *TCRA* na *UCSAF* karibu 111% na 99.2%. Tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza Wabunge wengi hapa kwamba, sasa duniani tunaenda kwa *digital economy, cashless economy* na tungetarajia kwa kweli Wizara hii iongeze *GDP* yetu. Nadhani nami nakubaliana lakini ni lazima tuwekeze sana kwenye Wizara hii. Nchi zinazofanya vizuri kwenye eneo hili ni kwamba, zimeweka pesa nyingi sana. Tuweke hela nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwekeza kwenye *ICT,* Serikali itakusanya kodi, shuleni huko na sasa tumeenda kwenye mitaala na wanafunzi wanatumia vishikwambi. Sasa bila kupata mtandao imara hata huko hatutafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, mimi nilidhani Wizara hii ndiyo ingepewa hela nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tu-*invest* ili tuwadai tunachotaka. Ni kweli huko duniani siku hizi kuna maeneo ukiwa na *cash* hupati huduma hata za *taxi.* Sasa ili twende huko ni lazima tuwawezeshe hawa ili waweze kututengenezea mifumo ya namna ya kutupeleka huko. Kwa hiyo, siyo shilingi bilioni mia moja na ngapi wanayoomba hapa, *it must be a few trillion.* Kwa kweli lazima tuwekeze hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba mkubwa ule tuliosaini aliokuja Mheshimiwa Rais, minara karibu 758 ulikuwa ni mradi mzuri sana na umegusa karibu kila mahali nchi hii. Mheshimiwa Waziri, kati ya minara 33 ya Manyara 12 ipo Kiteto. Mpaka sasa kati ya ile 12, minara sita imeshaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitaachaje kukusifia kweli *honestly?* Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kinua kwa kweli wamefarijika sana. Niipongeze Kampuni ya Airtel kwa kweli hata nilipokuwa Dar es Salaam *one-time* kuwaambia hebu nioneshení *plan of work* ya minara mnayojenga nyinyi ikoje? Walinipa na walinionesha ushirikiano mzuri sana na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba tu Mheshimiwa Waziri na nilishazungumza hapa, tangu uhuru, Kiteto tulikuwa hatupati Redio Tanzania lakini nashukuru sana katika bajeti yako kati ya wilaya ambazo mmeweka ni Kiteto. Wananchi wa Kiteto watafarijika sana kupata Redio Tanzania waanze kufuatilia mambo ya Taifa lao kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tumezungumza habari ya vyombo vya habari hapa. Ni kweli kuna uhuru wa vyombo vya habari lakini kama vyombo vya habari vinadai huu uhuru sasa uhamie kwenye kulipa haya madeni. Shilingi bilioni 18 nadhani ni kidogo sana. Mheshimiwa Nape wewe huwezi kushindwa shilingi bilioni 18. Mlipe ili sasa uhuru mliowapa wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kulipa haya madeni, sasa uhuru mnawapa halafu hawana pesa! Nadhani hebu mwasaidie. Mimi najua wewe unafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Waziri umetuambia hapa kwamba nchi imetoka kwenye nchi zenye uhuru wa vyombo vya habari kutoka 140 mpaka 94. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi kama Tanzania yenye sifa nyingi sana bado, hebu peleka mbele iende mpaka *digits* chache sana. Tunataka kwa sababu Ilani ya Chama cha Mapinduzi nilikuwa nasoma hapa ukurasa wa 175 wanasema “Habari ni moja kati ya haki za msingi za binadamu, kwa kuwa kila mwananchi anayo haki ya kutoa na kupokea habari.” Kwa sababu ilani imeweka vizuri, nadhani tuendelee tuwapite wengine, nchi yetu iendelee kutamalaki huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wameongea Wabunge hapa, nami nakubaliana kwamba, nchi yetu lazima tuijenge kwa kodi. Ili tuweze kuwa na makusanyo mazuri ya kodi ni lazima tuondoe *cash money*. Tuondoe mikono ya watu kwenye

kukusanya pesa, lakini hilo halitawezekana kama tusipofanya *a proper registration* tukamtambua kila mtu yupo wapi na akalipa *a fair tax.* Kitu ambacho hakiruhusiwi kwenye kodi ni kuleta kodi ambayo ni *unjustified* ama kwa sababu ya ubovu wa mifumo yetu unakuta ni kundi dogo tu fulani ambalo limefanikiwa ku-*register* ndiyo wanabeba mzigo wa nchi hii kama wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi ndio *the most faithful* wanalipa kodi kwa sababu inakatwa huko juu na kwa sababu mifumo ipo. Sasa haiwezekani nchi hii ibebwe na watu wachache. Nadhani hata asilimia zao zingepungua kama *tax base* ingeongezeka. Namna ya kuongeza *tax base* ni ku-*register.* Kila mtu awe *registered,* tulipe *a fair share.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *ICT* ni muhimu sana, lakini ni lazima tuweke pesa. Hatuwezi kutaka hawa au kutaka tupate pesa wakati hatuko kwenye mfumo sahihi. Kwa sababu tulianza na mradi ule wa kuboresha makazi, tuwe na kitambulisho, tukienda huko nadhani mambo yatakuwa sawa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza na Mheshimiwa Waziri, siku moja nikasema huu wizi unaotokea wa mitandao kwa sababu najua tunavyoenda kwenye *ICT* tunakutana pia na *complication.* Huko duniani watu wanakuwa *smart,* wizi unahamia huku kwenye *ICT.* Kwa hiyo, ni lazima tuwe na hapa nataka kuzungumza na kampuni za simu. Kampuni za simu lazima ziwe *cooperative* kwa wateja wao. Pale tunapotoa habari ya kwamba hii namba inanitapeli ama nimekosea pesa imekwenda hapa lazima watoe taarifa ili yule mtu ajue kwamba, ana-*obligation* fulani kwa mteja wake. Tukifanya hivyo nadhani itaongeza ukaribu zaidi kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa nchi nyingine pia hii *ICT* ikiwa nzuri na tukiwa imara kwenye eneo hili, hata nchi nyingine; unajua sasa hivi kutembea na kwenda kununua simu ya shilingi milioni tatu au tano, ule mfumo unaotumika kwenye nchi nyingine mtu analipa *on monthly basis.* Kwamba, unaweza leo ukaenda ukachukua simu na inakatwa kwa mwezi. Hii yote inakuja kama tutaweka *ICT* ikae vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Tuwapitishie bajeti hawa wakachape kazi. Ahsante na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa kisasa wa Taifa letu. Ni muhimu kutengeneza mfumo ambao utawezesha kupata taarifa za fedha ambazo zinapita kwenye mikono ya watu ili kufahamu kiasi cha kodi inayolipwa na kila moja wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumekuwa tukisema tuna watu wachache sana wanaolipa kodi. Tukitengeneza mfumo wa kidijiti, tungejua mashimo yalipo ya upotevu wa kodi kama zipo na kuboresha namna ya kukusanya kodi stahiki kwenye shughuli za uchumi wa Taifa ambayo itasaidia ujenzi wa miundombinu ya maji, afya, barabara, elimu na umeme kwa wananchi wetu wa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania kwa uchache wanamiliki *line* za simu mbili mpaka tano kwa sababu mbalimbali kama zifuatazo: -

(i) Kutokupatikana kwenye maneno yote mitandao ya simu. Unakuta inapopatikana *Vodacom, Airtel* haipatikani vivyo hivyo *Tigo* na *Halotel*.

(ii) Kutotabirika kwa *bundle* za simu na *internet* za makampuni yetu ya simu hivyo wananchi kuhangaika kutafuta unafuu kwa hisia kuwa mitandao mingine imekuwa ikiwapunja kwenye *bundle* wanazonunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo: Kwanza, makampuni ya simu yatengeneze mifumo inayoweza kuingiliana ili ukiwa na *line* moja uweze kupata mtandao kwenye minara ya

mitandao yote ya simu. Pili, *TCRA* na Wizara waimarishe udhibiti ili wananchi wapate uhalisia wa kile wanachonunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naomba Wizara itusaidie kupata mtandao wa uhakika kwenye Kata za Gidahababieg, Hidet, Simbay, Sirop, Gisambalang, Balang'dalalu eneo la Mureru na Marega, maeneo mengi ya Kata ya Gehandu, eneo la Dajameda Kata ya Laghanga, Kijiji cha Wandela kata ya Getanuwas, maeneo mengi ya Kata ya Bassodesh na Mulbadaw.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake mbalimbali katika Taifa letu hususan ustawi wa kijamii, kiuchumi, kisiasa, kidiplomasia pamoja na mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 hadi 2025. Ewe Mwenyezi Mungu umbariki Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Awamu ya Sita katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya mpango huu wa bajeti ya Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Taarifa ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iangalie utaratibu wa kuweka mtandao mmoja wa simu nchini kwa kuwa ujenzi wa minara nchini una gharama kubwa sana. Nayasema haya kwa sababu sote tunajua tulisaini mikataba ya ujenzi wa minara mwaka jana 2023 na katika minara mitatu iliyopangwa kujengwa katika jimbo langu la Mbulu Mjini hatujaweza kujenga hata mnara mmoja mpaka sasa hali inayosababisha hoja nyingi

kutoka kwa wananchi kote nchini na kwa kuwa tukio lile lilifanyika mubashara na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ifanye tathmini ya kina kwenye minara yetu ya *TTCL*, kwani kwa hivi sasa minara yetu inakabiliwa na changamoto ya usikivu. Mfano, kupitia ziara ya Mheshimiwa *Eng.* Andrea Kundo, aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii katika Jimbo langu la Mbulu Mjini ilibainika minara yetu miwili ilikuwa na shida ya usikivu. Kwa kuwa tayari tumeshawekeza, hivyo basi, ni muhimu kufanya tathmini ili kukabiliana na ushindani wa kibiashara na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye anaendelea kuturuhusu kutimiza ratiba zetu za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana kwa moyo wa unyenyekevu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kuendelea kunituma niweze kumsaidia kazi sasa katika Wizara hii ambayo ni Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Viongozi Wakuu wote kwa maana ya Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye kwa namna alivyonipokea kwa mapendo makubwa na moyo wa kunisaidia nami niweze ku-*fit* kwenye viatu vyake namna ameweza kufanya kazi nzuri sana katika hii Wizara. Kuna maboresho makubwa na tunaona namna ambavyo kuna mshikamano mkubwa ndani ya Wizara. Hivyo,

nipende kukushukuru bosi wangu Mheshimiwa Nape, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Menejimenti nzima kwa namna ambavyo wameweza kunipokea vizuri na kunipa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru familia yangu kwa namna ambavyo wameendelea kunivumilia ili niweze kutimiza majukumu yangu yote ambayo nimepewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote tunayafanya ni kwa sababu ya malezi mazuri ya Chama Cha Mapinduzi. Napenda kukishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa namna ambavyo pia kimeendelea kutulea, kutushauri na hata tunaweza kufanya kazi vizuri kama viongozi tunaomsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana sana, kwa moyo mkunjufu kabisa Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo mmeweza kunipa ushirikiano tangu nikiwa kwenye Wizara ya Maji na mpaka sasa nimeingia kwenye Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mmekuwa washauri wazuri, mmekuwa kaka na dada ambao mmekuwa mkisababisha niweze kutimiza majukumu yangu. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru Mheshimiwa Waziri Jumaa Hamidu Aweso, kwa miaka mitatu niliyoweza kufanya naye kazi. Kwa kweli amekuwa ni kiongozi mwenye kupenda kushirikiana na ndiyo maana tukaweza kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia ushauri mbalimbali ulioletwa baada ya Mheshimiwa Waziri Nape kusoma bajeti, kupitia Kamati yetu pendwa, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wote kwa namna ambavyo mmekuwa ni msaada mkubwa wa kuhakikisha tunaendelea kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wote waliofikisha michango yao kwa maandishi na walioongea, tunawashukuru sana. Kwa kweli mmechangia kwa namna ya kutushauri, kwa namna ya kuhakikisha kwamba Taifa linasonga mbele kwa kuona kuwa umuhimu wa Wizara upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kusema kwamba sisi Wizara ya Habari tutaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wawakilishi wa Watanzania huko nje, kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mei mwaka 2023 Mheshimiwa Rais alishuhudia mkataba wa ujenzi wa minara 758 ukisainiwa. Mpaka dakika hii kazi inaendelea vizuri kama alivyoongea Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto pale. Juzi Mheshimiwa Waziri alikwenda Kiteto, mimi niliondoka na Dkt. Chaya tulikwenda Manyoni. Ilikuwa tu ni *sampling* ya kuona namna gani utekelezaji wa hii minara unaendelea. Utekelezaji ni mzuri na wananchi wanafurahi kuona kwamba sasa wanatoka kule gizani na wanakwenda kuwa duniani na wao wanaanza kupata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii minara 758 ninaomba niwatoe hofu kwa namna ambavyo minara yote ilivyokuwa imepangwa inatatekelezwa ndani ya muda na itakwisha ndani ya muda; na ni mkataba wa miezi 24. Tunatarajia ifikapo Februari, 2025 hii minara itakuwa imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa ameendelea kutoa *support* kwenye Wizara yetu. Kwa yale maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge hatukuweza kuwafikia kupitia hii minara 758 Mheshimiwa Waziri Nape kwenye hii hotuba aliyoisoma hapa tuna minara mingine 600, ninampongeza. Hivyo, yale maeneo ambayo hatujaweza kuyafikia, tunatarajia pia kuyafikia. Lengo ni kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuongelea suala la maboresho ya hali ya wanahabari Tanzania. Katika vipindi vyote vilivyopita, Wizara imekuwa ikiendelea kufanya jitihada

mbalimbali katika kuhakikisha kwamba Waandishi wa Habari wanaendelea kuboreka kimaslahi lakini vilevile maeneo yao ya kazi pia yanaendelea kubaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu hapa, Waandishi wa Habari, Wanahabari wa Tanzania, kwa sasa katika Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wanahabari wako salama na watabaki kuwa na maslahi mazuri.

Wanahabari wategemee ustawi wa hali ya juu katika mazingira ya kazi na vilevile wao wenyewe binafsi. Haya yote tunatarajia kuyafanya kwa makusudi kabisa kwa sababu tunafahamu umuhimu wa wanahabari. Hapa juzi tu tumetoka kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari; na ili uhuru wa vyombo vya habari uweze kukamilika ni lazima maslahi, usalama na ustawi wa wanahabari tuuzingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025 ambayo Mheshimiwa Waziri Nape ametoka kuisoma nipende tu kusisitiza kwamba tunatarajia kuhakikisha Baraza Kuu la Wanahabari, Mfuko wa Waandishi wa Habari na Bodi ya Ithibati kwa ajili ya Waandishi wa Habari inaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Nibu Spika, haya yote tutahakikisha kwamba tunayafanya. Lengo ni kuona tunaunga jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuona kwamba tunawajali wanahabari ili waweze kufanya kazi yao vizuri, kwa uhuru na kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametushauri, mimi kwa nafasi yangu kama msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Nape napenda kusema tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Tunategemea kuendelea kuwa na ushirikiano wa karibu ili yote ambayo tunayatamani katika sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari yaweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru na ninasema ahsante kwa nafasi. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. Nianze kwa unyeyekevu mkubwa wa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo mmechangia kwenye mapendekezo ya bajeti tuliyoleta mbele yenu, sina mashaka kwamba tutapitisha kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Wabunge wote waliopata nafasi ya kusimama na kusema. Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Mlaghila, Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Chinguile na Mheshimiwa Condester.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tumeongeza nusu saa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Shigongo, Mheshimiwa *Eng*. Ulenge, Mheshimiwa Neema Lugangira, kaka yangu mwalimu wangu wa sheria Mheshimiwa Olelekaita lakini pia na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawahakikishia, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba maoni mengi ni ushauri ambao niwahakikishie tumeupokea kwa unyenyekevu. Tumeupokea na tutaenda kuufanyia kazi na yale ambayo tutahitaji ushirikiano wa mashauriano na ninyi tutawaona na tutashauriana, kwa sababu yote yaliyotolewa hapa ni kwa nia ya kujenga na kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, niguse vitu vichache sana. La kwanza, ninawahakikishia, kwenye hotuba tuliyoisoma hapa nimeeleza maombi ya fedha tunayoomba na mipango tunayokwenda kuifanya kwa mwaka 2024/2025. Kuna *frameworks* nyingi sana nimezitaja, takribani 14 ambazo tunakwenda kuzikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wasisahau kwamba Wizara hii hasa eneo la TEHAMA imeundwa mwaka 2021. Baada ya kuundwa kazi kubwa ya msingi ni kutengeneza misingi ya kisheria *(legal frameworks)* ili tunapokwenda kufanya hizi kazi tuwe na utaratibu fulani wa kufuata badala ya kwenda kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mnaunda taasisi zitakazosimamia hizo sheria. Ndiyo maana mnaona tulitunga sheria hapa ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, tumeanzisha tume, tumetengeneza kwa mfano nimetaja humu *frameworks* zaidi ya 14 ikiwemo ya *digital economy* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa ni Serikali ya ajabu sana, ningekuwa ni Waziri wa ajabu sana kuwasukuma Watanzania kukimbia kwenye haya mambo ya digitali bila kuwa na *frameworks* ambazo zinatuongoza. Tutagongana, tutalipeleka Taifa letu kwenye hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipokee ushauri wa dada yangu Mheshimwa Sichalwe, nimweleze ukweli, siyo kwamba tumekuwa hatusikii, ila ni kwamba hatuwezi kuwapeleka hawa vijana mahali ambapo hatuna *frameworks* za kisheria. Ndiyo kazi ambayo tumekuwa tukiifanya kwa miaka miwili mitatu hapa tangu Wizara imeanzishwa. Ninataka nimwambie, hawa majirani zetu kutangulia siyo kufika, Tanzania itakwenda mahali pazuri. Tutawafikia na tutawapita kwa sababu wengi wamekwenda bila hizi *frameworks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tuko salama. Vijana wa Kitanzania watuamini na Waheshimiwa Wabunge watuamini. *Frameworks* hizi zikikamilika ziko *loaded* na tumeanza kuzitekeleza, tumeanza kuimarisha taasisi. Tutakwenda vizuri. Niamininini, tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana kwa Bara la Afrika Tanzania ni ya pili kwa usalama mtandaoni. Kwa nini? Kwa sababu hatukurupuki. Tunakwenda hatua kwa hatua na tutafika, tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Eric Shigongo, nami nimekuwa nikisema mara kwa mara kwamba Watanzania, wazazi wa Kitanzania msiwaachie watoto wenu walelewe na mitandao, siyo salama, tunaharibu kizazi chetu. Ndiyo maana hapa nimesema, mwaka huu wa fedha tutakwenda kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama Mtandaoni ili kurekebisha mambo mawili makubwa. Moja, kuwalinda watoto na mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakati wa utunzi wa sheria hii tushirikiane ili tuwalinde watoto wetu kwa sababu kila moja hapa ni mzazi. Hata huko walikoanza wameanza kuzuia watoto wasiingie kwenye mitandao kwa sababu hawako salama. Tuwapeleke kwa *break* tuone namna ya kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kubwa tutakalolileta kwenye hiyo sheria ni namna ambavyo mtandao unavyoweza kutumika kwenye masuala ya ugaidi ili tuilinde nchi yetu. Kwa hiyo, mambo mawili; usalama wa watoto mtandaoni na suala la mambo ya kigaidi. Sheria hiyo tunaileta katika mwaka huu wa fedha tuipitie kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja ya namna ambavyo tunaweza kutumia miundombinu ya mawasiliano ya kampuni tofauti, wakashirikiana kwa ajili ya kutoa huduma. Nchi zote za wastaarabu hizi ndivyo wanavyofanya, nami nakubaliana na ninyi, nimechukua ushauri wenu. *TCRA* wako hapa, wakae na kampuni za simu tulimalize hili jambo. Tupunguze watu kutembea na simu tano, sita au saba, hakuna sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuwa na laini moja ukatumia mnara wowote unaoukuta ilimradi ni mnara wa mawasiliano. Watanzania wanataka ku-*enjoy* huduma. Nakubaliana na ninyi na tutakwenda kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Waandishi wa Habari, wako salama chini ya mikono ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni wakati wake ambapo tumeshuhudia uhuru mkubwa. Tumepanda kutoka nafasi ya 43 mpaka nafasi ya 96 na

ya 97 kwa wakati mmoja, haijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu na yeye ndiye ambaye anatuvuta shati mara kwa mara akisema Nape wapeni uhuru, zungumzeni. Wapeni ulezi badala ya kuwa Polisi wao, na hili linakwenda salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia wanahabari, yale yaliyobaki tulikubaliana. Acha tukamilishe sera, tutakwenda kushughulika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nakubaliana na ushauri kwamba umefika wakati kwenye bajeti tuwe na asilimia fulani iwe inatengwa maalumu kwa ajili ya vyombo vya habari. Maana bila *publicity* hii hamtakwenda. Tutatapa matatizo. Kwa hiyo, ni muhimu tutenge fedha kwa sababu hata hizi fedha zinazodaiwa zilitengwa hawakulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pia ameelekeza na Mheshimiwa Rais ameelekeza. Niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutasimamiana kuhakikisha madeni ya wanahabari yanalipwa ili vyombo vya habari visife. *It is unfair* kwamba tuna vijana wameajiriwa kule. Tusipowalipa maana yake wale vijana watakwenda barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ninyi Waheshimiwa Wabunge na ninadhani kuna haja ya kuwa wakali kidogo hasa wa taasisi ambazo zinaona kama vile hizi huduma ni za bure. Kuna watu wanafanya kazi, kuna watu wanatoka jasho, kuna vifaa vinatumika, kuna uwekezaji umefanyika, kuna kodi zinalipwa. Kwa hiyo, kutowalipa ni uharamia ambao hatuwezi kuukubali. Nakubaliana na ninyi, twendeni tuwalipe tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tumeyachukua, ni ushauri, na hivyo tunaufanyia kazi. Waheshimiwa Wabunge naomba tupitishe kwa kauli moja bajeti yetu. Acheni tukawatengenezee Tanzania ya kidigiti. Ninawaelewa, Wizara hii ndiyo *future* ya nchi. Ninaelewa matumaini mliyonayo, ninaelewa wajibu wetu kwa Watanzania. Tutawapa kile mnachokitaka. Tutawaunganisha, tutahakikisha kwamba wote ambao wako nje

ya mfumo wa uchumi wa kodi wanaingia ili tugawane huu mzigo. Nipitishieni hii bajeti tukawape raha. Nipitishieni hii bajeti tukaitengeneze Tanzania ya kidigiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa unyenyekevu kuwaomba, yale maombi niliyoyaweka mbele yenu kidogo kabisa, nyie nipitishieni nitawaletea matokea makubwa. Mkishamaliza kupitisha, jioni tukutane tucheke pale *Dodoma Carnival*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................Sh. 2,590,316,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa ndiyo sehemu hii ya mshahara, nina watu wawili. Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kimsingi sitaki kushika mshahara wa Waziri, lakini natamani sana kupata ufafanuzi. Tunafahamu kabisa kuwa mitandao ya kijamii ina faida kwa ajili ya maendeleo. Tunajua kuna ndugu zetu wanafanya biashara kupitia mitandao ya kijamii. Tunafahamu kabisa teknolojia hii haiko kwetu Tanzania peke yake na wala sisi siyo kijiji, tunashiriki na dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninatamani kufahamu na ufafanuzi wa usimamizi wa maadili. Mheshimiwa Waziri amezungumzia vizuri maadili ya Watoto, tumemwelewa, na amesema ataleta sheria hapa Bungeni, lakini bado kuna shida ya maadili kwenye mitandao. Kuna watoto, kuna wasichana, kuna vijana wetu wanatuma picha za utupu wakitangaza biashara mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Lugangira amezungumzia hapa kwamba kuna wakati mwingine watu wanasemwa vibaya kwenye mitandao kwa kutumia picha na mambo yasiyokuwa sawasawa. Mimi naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kwamba ni kwa namna gani atasimamia kama Waziri, kuweka katazo kubwa kabisa ili tuone faida kwa upande wa kwanza na kwa upande wa pili pia watu walindwe na kuwa na heshima ya kimaadili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahakikisha kabisa kanuni na taratibu ziwekwe ili kutumia mitandao hii katika utaratibu ulio bora. Naomba mwongozo wa Kiserikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahishwa na *concern* ya Mheshimiwa Mbunge juu ya usalama mtandaoni na maadili mtandaoni. Kwa kweli tukiliachia hivi tutaliharibu Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalihakikishia Bunge lako kwamba, sheria tulizozitunga za kusimamia maadili na usalama mtandaoni zipo na tunadhani kwa sasa zinatosha. Ningeweza

kutoa takwimu hapa, takribani kila siku tunafungia hizo *platforms* mtandaoni, nyingi sana. Kwa sababu ninadhani wakati tunaanza kuingia kwenye ulimwengu huu, watu walivamia wengi sana. Sasa wengine wahajui madhara yake, wengine wamekwenda hivi, wengine wamekwenda hivi. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ilikuwa ni kutunga sheria ambazo tumezitunga vizuri na dunia inatambua kwamba sheria tulizonazo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ni kuzisimamia na sisi tumekua tukichukua hatua ikiwemo ya kuzifunga na kuzikomesha kabisa. Hatua ya tatu ni kuwaelemisha watu wetu. Kuwaambia chochote mnachokifanya mtandaoni hakifutiki, hakibaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliwahi kuwaambia Wabunge hapa hata picha unayoipiga na kuifuta unaiona imetoka kwenye *screen* yako lakini ipo mahali, mtu asikudanganye kwamba imepotea. Kwa hiyo, hakuna kitu utakifanya mtandaoni kisiache alama. Kwa hiyo, kama Serikali tunaendelea kuzifungia, tunaendelea kuelimisha lakini tunaendelea kuchukua hatua kali zikiwemo za kuwafikisha Mahakamani watu wote ambao wanatumia mtandao vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tunayoipata mara nyingi, watu wanaoathirika mtandaoni wanaishia kunung'unika, hawataki kufuata utaratibu wa kushirikiana na mamlaka kuyashughulikia haya matatizo. Ninyi mnajua hapa, imetokea matatizo mtu anakwenda anatukana viongozi wetu, tumekuwa tukishughulika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo nyingine kwenye mtandao, *platform* nyingi hizi msingi wake haupo hapa, zimesajiliwa duniani huko. Kwa hiyo, wakijisajili kule wapo wengine mkitaka ku-*deal* nao lazima m-*negotiate* na mmiliki wa mtandao. Vinginevyo, mkifunga leo *issue* kama *Instagram* ina wafanyabiashara ndani yake karibia milioni saba, kwa hiyo, ukiipiga chini unapiga chini wafanyabiashara milioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachokiomba tuaminini. Tukielimishana, tukiendelea kuwakamata wanaokuwa wakorofi lakini tukiendelea kuwafungia wanaofanya vibaya baada ya muda hali ya mtandao wetu itakuwa salama. Tupitishieni hizi fedha tukaimarishe taasisi zetu tuendelee kusonga mbele, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa lingine sheria na kanuni peke yake hazitoshi, lazima wazazi tuwe na dhamira. Wazazi ni sehemu vilevile ya kuchangia maovu haya. Tunakuwa na urafiki na watoto wetu na tunasahau kuweka maadili kwenye familia zetu. Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sina nia ya kushika shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini Mheshimiwa Waziri wakati anatoa ufafanuzi hapa amezungumza kwamba matarajio ya Taifa letu ni kwenye Wizara hii na kwenye *tax base* ya nchi yetu kama ilivyozungumzwa na wachangiaji wengine. *Tax base* yetu katika watu milioni 61, Watanzania na watu karibia milioni 30, milioni tatu tu ndio wanalipa kodi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa dunia au uimara wa Taifa lolote na maendeleo ya Taifa lolote ni kodi, na ili miradi ya maendeleo iweze kutekelezeka hata iki-*double* mara tatu kwa hapa tulipo ni ukusanyaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa sasa ambao ni *digital economy* kwa maana ya kwamba *cashless economy,* Mheshimiwa Waziri, kwenye Taifa letu bado kuna watu wanaona fahari kutembea na lundo la fedha mfukoni, bado watu wanaona ni fahari kufanya malipo ya *cash*, wakati kuna Taifa ukienda ukitoa *cash* wanakuona wewe ni mtu mgeni kutoka kwenye nchi nyingine; wakati Tanzania mtu kutoa *cash* anajiona ni ufahari zaidi. Wewe ndio Waziri ambaye tunategemea utaisaidia *TRA* kwa sababu katika kauli mbiu yao ya kwamba ukilipa dai risiti imeonekana kwa *some percent* haifanyi kazi vizuri, lakini tukiutoa huu mfumo wetu wa uchumi tukaupeleka kwenye *cashless economy*, mtu hana haja ya kudai risiti. *Automatic* risiti itakuwa imepatikana na Serikali imepata mapato yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, hii *cashless economy* ina *advantage* kubwa sana. Kwanza ni uwazi, pili ni kuondoa rushwa kwa maana ya kuondoa mikono kwenye ukusanyaji wa fedha. Naomba kujua kwa niaba ya Watanzania, ni upi mkakati wa makusudi wa Serikali wa kuiondoa fedha mikononi mwa watu na kuipeleka kwenye *digital economy* ili Taifa letu likusanye kodi vizuri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya kizalendo sana ya Mheshimiwa Sanga. Ni kweli kwamba takwimu zinaonesha, takwimu za mwaka 2023 zilikuwa zinaonesha 79% ya fedha inayozunguka kwenye uchumi wetu ipo *cash*, ipo kwenye mikono ya watu. *It was only 21 percent* ndiyo ilikuwa kwenye mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati ule Bunge lako likafanya uamuzi hapa wa kupunguza baadhi ya gharama ambazo zilikuwa zina-*incur* kwenye kutumia *cashless,* kwa mfano, mnakumbuka tulikuwa na tozo tukaiondoa, tulikuwa na gharama zile za kupitisha *fiber* barabarani tukapunguza, ikaondoa, imeongezeka sana watu wamerudi mtandaoni lakini tumeweka *pillars* tano ambazo hizi tukizikamilisha tutakwenda kwenye *cashless economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hizi huduma ambazo zina-*facilitate cash economy* ziwe *available* ndiyo maana kuna hii minara, tunajenga mikongo ili mtu alipo kokote aweze ku-*access;* pili, ziwe *affordable,* mtu awe na uwezo, atumie kwa bei rahisi; tatu, ziwe na *quality* nzuri, Mheshimiwa Mlaghila alikuwa akizungumza hapa habari ya ubora wa hizi huduma; nne, iwe salama, kwamba anajua nikiingiza hela yangu ipo salama; tano, iwe ina *impact* kwamba hela yangu nikiiweka kwenye mtandao ipo salama na italeta *impact* kwenye maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *infrastructure* ikiwa ipo salama, sheria zipo sawasawa, taasisi zipo za kusimamia inabaki moja ambalo tunajadiliana sisi na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Watanzania waone nikilipa *cash* ni gharama kuliko nikilipa *cashless*. Sasa zipo hatua tunaweza kuchukua na tumekuwa tukishauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, kwamba kama kodi ni *18 percent* nikilipa *cash* nipigwe *18 percent*, nikienda *cashless* nipe nafuu kidogo watu watahama kutoka huku, watakuja kwenye *cashless* na wakishakuja kwenye *cashless* tutaona kila *transaction*, tutakusanya kodi, tutasonga mbele. Kwa hiyo, *it possible*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu hiki kinaafikiwa? Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…..............…Sh.669,444,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*…..........….Sh.27,738,365,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……………..............…….Sh. 375,056,000
Kifungu 1005 - *Legal Service Unit*…………........…….……Sh. 339,016,000
Kifungu 1006 - *Government Communication Unit*…………………….....……..……..Sh. 448,028,000
Kifungu 1007 - *Procurement Management Unit*…………………......………….……Sh. 444,568,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*.......................................................Sh. 429,003,840
Kifungu 2001 – *Communication Division*…………………….......………Sh.1,198,159,296
Kifungu 2002 - *Information Communication and Technology*…………...…………………………Sh. 0
Kifungu 4001 - *Information Services Department*…………….....…....……..Sh.2,534,102,000
Kifungu 4002 - *ICT- Systems Development Services Division*…………........……..…Sh.1,202,318,864
Kifungu 4003 - *Communication Safety and Security Unit*……….........………………Sh.371,756,000
Kifungu 4004 – *ICT – Infrastructure Unit*………...….........………………Sh. 566,530,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 - Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………….........……..…………Sh.67,427,762,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*…………........……………Sh.809,500,000
Kifungu 1006 - *Government Communication Unit*……………………………......….……...Sh.300,000,000
Kifungu 1007 - *Procurement Management Unit*………………………..………........…Sh. 325,000,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*......................................................Sh.1,405,154,000
Kifungu 2001 - *Communication Division*……………..……........…………Sh.12,655,350,000
Kifungu 2002 - *Information Communication and Technology*………………………………..………Sh. 0
Kifungu 4001 - *Information Services Department*……………………........…...Sh.980,000,000
Kifungu 4002 - *ICT- Systems Development Services Division*……………........………Sh.2,741,900,000
Kifungu 4003 - *Communication Safety and Security Unit*………………......….………….Sh. 902,550,000
Kifungu 4004 - *ICT – Infrastructure Unit*…………………........……………Sh. 29,622,678,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. Mheshimiwa Waziri wa Habari na Naibu, Watendaji, Wakurugenzi wote kwa kweli tunawapa pongezi kubwa sana, mnafanya kazi nzuri, shirikianeni na taasisi mbalimbali kuhakikisha nchi inakwenda katika mfumo wa kidunia. *(Makofi)*

Kuna vijana wengi sana wana uwezo mkubwa sana, jaribuni, kawekeni *clinic* ya vijana pamoja na waliopo madarakani wa-*share ideas* ili watazame nchi itakwendaje mbele. Kuna nafasi kubwa sana ya kuboresha mapato kwenye Taifa letu makubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana, bajeti yenu imepita rasmi, nendeni mkafanye kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa niwakumbushe tu, Mheshimiwa Shangazi, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Mnyama anaomba kuwatangazia kushiriki uzinduzi rasmi wa *Simba Executive Network* hapa Dodoma. Tukio hili litafanyika leo siku ya Alhamisi katika ukumbi wa *Midland View Hotel,* Kisasa. mgeni rasmi ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muda ni kuanzia ni saa 12.00 jioni na hakuna kiingilio.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa Tarehe 17 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*